**5 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 5 Mei, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Hati za kuwasilisha Mezani.

### HATI ZILIZOWAZILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, sasa aulize swali lake.

Mbunge wa Iringa yeyote aliyeko huu ndani au Njombe. Mheshimiwa Njalu Silanga kwa niaba yake.

Na. 235

### Hitaji la Soko na Stendi, Makambako

**MHE. NJALU D. SILANGA K.n.y. MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Stendi na Soko la kisasa katika Mji wa Makambako?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Makambako ipo kwenye Mradi wa kupendezesha Majiji, Manispaa na Miji

*(Tanzania Cities Transformation Infrastructures and Competitiveness – TACTIC)* ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Kupitia mradi huo, Mji wa Makambako utajengewa Stendi na Soko la Kisasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Njalu Silanga, swali la nyongeza.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa niulize swali dogo la nyongeza. kwa kuwa Mji wa Makambako ni mji mkubwa unaokuwa kwa kasi na unaunganisha nchi ya Zambia na nchi jirani ya Congo. Ni utaratibu upi wa haraka utakaofanyika kuhakikisha hayo majibu ya Mheshimiwa Waziri yatakamilika kwa muda muafaka ili wananchi wa Makambako wapate huduma iliyo bora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Mji wa Makambako upo katika *Tier III* katika mradi huu wa *TACTIC*. *Tier One,* ndiyo sasa wakandarasi wamepatikana, michakato imekamilika na wanakaribia kusaini mikataba ya kuanza kazi na wale wa *Tier II design* ya miradi ndiyo inafanyika hivi sasa tunavyozungumza, na tayari wale *consultants* wamepatikana. Hii *Tier III* ambayo Mji wa Makambako upo, nayo wanapatikana wataalam kwa ajili ya kuangalia *Master Plan* na *feasibility study* ya mji ule. Kwa hiyo, muda siyo mrefu mradi huu utaanza pale katika Mji wa Makambako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 236

## Ujenzi wa Jengo Jipya la Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga jengo jipya la Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji wa Jengo jipya la Utawala katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Hivyo, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ipo katika maandalizi ya kuanza ujenzi wa Jengo hilo kupitia fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri ambapo katika mwaka wa Fedha wa 2022/2023 jumla ya Shilingi milioni 500 zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imekamilisha maandalizi ya nyaraka za ujenzi wa jengo hilo na kuwasilisha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa ajili ya kuidhinishwa ili ujenzi uweze kuanza kwa kuwa Halmashauri hiyo imepanga kutumia mchoro wao badala ya mchoro ulioandaliwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imetenga pia Shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina swali moja la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa jengo hili la Halmashauri ya Bagamoyo limejengwa toka miaka ya 1970, na sasa hivi linavuja, nyaraka nyingi zinaloa na Mkurugenzi anapata shida kufanya kazi na wafanyakazi wake ambao wako katika maeneo tofauti tofauti: Je, Serikali haioni umuhimu katika bajeti ya mwaka huu kutuongezea pesa kuanza ujenzi huo mara moja, kwa sababu, mapato yetu ya Halmashauri ni madogo sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo linalotumika sasa ni la muda mrefu. Kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, wao wenyewe Halmashauri walitenga fedha, shilingi milioni 500 kwenye mapato yao ya ndani na katika bajeti ya mwaka wa fedha unaokuja vilevile wametenga tena shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Spika, vilevile wao wameenda na mchoro ambao utatumia zaidi ya shilingi bilioni 5.34, lakini mchoro ule uliotolewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ulikuwa una gharama ya shlingi bilioni 2.7 tu. Kwa hiyo, inaonesha wao walikuwa wana uwezo wa kujijengea jengo lao wenyewe na kutenga hizi fedha kwa sababu walichagua mchoro wa ghorofa mbili badala ya ghorofa moja, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 237

**Kuboresha miundombinu ya Shule za Mtapa, Kanani na Wangutwa, Wanging'ombe**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaboresha miundombinu ya Shule za Mtapa, Kanani na Wangutwa Wilayani Wanging'ombe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/2021, kupitia mapato ya ndani, Halmashauri ya Wilaya ya Wanging`ombe ilipeleka shilingi milioni mbili kwa Shule ya Msingi Kanani kwa ajili ya ujenzi wa vyoo. Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali ilitoa shilingi milioni 10 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali imetenga shilingi milioni 75 kwa ajili ya ukarabati katika shule hiyo.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Msingi Wangutwa inaendelea kufanyiwa ukarabati kwa kushirikiana na wananchi. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Serikali ilipeleka shilingi milioni 61.6 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa matundu ya vyoo. Vilevile,

katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, shule hiyo imetengewa shilingi milioni 75 kwa ajili ya kuongeza madarasa matatu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, Serikali ilitoa shilingi milioni 12.5 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vinne vya madarasa katika Shule ya Msingi Mtapa. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 shule hiyo ilipelekewa shilingi milioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Shule ya Sekondari ya Igwachanya kuna boma la bwalo ambalo limejengwa kwa nguvu za wananchi takribani miaka kumi sasa. Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo alipita akaahidi kupeleka pesa, na vilevile Mheshimiwa Bashungwa alipita tena akaahidi kupeleka pes: Je, lini mtapeleka pesa hizo zaidi ya Shilingi milioni 200 ili ziweze kukamilisha bwalo lile la Shule ya Sekondari ya Igwachanya?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Kuna Shule ya Msingi ya Saja, Usuka na Udonja, ziko kwenye hali mbaya sana, miundombinu yake ni chakavu sana: Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba shule zile zinakarabatiwa na kuwa bora kama shule nyingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali lake la kwanza la boma la bwalo katika shule hii ya sekondari ambayo ameitaja Mheshimiwa Neema, Serikali itaendelea kutafuta fedha na kuweka kipaumbele katika kumalizia bwalo hili. Kama alivyosema yeye, ni ahadi ya

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hivyo tutakaa na wataalam wetu kuona tutapata wapi fedha kuweza kwenda kumalizia mabwalo haya.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, la shule hizi za msingi ambazo ni chakavu, Mheshimiwa Mbunge amezitaja; Serikali inaendelea kufanya ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi na ninyi Waheshimiwa Wabunge humu ndani mtakuwa ni mashahidi, kuna zaidi ya Shilingi bilioni 230 ya mradi wa *boost* ambayo tayari fedha zile zimeshakuwa *disbursed* katika shule hizi kwa ajili ya kuanza ukarabati na ujenzi wa miundombinu mipya katika shule hizi za msingi na ni nchi nzima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu, sasa aulize swali lake.

Na. 238

**Hitaji la watumishi na vifaa tiba Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka Watumishi pamoja na Vifaa Tiba katika Hospitali ya Halmashauri ya Ushetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Jimbo la Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuajiri watumishi wa kada za afya. Katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 na 2021/2022, watumishi wa kada hiyo 10,462 waliajiriwa kote nchini. Katika ajira hizo, Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ilipangiwa watumishi 55 na watumishi 25 walipelekwa kwenye Hospitali ya Halmashuri ya Wilaya ya Ushetu. Aidha, Aprili, 2023, Serikali imetangaza nafasi 8,070 za ajira kwa kada za afya ambapo baadhi ya watumishi hao watapelekwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Ushetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Hospitali ya Wilaya ya Ushetu ilipelekewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kupitia Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* na tayari *MSD* wameanza kusambaza vifaa tiba kwenye Hospitali za Halmashauri 67 ikiwemo Hospitali ya Wilaya ya Ushetu. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Hospitali hiyo imepokea shilingi milioni 100 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya macho na meno. Vilevile, Hospitali hii imepokea vifaa tiba kwa ajili ya jengo la Kutolea Huduma za Dharura *(EMD)*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nawashukuru sana TAMISEMI kwa kazi wanazozifanya katika Jimbo la Ushetu. Tumepokea vifaa vya meno na *x-ray,* lakini hatuna wataalamu wa meno na mtaalamu wa mionzi: Je, katika ajira hizi 8,000 tutapatiwa hao wataalamu wa mionzi kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa Jimbo la Ushetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Nina Zahanati ya Bugomba A, Elias Kwandikwa, Bugera, Manungu pamoja na Makongoro, zina watumishi wawili wawili tu, inafika mahali Jumapili na Jumamosi wanafunga kwa ajili ya kupumzika. Katika watumishi hawa 8,000, na hizi zahanati zitapata watimishi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cherehani, swali lake la kwanza la wataalamu wa meno na mionzi, kwa sasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ina timu ambayo inazunguka katika Halmashauri mbalimbali zilizopokea vifaa tiba kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wataalamu wetu kule kuweza kujua namna ya kutumia vifaa hivi vya kisasa vinavyokwenda. Kwa hawa wataalam wa meno na wa mionzi, tutahakikisha kwamba hospitali hii pia inapata wataalamu hawa kwenda kusaidia wananchi wa kule Ushetu.

Mheshimiwa Spika, nikijibu kwenye swali lake la pili, kama ambavyo nimesema kwenye majibu yangu ya msingi, hawa watumshi 8,070 ni katika upungufu uliopo nchi nzima, ikiwepo kule Ushetu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Ushetu nayo itapokea watumishi hawa wa afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kituo cha Afya Nkwenda na Hospitali ya Wilaya ya Kyerwa ina upungufu mkubwa wa watumishi. Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi na vifaa tiba ili kuondoa adha wanayoipata wananchi wa Jimbo la Kyerwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, katika hawa watumishi 8,070 ambao Serikali itaajiri hivi punde, tutahakikisha Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa nayo inapata watumishi hawa. Kwenye vifaa tiba, Serikali ilikuwa imeshatoa shilingi bilioni 34 nchi nzima katika kuhakikisha hospitali hizi za Wilaya zinapata vifaa tiba na tutaangalia pia kama hospitali ya Wilaya ya Kyerwa imo na kama haimo, basi itaingia katika mwaka wa fedha ambao unafuata.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Kata ya Ndanda wananchi walijitolea, lakini pia walishiriki na nguvu ya Ofisi ya Mbunge kwa maana ya Mfuko wa Jimbo, kukamilisha Kituo cha Afya baada ya kupata pesa Shilingi milioni 50 kutoka Serikali Kuu. Sasa hivi limebaki suala moja tu ili iweze kufunguliwa, ambalo ni choo. Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutoa maelekezo kwa *DED* wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, *DC,* wakamilishe choo hicho ili zahanati ianze kutumika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri mbele ya Bunge lako hili kwamba Mheshimiwa Mwambe alishakuja kulifuatilia jambo hili ofisini kwa karibu kabisa. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha anajenga choo hiki kupitia mapato yake ya ndani ili huduma ziweze kuanza kutolewa katika kituo hiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Buyungu, swali la nyongeza

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naitwa Aloyce John Kamamba.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tunaishukuru Serikali kwamba imekamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kakonko, lakini tuna upungufu mkubwa wa watumishi na vifaa tiba. Lini Serikali itapeleka watumishi na vifaa tiba katika hospitali yetu ya Wilaya ya Kakonko? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, Serikali inaajiri watumishi wa afya 8,070, na katika hawa ambao wataajiriwa, Hospitali ya Wilaya ya Kakonko nayo itapata watumishi hawa.

Mheshimiwa Spuika, kwenye vifaa tiba, vilevile Serikali imetenga zaidi ya Shlingi bilioni 34 ambazo zimeshakwenda kwa wenzetu wa *MSD* kwa ajili ya kupeleka vifaa tiba kwenye hospitali za Wilaya mbalimbali hapa nchini na tutaangalia kama Hospitali ya Wilaya ya Kakonko nayo ipo, kama haipo tutaiweka katika mwaka wa fedha unaofuata.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 239

**Kutoa kipaumbele cha ajira kwa vijana wanaojitolea katika Utumishi wa Umma**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa kipaumbele cha ajira kwa vijana wanaojitolea kutumikia katika kada mbalimbali za utumishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, naomba kujibu Swali Na. 239, lililoulizwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliweka mazingira ya kuwawezesha vijana wanaohitimu katika vyuo mbalimbali kujitolea katika Taasisi za Umma kwa lengo la kuwawezesha kujipatia sifa za ziada zitakazowawezesha katika ushindani pindi nafasi mbalimbali za ajira zinapotangazwa. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kifungu Na. 2.1.2 cha Sera ya Menejimenti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Toleo la Pili la Mwaka 2008 na Kanuni D. 6 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 ikisomwa pamoja na Kanuni Namba 12(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022, ajira kwa nafasi zilizo wazi katika Utumishi wa Umma hujazwa kwa ushindani na uwazi kwa kufanya usaili na kupata washindi katika nafasi husika.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nitumie nafasi hii kuwashauri na kuwahamasisha vijana wanaojitolea katika kada mbalimbali za utumishi wenye sifa stahiki, kuomba nafasi za kazi pindi zitakapotangazwa ili waweze kushindana na waombaji wengine wenye sifa stahiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, swali la nyongeza.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, moja, kwa vile wakati tunapitisha bajeti ya Wizara hii, Wabunge wengi ambao ni wawakilishi wa wananchi walionesha haja ya kuiomba Serikali kuwaangalia vijana mbalimbali wanaojitolea kwa jicho la tatu, hasa katika maombi ya kazi, na kwa vile Serikali yenyewe ndiyo imesema kwamba ilitengeneza mazingira haya ili kuwapa *competitive advantage* vijana hawa wanapotoa nafasi za kazi, swali la kwanza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuja na mabadiliko ya hizi sera, kanuni au sheria ili kuweka hii *competitive advantage* kwa hawa vijana pindi maombi ya kazi yanapopelekwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nini sasa kauli au *commitment* ya Serikali kwa vijana mbalimbali waliopo katika vituo mbalimbali vya kazi sasa wakiwa wanajitolea kutoa huduma mbalimbali kwa Watanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu

maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijajibu maswali yake ya nyongeza, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo hajawasahau vijana wake, na kwa kweli anafanya kazi nzuri, na Mwenyezi Mungu atakujalia dada yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo ya ziada aliyoyatoa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ninaunaga naye moja kwa moja, ni kweli Bunge lako wakati linajadili Hotuba ya Bajeti hii ya Wizara yetu ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Wabunge wengi walizungumza sana juu ya jambo la vijana wanaojitolea. Na nataka nirudie tena kueleza kwa kifupi juu ya *commitment* ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikiri kupokea maoni ya Wabunge wote na kwamba tutakwenda kuyafanyia kazi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ninapozungumza leo saa nane kikao cha kwanza kwa ajili ya kujadili jinsi gani Serikali inakabiliana na tatizo la ajira tunakwenda kuanza chini ya uongozi wangu, kwa sababu Mheshimiwa Waziri amenikasimia mamlaka hayo niweze kulisukuma mbele jambo hili la ajira kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwenye swali lake la pili juu ya *commitment* ya Serikali; kwa maelezo niliyotangulia kutoa hapa, ni wazi kwamba Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imejizatiti kuhakikisha kwamba inakabiliana na jambo hili, na tuko bega kwa bega naye Mheshimiwa Rais sisi kama watendaji wake, kuhakikisha kwamba tunakwenda kuli-*address* jambo hili na kulitafutia mwarobaini wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly Ntate.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Serikali; je, sasa kwenye *Ajira Portal* ni lini mtaongeza *key* ambayo itam-*pick* yule kijana ambaye amejitolea ikawa ni sifa ya nyongeza katika kuajiriwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba kurejea tena kwenye maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wakati anafunga mjadala wa hoja ya Wizara yetu wakati wa bajeti. Alieleza na ninaomba ni-*quote* kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alieleza kuwa; Serikali imeyachukua maoni yote yaliyotolewa na Wabunge, na kwamba tunakwenda kuyafanyia kazi na utakapofika muda wa kuwashirikisha Wabunge kama wadau kwa kutoa maoni juu ya mfumo mzuri wa kutoa ajira kwa vijana wetu ambao mawazo mazuri kama haya anayoyatoa Mheshimiwa Mbunge yataingizwa ndani yake, tutakuja kulishirikisha Bunge lako na Wabunge watapata nafasi hiyo ya kueleza yale yote ambayo wanayataka yaingie katika mfumo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji; Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 240

**Ujenzi wa Mradi wa Maji Kutoka Ziwa Victoria – Biharamulo**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza na kukamilisha ujenzi wa mradi wa maji toka Ziwa Victoria kwenda Biharamulo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa Mji wa Biharamulo ni asilimia 86. Katika kupunguza kero ya maji kwa wakazi wa mji huo, Serikali ina mipango ya muda mfupi na mrefu. Katika mpango wa muda mfupi, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa kuboresha miundombinu ya maji Biharamulo, na kazi zinazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa chujio, bomba kuu la urefu wa kilomita 2.8, tanki la ujazo wa lita milioni moja na ununuzi wa pampu yenye uwezo wa kusukuma maji lita laki 120 kwa saa. Utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 65 na unatarajia kukamilika mwezi Juni, 2023 na kuongeza huduma ya maji kufikia asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mrefu, Serikali itajenga mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Biharamulo. Usanifu wa mradi huo umekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2023/24.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, na *especially commitment* ya Serikali kwamba Mradi huu wa Maji ya Ziwa Victoria unaanza katika mwaka wa fedha huu wa 2023/2024. Lakini kama ulivyosema, utekelezaji wa miradi ya maji kwa Biharamulo uko asilimia 65 sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba, umesema mmetuwekea 2.8 kilometa mtandao. Sasa kwa sababu maji yanakuja, naomba ufanye *commitment,* kwa sababu sasa bahati nzuri leo najibiwa na Waziri mwenyewe, angalau uniongezee kilometa tatu nyingine waweze kusambaza mabomba zaidi pale mjini ili maji yatakapofika yawafikie wananchi wengi zaidi. Swali la kwanza hilo, naomba tu *commitment*.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mradi huu wa Maji wa Ziwa Victoria tulikuwa tumeahidiwa pia kutoa maji Ziwa Victoria tupite katika Kata za Nyamigogo, yale Kabindi, Nyabusozi, Nemba yaende Nyantakara yafike mpaka Nyakanazi katika kata ya Lusahunga. Sasa ni lini mradi huu wa kutoa maji za Ziwa Victoria katika *line* hii ya kuyapeleka mpaka Nyakanazi utatekelezwa na Serikali kwa ajili ya wakazi wa Buharamulo na hususan Nyakanazi, *center* kubwa inayokuwa pale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na kipenzi cha Wanabiharamulo, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Nimhakikishie kwamba Wizara ya Maji jukumu letu ni kuhakikisha Wanabiharamulo wanapata maji. Kwa hiyo, juu ya ombi lake la kuongeza mtandao, tupo tayari kutoa

fedha kwa ajili ya uongezaji wa mtandao wananchi wake waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni juu ya ujenzi huu wa mradi mkubwa. Ujenzi wa mradi huu chanzo tunachukua pale eneo la Chato na ni miongoni mwa miradi ya miji 28 na mkandarasi amekwishapatikana, *advance payment* imekwisha tolewa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba safari moja huanzisha mwingine, uanzaji wa mradi huu ndiyo tunakwenda kukamilisha ujenzi wa mradi wa Biharamulo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 241

**Usambazaji wa maji kutoka Mlandizi hadi Mzenga**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatekeleza mradi wa kusambaza maji kutoka Mlandizi hadi Mzenga – Kisarawe?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na usanifu wa kina wa mradi wa maji kutoka bomba kuu la *DAWASA* Mlandizi kupeleka kwenye vijiji 19 vya Wilaya ya Kisarawe vikiwemo vijiji vya Kata ya Mzenga. Usanifu huo unatarajia kukamilika mwezi Agosti, 2023 na ujenzi kufanyika katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza niishukuru Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri hapo, nimefuatilia leo na kupata uhakika kwamba mafundi sanifu wako *site* kwa ajili ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tarafa hii ya Mzenga, na hususan Kata hii ya Mzenga, zikiwemo Kata za Vihingo, Kurui na Mafizi, zina shida kubwa ya maji, licha ya kwamba Serikali mmetoa *commitment.*

Je, ni namna gani Serikali inaweza kutusaidia kwa dharura ikizingatia tumeshapata lile gari la kuchimba visima? Na tunaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikali yetu ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya miradi mingi ya maji Mkoa wetu wa Pwani na Tanzania kwa ujumla.

Je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kuweza kupunguza gharama za kuunganisha maji, hasa vijijini, ili wanawake watumie maji majumbani ili iweze kuleta tija ya miradi mikubwa iliyofanyika? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyowapigania wananchi katika Mkoa wa Pwani. Kubwa ambalo nataka nisisitize ni kwamba Mheshimiwa Rais ametupatia fedha juu ya ununuzi wa mitambo na mitambo tumekwisha

inunua, niwaelekeze watu wa *DDCA* wafike katika haya maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaomba ili tuweze kufanya tafiti za haraka na kuhakikisha visima hivi vinachimbwa wananchi hawa waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, amezungumza juu ya gharama za maunganisho, hasa kwa wananchi kupata maji majumbani. Tumekwishatoa maelekezo katika Wizara ya Maji na watendaji wanalifanyia kazi. Tunataka tuwe na bei elekezi, hasa juu ya maunganisho ya maji majumbani. Kwa hiyo tunalifanyia kazi na tumelipokea kuhakikisha kwamba gharama zake zinakuwa *reasonable* na wananchi waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Magomeni, sasa aulize swali lake.

Na. 242

**Tatizo la watuhumiwa kutopewa dhamana kwa makosa yenye dhamana**

**MHE. MWANAHAMIS KASSIM SAID** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza tatizo la watuhumiwa kutopewa dhamana kwa makosa yenye dhamana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pauline Gekul, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, dhamana katika kesi za jinai ni haki ambayo imewekewa utaratibu wa kisheria. Kwa mujibu wa sheria zetu yapo makosa yanayodhaminika na yapo makosa ambayo hayana dhamana. Kifungu cha 148(5) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Sura 20 kimeainisha makosa yote ambayo hayana dhamana. Hivyo, kwa makosa yote ambayo hayajatajwa na kifungo hicho yana dhamana ambayo ni haki ya mshtakiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, swali la nyongeza.

**MHE. MWANAHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, majibu anayoyajibu Mheshimiwa Waziri, mimi sina, sijayaona kwenye swali langu. Hapa sikuuliza sheria kwa sababu sheria haina matatizo, wale watekelezaji wa sheria ndio wenye matatizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na jibu la msingi ambalo ni zuri kama alivyolieleza Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, wasimamizi wa sheria ni pamoja na Jeshi la Polisi, na huenda dhamana anazozikusudia ni zile ambazo zinatolewa na Jeshi la Polisi lakini watu hawatoki. Jambo la msingi ambalo tumelifanya Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia *IGP* ni

kuwataka *RPCs, OCDs* na wale wakuu wa vituo *(OCSs)*, kukagua mara kwa mara mahabusu zetu na kuona watu waliomo ndani na sababu gani zimesababisha awe ndani ili waweze kuachiwa kama hakuna sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, lakini tumebaini pia kwamba kuna baadhi ya watu wanawekwa ndani hata ndugu zao wanagoma kuwawekea dhamana, na hii ni kwa sababu ya matukio ya mara kwa mara yanayojirudia kiasi kwamba yanafedhehesha jamii. Kwa hiyo, niwaombe pia ndugu wawe wepese kuwadhamini kwa wale ambao dhamana zinakuwa wazi.

Mheshimiwa Spika, tumewasisitiza wakuu wa vituo pale inapowezekana kwa makosa yanayodhaminiwa waweze kutoa dhamana. Na kama Mheshimiwa Mbunge ana jambo *specific,* niko tayari kukutana naye baada ya kipindi cha maswali na majibu ili tuweze kuambiwa halafu tuone ni kitu gani kilichokwama, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona Mheshimiwa Mwanakhamis ameridhika na hayo majibu. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 243

**Ujenzi wa meli Bandari ya Mtwara**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga meli katika Bandari ya Mtwara itakayorahisisha mawasiliano na nchi ya Comoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa mawasiliano baina yake na mataifa jirani, hasa Nchi ya Comoro. Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL),* imetenga fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu *(feasibility study)* katika Bahari ya Hindi kwa lengo la kujiridhisha na kiwango cha mahitaji ya usafiri huo kwa wananchi wa mwambao wa Pwani ya Bahari ya Hindi na nchi jirani ikiwa ni pamoja na Visiwa vya Comoro. Upembuzi huo utasaidia Serikali kuamua aina ya meli itakayojengwa kulingana na hitaji la wananchi na soko kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hiyo ya kufanya upembuzi yakinifu, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imefanikiwa kuishawishi Kampuni ya Meli ya *CMA CGM* kutumia Bandari ya Mtwara kama kitovu *(hub)* cha mizigo inayokwenda Visiwa vya Comoro. Hivyo, mizigo inayotoka Nchi za Ulaya na Asia kwenda Comoro na ile inayotoka Tanzania kwenda Comoro *(transshipment)* imeanza kuhudumiwa katika Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, meli ya Kampuni ya *CMA CGM* ilianza safari za kupitia Bandari ya Mtwara tarehe 20 Aprili, 2023 na itaendelea kutoa huduma hiyo kila baada ya wiki moja. Aidha, meli ya kwanza kutoka Mtwara kwenda Comoro iliondoka tarehe

02 Mei, 2023 na itaendelea kutoa huduma hiyo kila baada ya wiki mbili, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, suala la upembuzi yakinifu limechukua muda mrefu sana, ndiyo kwanza saa hizi Serikali imejipanga kuanza kutenga fedha.

Je, Serikali haioni kwamba ujenzi wa bandari katika mwambao wa Bahari ya Hindi ungerahisisha sana na kupunguza suala la ukosefu wa ajira kwa wananchi wa Tanzania, hususan wa Mikoa ya Kusini ya Mtwara na Lindi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mkoa wa Mtwara unalima mazao ya mihogo, njugu, mbaazi, nazi, mazao ambayo yanahitajika sana kule Comoro. Je, Serikali haioni kwamba kama kungekuwa na meli hii uwepo wake ungechechemua sana uchumi wa watu wa Mikoa ya Mtwara, Lindi pamoja na Ruvuma? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imechukua muda mrefu kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na ulianza tangu mwaka 2019 na 2021. Hii ilikuwa ni kwanza lazima ilitakiwa tujiridhishe – na huu ulikuwa upembuzi yakinifu wa awali – tujiridhishe kiasi cha mzigo utakaotoka Mtwara kwenda Comoro ili

tujue ni aina gani ya mali na ukubwa wake, ambaye Serikali kwayo itakwenda kujenga ama kutengeneza.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, kwa kuwa katika Mwaka wa Fedha ujao tumetenga fedha sasa kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa kina wa mwisho ili tupate uhalisia wa aina gani ya meli hii.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili; Serikali inatambua juhudi za wakulima wa Mtwara, hususan wale wote ambao wanalima mazao mbalimbali. Na kuna kila sababu ya kwamba wawe na meli inayosafirisha mazao yao kutoka Mtwara kwenda Visiwa vya Comoro.

Mheshimiwa Spika, na kwa jitihada hizo, kupitia Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ziara aliyoifanya Ufaransa, ndiyo maana meli hizi sasa zimeshaanza kuja nchini, hususan katika Kampuni ya *CMA, CGM* pamoja na *UFL Express,* maana kwamba Mtwara itakuwa *hub,* na Nchi jirani kama Comoro, *Mozambique* pamoja na Malawi watakuwa wanachukua mizigo pale kwenda maeneo yao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, Mbunge wa Tumbe, sasa aulize swali lake.

Na. 244

**Bajeti ya kukamilisha miundombinu ya nchi**

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK** aliuliza: -

Je, kwa mujibu wa *master plan* ya miundombinu ya barabara Tanzania, tunahitaji fedha kiasi gani kukamilisha miundombinu hiyo?

**SPIKA:** Mheshimwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, Mbunge wa Tumbe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* inasimamia mtandao wa barabara wenye urefu kilometa 36,760.29, kati hizo kilometa 12,223.04 ni barabara kuu (Trunk Roads) na kilometa 24,537.25 ni barabara za mkoa *(Regional Roads)*. Kati ya kilometa 36,760.29, kilometa 11,587.82 sawa na asilimia 31.50 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 25,172.48 zilizobaki ni za changarawe, sawa na asilimia 68.50. Ili kujenga kwa kiwango cha lami kilometa 25,172.48 zilizobaki, inakadiriwa kiasi cha shilingi trilioni 45.3 zinahitajika kwa wastani wa gharama za ujenzi bilioni 1.8 kwa kilometa kilometa moja, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amour Khamis swali la nyongeza.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Spika,ahsante sana, na nimpongeze Waziri kwa niaba ya Serikali kwa majibu mazuri sana, ila nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, hizi kilometa 25172.42 zilizo bakia ambazo zimejengwa kwa changarawe zitajengwa lini kwa lami na zitatumia muda gani?

Swali la pili bajeti hii ya bilioni 1.8 ninavyoamini ni pamoja na kujenga michirizi au mifereji ya maji sasa kuna maeneo ambayo mifereji hii haijajengwa hata hapa Mjini Dodoma; je, ni lini mifereji hii itajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo : -

Mheshimiwa Spika,kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, fedha inayokadiriwa kukamilisha mtandao wa barabara ambazo zinahudumiwa na *TANROADS* ni takribani tirioni 45; na bado barabara zingine zinaendelea kupandishwa daraja kuja, kwa hiyo zitaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika,na Serikali kusema ni lini tunaweza tukakamilisha ujenzi wa barabara zote kwa kiwango cha lami hii itaendelea kuwa ni kazi endelevu kadri fedha inavyopatikana. Kwa sababu, Mbunge atakubaliana nami kwamba bajeti tu ya nchi kwa mwaka ni zaidi ya tirioni 40 kwenda 41 kwa bajeti tunayoitekeleza sasa barabara hizi ni tirioni 45 kwa hiyo Serikali inajitahidi kujenga barabara kadri ya uwezo lakini hasa barabara zile za kipaumbele. Kwa hiyo kadri tutakavyoendelea tunahakikisha tutaendelea kupunguza idadi ya barabara za changarawe.

Mheshimiwa Spika,kuhusu swali lake la pili, ni kweli barabara zinajengwa lakini zingine hazina mitaro, lakini kipaumbele za kuweka mitaro hasa ni barabara ambazo ziko kwenye miji na maeneo ambayo wananchi wako wengi kwa ajili ya usalama. Na changamoto kubwa ambayo tunaipata kwenye uzibaji wa mitaro ni pale ambapo huduma za kijamii zinasababisha ile mitaro inaziba na basi maji hayo yanapanda kwenye barabara na kuharibu zile barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe Mbunge wa Hai sasa aulize swali lake.

Na. 245

**Serikali kufufua jengo la viwanda vidogo vidogo – Lwosaa**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kufufua jengo la viwanda vidogo vidogo – Lwosaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha tathmini ya jengo hilo na kupata gharama za ukarabati wa kukamilisha ujenzi wa jengo hilo ambazo ni jumla ya shilingi 293,986,850. Pia Serikali kupitia *SIDO* inaendelea kufuatilia suala la umiliki wa eneo hilo ili kuanza ukarabati na kumalizia ujenzi. Aidha, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati na kukamilisha ujenzi wa jengo hilo ili shughuli kusudiwa zianze kufanyika kwa manufaa ya wananchi wa Lwosaa na Taifa kwa ujumla. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba eneo hili limepimwa na lina hati ya Kijiji kwa ajili ya shughuli hiyo, na tayari Katibu Mkuu alitembelea eneo hili kwa hiyo hakuna mgogoro wowote wa umiliki.

Swali langu, kwa kuwa ujenzi huu umesimama tangia mwaka 1974 na sasa ni miaka 47 haujaendelezwa; je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi?

Swali la pili, kwa kuwa kuna kiwanda cha aina hiyo hiyo kimejengwa kata ya Rundugai na kimefadhiliwa na mradi wa *TASAF*; je, hatuoni iko haja ya Serikali kuchukua na kukiweka chini ya *SIDO* ili kiweze kutoa huduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana; kwanza niwapongeze sana wananchi wa Jimbo la Hai kupitia Mbunge mahiri, ndugu yangu Saashisha Mafuwe kwa ufuatiliaji lakini pili kwa kutenga haya maeneo mahsusi na kuanza ujenzi wa jengo hilo ambalo ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya Viwanda.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie wana- Hai na hasa wana-Lwosaa kwamba sisi kama Wizara tutahakikisha tunaendeleza jitihada hizi za wananchi katika kujiwekea maendeleo kupitia *SIDO* na taasisi zetu nyingine kuanza kukamilisha jengo hilo. Kama umiliki sasa ukihamishiwa kwenda *SIDO* maana yake tutakuwa na ule uhakika wa kuendeleza na kuwekeza zaidi katika ujenzi wa jengo hilo na kukamilisha kama ambavyo tumesema kwa sababu tathmini imeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini pili na hili jengo lingine ambalo katika kata hiyo mpya Mheshimiwa Mbunge amesema nalo sasa wakati wanakuja kufanya uhamisho wa umiliki wa eneo hili la Lwosaa nawaagiza *SIDO* watembelee na kukagua pia jengo hili ili nalo tuweze kuliwekea katika mipango la kuliendeleza na kuwajengea wananchi hawa chuo cha ufundi kupitia *SIDO* katika Jimbo la Hai.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wengine wote na sisi wananchi tutenge maeneo kwa ajili ya maendeleo ya viwanda pamoja na masoko kwa ajili ya kujiletea maendeleo kupitia *SIDO* na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Stella Simon Fiayo Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 246

**Hitaji la Gari la Zimamoto – Songwe**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kununua Gari la Zimamoto katika Mkoa wa Songwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Songwe lina magari mawili ya kuzima moto. Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe Wilaya ya Mbozi Mji Mdogo wa Vwawa kuna gari moja aina ya Fuso yenye namba za usajili ZT 0014. Gari hilo linaujazo wa lita 1,500 za maji na lita 500 za *foam*. Katika Wilaya ya Tunduma kuna gari moja aina ya Mitsubish Canter yenye namba za usajili STL 4914 na lina ujazo wa lita 1,200 za maji.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Serikali itaendelea kuliimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kuliongezea wataalam na vitendea kazi ikiwemo magari ya kuzima moto na uokoaji kwa Mkoa wa Songwe kwa madhumuni ya kuzifikia wilaya zote kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Simon Fiayo, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mkoa wa Songwe una halmashauri tano na magari yako katika halmashauri mbili ambayo ni halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na Halmashauri ya Mji wa Tunduma, lakini kuna halmashauri ya Ileje, Momba na Songwe mpaka sasa hayana magari ya zimamoto.

Je, mnatumia njia gani kukabiliana na majanga ya moto yanapotokea katika Wilaya hizi?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa magari yaliyopo katika Wilaya ya Halmashauri ya Mbozi na Halmashauri ya Mji wa Tunduma ni magari madogo hayana uwezo mkubwa wa kukabiliana na majanga makubwa ya moto.

Je, ni lini mpango wa Serikali kuhakikisha wanaleta magari makubwa na ya kisasa kwa akili ya kukabiliana na majanga ya moto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua uwepo wa Halmashauri tatu za Wilaya ambazo hazina magari, na ndiyo maana kwenye jibu la msingi nimesema tunaendelea kuliwezesha Jeshi la Zimamoto hatua kwa hatua kutegemea upatikanaji wa fedha. Hata hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wabunge wa majimbo, akiweno Mwenisongole amewasiliana na Wizara kwa kaaribu na Mkuu wa *Fire* nchini na tumewaahidi kuwapa gari moja hata kabla ya magari ambayo tuna *plan* kununua hatujanunua.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu uwezo mdogo wa magari tunatambua, ndiyo maana kwenye bajeti ijayo ambayo tutaleta

tuombe Bunge lako lituhidhinishie ipo bajeti ya kununua magari makubwa na kadri yatakavyokuwa yananunuliwa tutakuwa tunapeleka kwenye Wilaya zenye changamoto zikiwemo hizo Wilaya za Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru watu wa Songwe, kwenye wilaya tatu alizozitaja hakuna matukio ya mara kwa mara ya majanga ya moto yanayohitaji uokoaji. Tunashukuru kwamba elimu ya zimamoto na wokozi wanaizingatia wananchi wa Mkoa huo. Ahsante**.**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Hapo mwishoni umezungumza kuhusu maeneo ambayo yanapata majanga ya moto mara kwa mara. Mbeya Jiji hakuna gari la Zimamoto na majanga ya moto yapo kila wakati. Kwa hiyo pelekeni gari.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir Mbunge kutoka Baraza la wawakilishi sasa aulize swali lake.

Na. 247

**Kuimarisha utalii wa ndani nchini**

**MHE. AMEIR ABDALLAH AMEIR** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha utalii wa ndani unaimarika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa niaba ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utaii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika; katika kuhakikisha utalii wa ndani unaendelea kuimarika nchini, Wizara inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukuza utalii wa ndani ikiwemo:-

i. Kuwa na huduma bora zenye gharama nafuu kwenye vivutio zikiwemo malazi, chakula, usafiri na viingilio;

ii. Kuendelea kuhamasisha makundi mbalimbali ya kijamii ikiwa ni pamoja na wanafunzi, wajasiriamali, wafanyakazi na makundi maalum kutembelea maeneo ya vivutio vya utalii na pia kufanya mikutano; na

iii. Kuendelea kutoa elimu kwa umma na kutumia chaneli maalum *(Tanzania Safari Channel)* ya kutangaza utalii kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii pamoja na kuhamasisha wananchi kutembelea vivutio hivyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuongeza maeneo ya utalii, kuibua vivutio na mazao mapya ya utalii na kuendeleza miundombinu ya utalii katika kanda zote za utalii nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir, swali la nyongeza.

**MHE. AMEIR ABDALLAH AMEIR:** Mheshimiwa Spika,ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningeomba kuuliza masuala mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tuna maeneo ambayo yana vielelezo vya kihistoria kati ya Tanzania bara na Tanzania visiwani yanayo shabihiana; kwa mfano hatuwezi kuzungumza biashara ya utumwa tukaielezea sehemu moja ina elezeka sehemu zote mbili wanahistoria Dkt. Livingstone.

a) Je, Wizara yako sasa inaampango gani wa kuyahuisha maeneo haya yenye vielelezo vya kihistoria vinavyotegemeana ili sasa kuusaidia utalii wetu wa ndani kukua zaidi kimapato?

Mheshimiwa Spika, kutokana na mtikisiko wa Uviko 19 tumeona kwamba utalii wetu wa ndani kidogo uliyumba;

b) Je, Wizara sasa ina mpango gani wa mikakati mipya na imara ukiachia mbali hii ya kawaida unayoelezea ya kuweza sasa kuufanya utalii wetu wa ndani uweze kujitegemea angalau kwa asilimia hamsini kwa hamsini, huku ukizingatia kwamba tunapoboresha vya kutosha Tanzania kutokana na ongezeka la watu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ipo mikakati kabambe ambayo imeshaandaliwa na Serikali kuhakikisha kwamba tunaendelea kutunza maeneo haya ya kihistoria. Moja ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kuyatunza maeneo hayo yenyewe ili lengo na madhumuni sasa tuweze kuvutia watalii wengi; lakini cha pili kuendelea kufanya utafiti kwa sababu tunachoamini kwamba bado yapo maeneo ya vivutio vya watalii inawezekana bado

hatujayavumbua yakiwemo maeneo ya kihistoria ya hiyo historia utumwa na vitu vingine. Sasa kuendelea kuyatangaza, kwa sababu kuwa nayo na kuyavumbua ni suala moja lakini kuendelea kuyatangaza ili walio nje na ndani ya nchi yetu waweze kutambua wapi wanaweza wakajifunza na wakapata kujua hiyo historia.

Mheshimiwa Spika, swali lingine, ni nini sasa matarajio yetu, Matarajio yetu ni kuhakikisha kwamba tunaongeza idadi kubwa ya watalii kutoka idadi tuliyo nayo kuendelea idadi kufika hata watalii milioni tano. Lengo na madhumuni ni kuongeza sasa mapato ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kufikia hayo matarajio kwanza tuhakikishe kwamba tunatoa elimu kwa wananchi ili waweze kutambua umuhimu wa utalii wa ndani, lakini cha pili kutoa huduma bora hicho tumekipanga ili lengo na madhumuni wanapo kuja kujifunza waweze kupata huduma bora.

Mheshimiwa Spika,nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, sasa aulize swali lake.

Na. 248

**Kero ya nyani, tumbili na ngedere kwa wananchi wanaopakana na Mlima kilimanjaro**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua kero ya nyani, kima, tumbili na ngedere kwa Wananchi wanaopakana na Mlima Kilimanjaro?

**SPIKA:**Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu suali la Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro ina vituo vya askari wanyamapori kwenye Wilaya zote zinazopakana na Hifadhi, ambapo Moshi kuna vituo vinne, Rombo kuna vituo vitatu, Hai kuna kituo kimoja, Siha kuna kituo kimoja na Longido kuna vituo viwili. Vituo hivyo vina askari wa Jeshi la Uhifadhi ambao kwa kushirikiana na maafisa wa wanyamapori kutoka wilaya husika wamekuwa wakifanya kazi ya kuwafukuza wanyamapori wakali na waharibifu pindi wanapovamia makazi ya wananchi au mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini wanaopatwa na madhara ya wanyamapori, wakiwemo nyani, kima, tumbili na ngedere na kadhalika kutoa taarifa kwa askari wa uhifadhi wa vituo hivyo pale wanyamapori hao wanapoingia kwenye maeneo yao ili waweze kudhibiti wanyamapori hao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK ALOIS NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, Nakushukuru kwa kunipa tena fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Je Serikali ina mpango gani wa kushirikisha jamii ya vijiji vyote vinavyozunguka mlima Kilimanjaro ili kutunza rasilimali ambazo zipo katika mlima huo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Maporomoko ya Materu au Materu *water falls* iliyopo katika mto Kware katika viunga vya Mlima Kilimanjaro ni kivutio kikubwa cha watalii;

Je, Serikali ina mpango gani kusaidia juhudi za wananchi katika kuboresha maporomoko hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Patrick Alois Ndakidemi Mbunge wa Moshi Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, namna gani tunaweza tukawashirikisha wananchi; Ushirikisho wa kwanza ni kuendelea kuwapa elimu, kwa sababu tunaamini kwamba moja ya miongoni mwa mambo ambayo yanaweza yakahifadhi hili eneo au yakatoa huo ushirikiano wa kuwashirikisha wananchi au wanakijiji ni kuendelea kuwapa taaluma.

Mheshimiwa Spika, lakini cha pili ni kuanzisha na kuendeleza vikundi shirikikishi. Vikundi ambavyo vitasaidia katika kulinda haya maeneo. Lakini kingine, tumeona moja miongoni mwa njia ya kuweza kunusuru maeneo haya ni kuhakikisha kwamba tunawasisitiza wananchi wanaendelea kupanda miti kwa wingi. Kikubwa zaidi tunaendelea kuwaomba wananchi wa maeneo yale waache kufanya shughuli za kibinadamu katika maeneo yale ya Mlima Kilimanjaro, zikiweno shughuli za Kilimo, shughuli za ukataji miti lakini mwisho wa siku wanakwenda kuchoma miti pale

na hatimaye inapelekea majanga makubwa. Kwa hiyo hiyo ni sehemu kubwa ambayo tumeichukua kama hatua ya kuwashirikisha wanakijiji.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili katika suala la kuboresha na kutunza hichi chanzo cha maji cha Materu *Water Falls*, cha kwanza tunaendelea kutoa elimu kama kawaida yetu kwa sababu tuna amini elimu ndiyo itakayokitunza kile chanzo. Cha pili tumesisitiza watu waendelee kuipanda miti pale kwa sababu kisayansi miti ile ndiyo inayokwenda kuvuta mvua ile na tayari kile chanzo kina imarika. Kikubwa tunaendelea kusisitiza Wananchi wasifanye shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya vyanzo vya maji mwisho wa siku wanaharibu hivyo vyanzo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 249

**Hitaji la Malambo ya Mifugo-Nkasi**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga malambo ya kunyweshea mifugo katika Kata ya Chala, Kate, Myula na Nkandasi Wilayani Nkasi?

**SPIKA:** Mheshimiwa

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto ya upungufu wa maji kwa ajili ya mifugo katika Kata za Chala, Kate, Myula na Nkandasi, Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024, imepanga kufanya tathmini ya miundombinu ya maji na usanifu utakaowezesha kujenga malambo au kuchimba visima virefu katika maeneo hayo. Matokeo ya tathmini hiyo yataiwezesha Serikali kujenga miundombinu hiyo kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa changamoto ya uhaba wa maji kwa ajili ya mifugo, nazikumbusha Halmashauri za Wilaya nchini kutekeleza Waraka wa Rais Na.1 wa mwaka 2002 kuhusu kutenga asilimia 15 ya mapato yatokanayo na Sekta ya Mifugo ili kujenga na kukarabati miundombinu ya maji. Pia, nitoe wito kwa wafugaji na wadau wengine kuwekeza kwenye ujenzi wa malambo au kuchimbaji visima virefu

**SPIKA:** Mheshimiwa Vincent Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Nkasi Kusini lina idadi kubwa sana ya mifugo na wananchi wa Kata ya Ntuchi pamoja na Chala wameshaandaa maeneo ya ujenzi wa majosho. Je, ni lini Serikali itakuja kujenga majosho hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, natambua kazi kubwa anayoifanya katika ufuatiliaji wa kuhakikisha maeneo yake yanapata majosho pamoja na malambo. Kwa bahati nzuri tulishakaa ofisini na kukubaliana jambo hili kwamba, katika mwaka wa fedha kwa sababu tunaendelea na mazungumzo na Wizara ya Fedha, fedha itakayotoka tutapeleka katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameainisha, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Kuhusu maswali Waheshimiwa Wabunge, tumerejea tena kwenye maswali marefu sana. Sasa leo nawakumbusha, wiki ijayo tutarejea kwenye utaratibu wetu wa kukukatisha ukiwa unauliza swali kwa kirefu sana. Kinachoyafanya maswali yenu yawe marefu ni pamoja na kuanza na pongezi. Pongezi tutoe wakati wa kuchangia sio wakati wa kipindi cha maswali na majibu.

Nasema hivi kwa sababu kama umesimama na una swali kwa Serikali halafu unaanza na pongezi, sasa swali lako linatoka wapi? Maana yake majibu unayo tayari kwa mambo mazuri yaliyofanyika, maana yake huna swali. Kwa hiyo tutakapofika hapo ili mtu asijisikie vibaya naanza kwa kuwakumbusha kwamba tunarejea kwenye utaratibu wetu wa maswali mafupi na majibu mafupi.

Pongezi ni kwa pande zote mbili, pongezi kutoka upande wenu Wabunge, lakini pia kutoka upande wa Serikali. Kila Mbunge anafanya kazi nzuri ya Jimbo lake, kwa hivyo, Mbunge akiamua muda wake wa kuchangia ni sawa lakini huu wa maswali Wabunge tuko wengi na Wabunge wengi mngependa

kuuliza maswali. Kwa hivyo, ukiuliza marefu muda wetu unatuishia na Wabunge hampati nafasi ya kuuliza maswali kwa niaba ya wananchi waliowatuma hapa ndani.

Sasa katika kuokoa muda nilishazungumza kuhusu majibu kwa upande wa Serikali kama ifuatavyo, kwamba:-

(i) Huna haja ya kurejea kwa niaba wakati wa swali la nyongeza.

(ii) Huna haja ya pongezi.

(iii) Huna haja ya kurejea majina ya Mbunge kama Spika alishamwita huyo Mbunge. Huna haja ya kusema Mbunge tena, unamaliza ule muda wa kuuliza maswali ya nyongeza kwa upande wa Wabunge.

Kwa hiyo, naamini Mheshimiwa Waziri wa Nchi, utatusaidia kwa sababu majibu mara nyingi yanatolewa hapa na Naibu Mawaziri. Utazungumza nao maana wakati mwingine tukizungumza haya sio wote wanakuwa hapa ndani. Kwa hivyo, hawapati ule ujumbe, wakija hapa mbele wanarejea kule ambako tumetoka, halafu inakuwa haipendezi nikikaa hapa mbele namwambia Mheshimiwa Waziri, jibu swali, jibu swali inakuwa haipendezi. Hata hivyo, ni mambo ambayo tunaendelea kujifunza ili tuweze kuokoa wakati mchache ambao tunao na Wabunge wengi mnakuwa mnasimama kila wakati kutaka maswali ya nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nilete matangazo niliyonayo hapa mbele na mambo mengine ambayo nitataka kuyazungumza. Kwanza ni tangazo la wageni walioko hapa Bungeni waliokuja kututembelea.

Tunao wageni 37 wa Mheshimiwa Mary Masanja, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni wadau wa klabu ya *Green Awareness* kutoka Chuo cha Misitu Jijini Arusha. *(Makofi)*

Tunao wageni 60 wa Mheshimiwa Innocent Bilakwate ambao ni Wenyeviti wa CCM wa Kata, Makatibu Waenezi wa CCM wa Kata na Makatibu wa Kata wa CCM wakiongozwa na Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM Wilaya ya Kyerwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Kavejuru Felix ambaye ni Kiongozi wa Ushirika wa Wakulima wa Tangawizi kutoka Buhigwe, Mkoa wa Kigoma, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambao ni wajasiriamali kutoka Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Tabu Magomba, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Cecil Mwambe ambaye ni mfanyabiashara na Mjumbe wa Bodi ya Wasanii wa Uchongaji kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Mwantumu Zodo kutoka Kampuni ya *Nice and Free Sanitary Pads* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara ambao ni Mwenyekiti na Mjumbe wa Bodi kutoka Mkoa wa Mtwara, Ndugu Anafi Nahonyo na Ndugu Dadi Akayoha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani ambao ni Viongozi wa Vyama vya Ushirika kutoka Kishapu Mkoani Shinyanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Michael Kembaki ambaye ni Katibu Mwenezi wa CCM, Kata ya Kenyamanyori, Wilaya ya Tarime Mkoa wa Mara, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 29 kutoka Chuo cha Kodi cha Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Rais wa Chuo hicho, Ndugu Lucky Lugwisha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanachama 15 wa *Tanzania Drama and Film Actors Association (TDFA)* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wamiliki na walimu 32 wa shule za *Day-care* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi na walimu 40 wa Shule ya Sekondari *DCT* ya Mvumi Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 90 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao Bungeni asubuhi hii, lakini wengine tutaendelea kuwatangaza kadri watakavyokuwa wakija.

Ninalo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Taasisi ya

Kumbukumbu ya Mwalimu J. K. Nyerere inawaalika kwenye Sherehe ya Kumbukizi ya Miaka 101 ya Baba wa Taifa Mwalimu J. K. Nyerere. Sherehe hiyo itafanyika kesho siku ya Jumamosi tarehe 6 Mei, 2023 kuanzia saa tatu asubuhi katika Ukumbi wa Chimwaga, Chuo Kikuu cha Dodoma. Mambo yatakayofanyika katika kumbukizi hii ni pamoja na kufanya Kongamano la Kumbukizi ya miaka 101 ya kuzaliwa kwa Baba wa Taifa; uzinduzi wa Klabu za Mazingira za Mwalimu J.K. Nyerere vyuoni na kwenye shule za msingi na sekondari kwa minajili ya utekelezaji wa Kitaifa wa utunzaji wa mazingira endelevu; na pia kutakuwa na kuzindua Mpango Maalumu wa urithishaji kwa watoto na vijana mambo mazuri ya Baba wa Taifa aliyoliachia Taifa letu kupitia Midahalo, Semina, Makongamano, majadiliano, mashindano mbalimbali na usajili wa wanachama.

Mgeni Rasmi katika Kumbukizi hii anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote tunakaribishwa katika tukio hili muhimu sana, lakini pia anaekwenda kuwa Mgeni Rasmi ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, twende tukamuunge mkono. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia sasa kwa sababu ndio tumemaliza maswali na hapa kuna mwongozo unaohusu maswali. Mwongozo huu uliombwa na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputi Mollel, kuhusu swali lake Na. 222 kutojibiwa kikamilifu.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 3 Mei, 2023 katika Kikao cha Kumi na Saba cha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, Mkutano wa Bajeti, Mheshimiwa Noah Mollel, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 76 na Kanuni ya 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2023, kuhusu swali lake Na. 222 kutojibiwa Kikamilifu.

Waheshimiwa Wabunge, wakati wa kipindi cha maswali na majibu, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputi, aliuliza swali la msingi Na. 222 kwa Wizara ya Kilimo, kama ifuatavyo; "Je, Serikali ina mkakati gani wa kushusha bei ya mbolea na pembejeo nyingine za kilimo ili kuongeza uzalishaji?"

Swali hilo lilijibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa niaba ya Waziri wa Kilimo kwamba; "Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya Kupunguza gharama za upatikanji wa mbolea na pembeo nyingine kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji na tija kwa mazao ya kilimo. Aidha, Mheshimiwa Naibu Waziri, alielezea zaidi kwamba mikakati hiyo ni pamoja na kutoa ruzuku ya mbolea, mbegu bora kwa mazao mbalimbali pamoja na viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti milipuko na visumbufu vya mimea".

Vile vile, Mheshimiwa Naibu Waziri, alieleza Bunge kwamba kufikia Aprili, 2023, jumla ya tani 345,922 za mbolea zimenunuliwa na wakulima 799,935 kwa bei ya ruzuku. Aidha, alifafanua kwamba Serikali imetoa Jumla ya lita 48,033 za viuatilifu kwa utaratibu wa ruzuku kwa ajili ya kudhibiti viwavi jeshi vinavyoshambulia mazao mbalimbali.

Kwa kumalizia Mheshimiwa Naibu Waziri, aliahidi kwamba utaratibu wa utoaji wa ruzuku na pembejeo za kilimo kwa wakulima utaendelea kufanyika kulingana na bajeti ya Serikali."

Waheshimiwa Wabunge, mara baada ya kuuliza swali la msingi, kiti kilimpatia Mheshimiwa Mollel, fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza ambapo aliuliza kama ifuatavyo; "Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa Mawakala ambao walitakiwa kutoa mbegu katika Jimbo la Arumeru Magharibi, wamekataa kutoa mbegu kwa madai kwamba Serikali haijawalipa fedha zao na kusababisha wakulima kutopata mbolea katika maeneo husika. Je, nini kauli ya Serikali

kwa ajili ya kuwasaidia wakulima hawa kwa haraka ili waweze kupata mbolea katika msimu huu wa kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa mawakala hawa wanateuliwa na Wizara moja kwa moja kwenda kwenye majimbo au halmashauri, je, Serikali haioni sasa ifanye jambo la haraka kuwateua Mawakala wa uhakika watakaokwenda kutoa huduma hiyo kwa wananchi hawa ili waendelee kupata huduma?"

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu maswali hayo nanukuu kama ifutavyo; "Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba Mawakala hawajalipwa fedha zao ndio sababu ya kutopeleka mbolea ya ruzuku kwa wananchi, jambo hili sidhani kama lina ukweli wowote isipokuwa ni kwamba Serikali inafanya taratibu za kumalizia malipo kwa baadhi ya Mawakala ambao watalipwa na kazi yao itafanyika lakini kigezo cha kutolipwa kwa sababu hiyo ni kigezo ambacho Serikali kupitia Wizara ya Kilimo haioni kama ni njia muafaka ya kuwasaidia wakulima na wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatake mawakala wote kutekeleza yale maelekezo ya kimkataba ambayo walisaini kati ya Mawakala na Wizara ya Kilimo."

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu kuteua mawakala wa uhakika, Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza kwamba; "Serikali inafanyia kazi suala hilo na kwamba inaendelea kujifunza ili mapungufu yanayojitokeza yatatuliwe na yasijitokeze katika msimu ujao wa kilimo."

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na majibu hayo, Mheshimiwa Mollel, aliomba Mwongozo wa Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 76 na Kanuni ya 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, katika maombi hayo aliomba ufafanuzi zaidi utolewe kwa

sababu majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri hayakuwa ya kuridhisha.

Katika maelezo yake Mheshimiwa Mollel, alieleza kwamba majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, yanaweza yakaleta tafsiri kwamba taarifa ya Mheshimiwa Mollel, kwamba Mawakala wanakataa kuwapa mbolea wakulima ni taarifa ambazo sio za kweli.

Waheshimiwa Wabunge nimepitia swali Na. 222, maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mollel, Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard),* majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri na nimepitia Masharti ya Kanuni ya 76 kuhusu Mwongozo wa Spika na Kanuni ya 53 kuhusu maswali kujibiwa kikamiliifu ili kujiridhisha na malalamiko yaliyotolewa na Mheshimiwa Mollel.

Waheshimiwa Wabunge, katika kutafakari maombi hayo ya Mwongozo nilijiuliza swali ambalo linapaswa kutolewa mwongozo, je, Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kikamilifu maswali aliyoulizwa na Mheshimiwa Mollel na je, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yalikuwa ni ya kuridhisha?

Swali la Msingi Na.222, liliuliza kuhusu mikakati inayowekwa na Serikali kwa ajili ya kushusha bei ya mbolea nchini? Mheshimiwa Naibu Waziri, alitoa ufafanuzi wa kina kwamba Serikali inayo mikakati mbalimbali ya kupunguza gharama za mbolea na pembejeo ili kuongeza uzalishaji. Aidha, alieleza jitihada zilizopo za Serikali za kutoa ruzuku kwa mbolea, mbegu na viuatilifu ili kuzuia visumbufu vya mimea. Vile vile, alieleza kwamba utaratibu wa ruzuku utaendelea kufanyika kwa kutegemeana na bajeti ya Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, katika swali la kwanza la nyongeza la Mheshimiwa Mollel, alitaka kupata kauli ya Serikali kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wa Jimbo la Arumeru Magharibi,

kupata mbolea kutokana na kitendo cha Mawakala wa Mbolea kukataa kuwapa mbolea wakulima kwa madai kwamba Serikali haijawalipa fedha zao.

Katika kujibu swali hili, Mheshimiwa Naibu Waziri, alieleza kwamba hadhani kama jambo hilo lina ukweli kwa sababu Serikali inafanya taratibu za kumalizia malipo kwa Mawakala wanaoidai. Vilevile, alitoa ufafanuzi kwamba utaratibu wa kugawa mbolea umewekewa masharti kwenye Mkataba baina ya Wizara ya Kilimo na Mawakala.

Mheshimiwa Naibu Waziri, alihitimisha kwa maelezo kuwa Wizara ya Kilimo, haioni kama ni jambo linalokubalika la Mawakala wa Mbolea kukataa kuwapa mbolea wananchi kwa kutumia kigezo cha kutolipwa fedha zao. Aidha, Mheshimiwa Naibu Waziri, alielekeza Mawakala wote kutekeleza mikataba waliyoingia na Wizara ya Kilimo kuhusu kuwapa mbolea wananchi na alilieleza Bunge kwamba Serikali italifanyia kazi suala la kuteua Mawakala wa uhakika ili mapungufu yanayojitokeza yasijirudie.

Kwa ujumla wake maswali yaliyoulizwa na Mheshimiwa Mollel, yalitaka kujua mikakati ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wanapata mbegu, mbolea na viuatilifu kwa ajili ya kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Waziri, alitoa ufafanuzi wa namna Serikali inavyofanya jitihada katika eneo hilo na taratibu za kuboresha uteuzi wa Mawakala wa mbolea ili kusaidia wakulima kupata pembejeo kwa urahisi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia maelezo ya hapo juu, nimeridhika kuwa majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, yalikuwa ni majibu sahihi kwa swali la msingi na maswali ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Mollel. Huo ndio

Mwongozo wa Spika kwa Mwongozo uliokuwa umeombwa na Mheshimiwa Mollel. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Shaban Mtenga, na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga ajiandae.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nishukuru kwa kupata nafasi hii ya mwanzo kuchangia Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Kwanza kabisa, napenda nitoe shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuimarisha Wizara hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuleta uwekezaji hapa nchini. Kwa kweli Mheshimiwa Rais

anafanya kazi kubwa sana, wawekezaji katika nchi hii sasa hivi wanakuja kwa wingi sana, na nina imani kabisa Tanzania itakwenda mbele zaidi kibiashara pamoja na Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie suala moja kuhusu ushindani wa kibiashara. Katika suala hili, kidogo bado kuna changamoto, na hasa katika suala la biashara ya mafuta ya kula. Pale kwangu Bagamoyo, pamoja na shughuli nyingine za watu wa Bagamoyo, biashara kubwa sana pale inayofanyika kupitia Bandari yetu ya Bagamoyo ni ni biashara ya mafuta. Wafanyabiashara wengi wa Bagamoyo wanatoa mafuta kutoka Zanzibar, wanayaleta Bagamoyo na hatimaye kwenda kuyauza katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara hawa wanapata changamoto kubwa sana ya ushindani. Wanalalamika kwamba wenye viwanda, Serikali katika bajeti iliyopita wamewapatia *zero percent* ya *import duty,* lakini hii *zero percent* wafanyabiashara wanatakiwa walete mafuta ghafi *(crude oil)*. Inavyosemekana ni kwamba wafanyabiashara hawa hawaleti mafuta ghafi, wanaleta mafuta yaliyosafishwa ambayo ni *refined oil* na kwenda kuya-*park* katika viwanda vyao, na hivyo kwenda kuyauza. Hili linajidhihirisha wazi kwamba mpaka sasa bei ya mafuta pamoja kwamba Serikali imeshusha, wanafanyiwa *zero percent,* lakini bado bei ya mafuta iko juu, pamoja na kwamba Serikali imewapunguzia kodi hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfanyabiashara wa kawaida anachajiwa asilimia 25 ya kodi, lakini mfanyabiashara mkubwa anawekewa *zero.* Sasa hii kweli tutaleta ushindani wa kibiashara na tunaweza kuwakuza kweli wafanyabiashara wetu katika nchi hii?

Mheshimiwa Spika, leo hii mtu wa Bagamoyo anachukua dumu la mafuta kutoka Zanzibar, likifika Bagamoyo pale

linachajiwa shilingi 33,000 kodi, ukijumlisha bei ya manunuzi aliyonunulia kule, na gharama nyinginezo za *TBS,* mionzi, sijui nini, dumu hili linafikia mpaka shilingi 75,000 au shilingi 78,000 mpaka shilingi 80,000. Hivi huyu mtu anafanya biashara gani?

Mheshimiwa Spika, ile bandari kipindi cha nyuma tulikuwa tunafanya biashara, *TRA* walikuwa wakipata mapato makubwa sana. Ilifikia wakati tunatengeneza mpaka Shilingi bilioni mbili na zaidi kwa mwezi kwa kupitia Bandari ya Bagamoyo na wafanyabiashara wa Bagamoyo, lakini leo hali ni tofauti. Namwomba Mheshimiwa Waziri, katika ushindani wa biashara azungumze na Wizara ya Fedha, hizi kodi ambazo wanawapunguzia wafanyabiashara wakubwa katika mafuta ya kula, zinawapa changamoto wafanyabiashara wadogo, wanashindwa kuendelea, hawafiki mbali kibiashara.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka kuzungumza ni suala la *SEZ (Special Economic Zone)* Bagamoyo. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kipengele cha 195 ameelezea vipaumbele vya bajeti ya mwaka 2023/2024 katika maeneo maalum ya uwekezaji. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri hili. Nimeona Bagamoyo katika mipango yako ya vipaumbele umeiweka katika kipaumbele. Nashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Bagamoyo kuwajali katika hili.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika malengo ya Wizara kwa mwaka 2023/2024 sehemu ya 196 Mheshimiwa Waziri amezungumzia uendelezaji wa miradi ya Kitaifa ya kielelezo, *(National Flagship Projects)*. Kwa kweli kwa hili wananchi wa Bagamoyo wanampongeza sana Mheshimiwa Waziri na wanamshukuru sana, amewatendea jambo la haki sana.

Mheshimiwa Spika, haitoshi, katika kipengele hicho hicho Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la fidia kwa watu wanaopitiwa na huu mradi wa *SEZ*. Namshukuru sana

Mheshimiwa Waziri, kwa kweli amefanya kazi kubwa sana, wananchi wa Bagamoyo Kata ya Zinga, maeneo ya Mlingotini, Pande na maeneo mengineyo ya Kondo walikuwa wanalalamika sana kuhusu hili jambo, na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri ameituma timu kule inayoongozwa na Dkt. Mchome wa Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es Salaam, wanafanya kazi nzuri, nami nimezungumza nao, wanaendelea na kazi nzuri kabisa ili kuweza kuliweka jambo hili sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakapofikia kipindi, wananchi wa Bagamoyo wamelipwa katika hili jambo kwa kweli watampongeza sana Mheshimiwa Waziri na watamwombea sana kwa Mwenyezi Mungu. Maana ni mwaka wa 13 sasa hivi, wananchi wa Bagamoyo wa sehemu hizo bado hawajapata malipo yao. Kwa bajeti ya mwaka huu, kwa kulizungumzia hili la fidia ya wananchi hawa, kwa kweli sina budi kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala ushindani wa biashara, naomba Mheshimiwa Waziri wa hii Wizara na Waziri wa Fedha waangalie jinsi gani ya hizi kodi zitashuka ili wafanyabiashara nao wapate kufanya biashara zao na kupata faida. Bagamoyo inaendeshwa na bandari, wafanyabiashara wengi wanaendeshwa na bandari ya ile, mama ntilie wanafanya kazi kupitia ile bandari, wabebaji mizigo wanafanya kazi kupitia ile bandari, lakini suala la mafuta ya kula, itakapokuwa kodi kubwa, wafanyabiashara wa Bagamoyo hawatapata fursa ya kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hassan Shaban Mtenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani ajiandae.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru na nikuombe kwa ridhaa yako nirekebishe jina. Naitwa Hassan Seleman Mtenga.

Mheshimiwa Spika, nami nianze kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anazozifanya kwenye suala la kulihudumia Taifa, hasa Jimbo la Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara. Dada yangu kwa kweli anastahili sifa na anafanya kazi ya kumwakilisha Rais. Pia Mheshimiwa Waziri amepata msaidizi mzuri sana, Katibu Mkuu, Dkt. Hashil, naweza nikasema ni Katibu Mkuu wa mfano; moja ya Makatibu bora ambao wanapokea simu za Wabunge *any time*. Huyu bwana, kwa kweli anatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Liganga na Mchuchuma, tunarudi nyuma tunasema kwamba huu mfupa ambao ulimshinda fisi. Kwa ushirikiano mkubwa wa Katibu Mkuu na Waziri wa Viwanda na Biashara, nadhani mgogoro huu umefika mwisho, na Watanzania sasa watapata stahiki zao, nikizungumza Serikali kupata mafao kupitia Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Viwanda na Biashara ndiyo Wizara mama ambayo inategemea uchumi mkubwa ndani ya Taifa letu. Kwa nini nazungumza hivi? Tunazungumza kwamba tuna viwanda, na tunapozungumza ajira, zipo kwenye viwanda. Sasa tukiangalia Mtwara, Lindi na Dar es Salaam, tunavyo viwanda zaidi ya 5,000 ambavyo vinazalisha chumvi. Viwanda hivi 5,000 ni viwanda vidogo vidogo ambapo huko nyuma tulipoanza ingekuwa sasa hivi, tumeshapata viwanda vikubwa zaidi ya vitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo kwa kweli linasikitisha sana. Chumvi yetu ya Tanzania imefika sehemu imeuawa na kukosa soko kwa sababu ya mwekezaji mmoja tu. Chumvi hii ambayo sasa hivi imekosa soko, na mara nyingi wataalam wa Kiwanda cha *Neel* wanasema chumvi hii ina madini ambayo siyo salama kwa binadamu.

Mheshimiwa Spika, unayeniona nimesimama hapa, nimeanza kula chumvi ya Mtwara mpaka umri huu unaoniona, sijapinda mgongo, sijapinda kichwa wala miguu. Sasa hawa wataalam wanaofika mahali wanaua soko na chumvi ya Watanzania eti kwa sababu ya chumvi ya nje, leo chumvi ya Mtwara, Lindi na Dar es Salaam ilikuwa inauzwa Afrika kwa ujumla toka tumeanza, sasa hivi hii chumvi haiendi huko, kwa sababu wataalamu wa *Neel* wanaagiza chumvi kutoka nje, lakini wana-*expor*t kutoka Tanzania kwenda Kongo na Malawi wakati chumvi ya Watanzania ipo.

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri, alitembelea Lindi Mtwara na Kilwa na akaona mwenyewe kwa macho yake chumvi ilivyokuwa nzuri, na chumvi ilivyojaa kwenye maghala, alitoa tamko, akaelezea umma ya Watanzania kwamba kuanzia sasa *Neel* wasipewe kibali cha kuagiza chumvi nje, wachukue chumvi yetu ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengine yanasikitisha sana. Wakati Mheshimiwa Waziri anatoa tamko, Wizara ya Madini imefika mahali wakasema huyu tumpe kibali. Sasa ninashauri, hawa ni Mawaziri wawili, hata kama kuna mambo ya kiutaalamu, anapotoa tamko Waziri wa Madini ambalo linamhusu Waziri kwenye sekta nyingine, basi wakae wazungumze. Siyo anatoka mtumishi mmoja, anasema aah, huyu mwana mama ni mwanasiasa. Tusizungumze siasa kwenye maslahi ya watu. Tunazungumza maisha ya watu wa Lindi, Mtwara na Dar es Salaam wanaozalisha chumvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukija Mtwara ukiwaona wananchi wa Mtwara ambao walikuwa na utajiri wa chumvi, utayemkuta ana kiatu kizuri cha shilingi 60,000, ukimkuta mwananchi mwenye shamba la chumvi ana kiatu cha kuvaa chenye thamani ya shilingi 60,000 mimi nadhani nitatafuta milioni, nikakupatia, kwa hali ilivyo mbaya na wananchi jinsi walivyoathirika na uchumi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, hawa ni Watanzania wetu, tuna kila sababu ya kuwasaidia. Tulipofikia sasa hakuna haja ya kuagiza chumvi nje. Katika viwanda hivi nazungumza zaidi ya 5,000 wamekosa ajira watu wangapi? Yuko mzee mmoja, Mohamed Nassor pale Mtwara, alikuwa na mashamba yake ya chumvi, lakini kwenye uzalishaji alikuwa ni mzalishaji bora. Kulikuwa kuna akina mama pale zaidi ya 400 ambao wanafanya kazi na wanalipwa, wale akina mama 400 wote wamepoteza ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa unaweza ukatuona tunazungumza kwa sauti kubwa sana.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa tena ndugu yangu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea.

**TAARIFA**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, nomba nimtaarifu mzungumzaji kuwa Tanzania ina mahitaji ya chumvi

tani 250,000 kwa mwaka, na tunaingiza asilimia 70 kutoka nje, na wakati sisi tuna uwezo wa kuzalisha chumvi zaidi ya tani 300,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa hiyo mchangiaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea taarifa hiyo kwa mikono yote miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze kuhusu Wizara hii. Nimeangalia bajeti ya viwanda na biashara, nadhani inafika kwenye Shilingi bilioni 109, lakini huu ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili. Leo tunakwenda kuweka bajeti ya Wizara fedha hii, na kwenye uhalisia hatuwezi kuwapata wawekezaji bila Ofisi ya Katibu Mkuu, Waziri mwenye dhamana, wakazunguka nje na ndani kutafuta wawekezaji, hela hii itakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kama kuna uwezekano, safari tunayokuja, ya bajeti nyingine, Wizara hii tuiangalie kwa jicho la huruma. Fedha hii iliyotengwa ni ndogo mno. Tuna haja ya kuwa na wazawa ambao wanaweza kuwa na viwanda ndani ya nchi hii, lakini kwa mfumo uliokuwepo sasa, wa mabenki yetu, hatuwezi kuwapata wazawa kwa asilimia 70 ambao wanaweza kuwa na viwanda ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, leo wako watu walikuwa wanatafuta *LCs* za benki wapate dhamana ya mtaji wafungue viwanda. Wamesaga lami, wamesaga viatu zaidi ya miaka saba, nane, lakini leo anakuja mtu na *briefcase* hapa. Tulimsikia Mheshimiwa Rais analalamika hapa, anasema kaja mtu mmoja hapa, kaingia huku, kaingia huku, hana nyumba hana kitu gani, amechukua mabilioni ya Shilingi na ameondoka. Rais wetu analalamika.

Mheshimiwa Spika, haya inawezekana humu tukaishauri Serikali kila mkoa tuunde pale Kamati, wale wafanyabiashara waliotafuta *LCs* za benki na wakitaka mikopo mikubwa, vikwazo gani wamekutana navyo? Tutapata majibu humu, maana yake inawezekana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30 Mheshimiwa malizia.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, inawezekana tunakuja humu tunajifungia, tunazungumza, lakini yaliyokuwa nyuma ya pazia hatuyajui. Kama tunataka kumsaidia Rais kwa dhati kabisa, hebu ifike mahali sasa tuwe tuna maamuzi. Nimeshauri kuhusu kiwanda cha *Neel,* biashara ya kuleta chumvi, nadhani ifike mahali tuseme, inatosha sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani, na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi. Nawapongeza Wizara kwa mipango na mikakati mizuri ambayo wanaendelea kuifanya na kuleta matumaini makubwa ndani ya sekta ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia maeneo machache, la kwanza nitazungumzia viwanda ambavyo Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake amevielezea kwamba ana mpango wa kufufua viwanda vya kimkakati. Nitajikita kwenye viwanda vya pamba ambavyo unatoka Kanda ya Ziwa kule, ndio sehemu kubwa ilikuwa na viwanda vya nyuzi enzi za utawala wa Mwalimu

Julius Kambarage Nyerere. Sasa atakuja kutuambia mikakati hiyo ameiweka kuhakikisha kwamba viwanda hivi vya kuchakata zao la pamba, naamini asilimia 70 ya zao la pamba tuna *export* asilimia 30 inabaki ndani ya Nchi. Sasa na mpango huu ukifanikiwa utatengeneza uchumi wa Taifa lakini vilevile utaongeza ajira kubwa kwa Watanzania hususan vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye zao la pamba lina vitu vingi ambavyo viko mule ndani. Kuna mbegu ambazo hutengeneza mafuta lakini kuna pamba yenyewe ambayo itatengeneza majora, itatengeneza khanga na vitu vingine. Jambo kubwa hapo ili kulinda masoko yetu ya ndani lakini na kuongeza thamani ya maji tunayozalisha hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, la kwanza; ni vizuri makorido ambayo yanaingiza khanga kwa njia za uchochoro yakadhibitiwa ili kuongeza thamani ya pamba katika Nchi yetu ya Tanzania. Vilevile na kuweka mkakati kwa sababu ameweka kwenye hotuba yake kwamba wanaenda kufufua viwanda. Sasa viwanda unavyovifufua hivi lazima tuweke utaratibu, taasisi zote za umma, magereza, jeshi, *MSD* na vitu vingine vyote vinavyotumia rasilimali hiyo ya pamba. Naamini kwa mpango huu mkiingiza hiyo *component* naamini kwamba tunaweza tukafanya vizuri zaidi na kuhakikisha kwamba viwanda vinafanya kazi kwa muda unaotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwenye viwanda vyetu vya korosho kule Mtwara, tunayochangamoto lakini naamini kwenye mpango wenu Wizara mlivyojipanga mkilisimamia vizuri na tukaja na majibu sahihi ambayo yataleta tija kwa Watanzania naamini jambo hili linaweza likafika mwisho na tunatengeneza historia kwenye nchi yetu tukaondokana na maneno ambayo kila siku tukiamka tunahubiri. Sasa tunahitaji tutoke hapa twende kwenye vitendo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala la kibiashara. Nchi yetu tangu ipate uhuru ilikuwa na viwanda vya *cement* vichache, kuanzia uhuru mpaka 2020 tulikuwa na viwanda tisa. 2020 mpaka 2023 leo tuna viwanda 14 na maana yeke ni nini? Maana yake wafanyabiashara wanapoongezeka ndio ushindani unaongezeka kupunguza mahitaji kwa wananchi wetu wa kawaida hususan watu tunaotoka mkioa ya Kanda ya Ziwa na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viwanda vyote viko Dar es Salaam, viko Tanga na maeneo mengine lakini wahitaji wakubwa ni nchi nzima kwa maana ya kanda zote kwenye mikoa ambayo inauhitaji kwenye vitu hivi.

Mheshimiwa Spika, ijulikane kabisa, tunajenga barabara, tunajenga hospitali, tunajenga madarasa na wananchi wanajenga nyumba yote inahitaji *cement*.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikisikiliza jana mjadala huu wa *Tanga Cement*, ukiangalia *Tanga Cement* kibiashara pale na Simba ndio ipo kwenye soko na hii Simba iko kwenye soko na zamani *Twiga cement* nayo ilikuwa inachechemea pale Dar es Salaam. Watu walikuwa wakitumia magari kwenda kupakia, umebahatika sana unachukua wiki tatu au wiki mbili na *Tanga Cement* leo ndivyo hivyo hivyo ilivyo. Sasa ninajiuliza kama viwanda vinaongezeka na huyu anataka kuuza mali *share* yake sijui anamuuzia nani? Na ninyi Serikali kama mna mpango mzuri basi mashirika yenu ya umma yaunganisheni yanunue hiyo hisa asilimia 68 ili ninyi mmiliki kuondokana na sintofahamu iliyoko hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tumefikia viwanda 14, bado tunaanza kulalamika kwamba tuna hofu. Mimi sidhani mtu anayefanya biashara awe na hofu, hofu ya aina gani kwenye

shughuli ambayo anajipatia kipato. Kwa hiyo, hili jambo ni vyema sana Serikali mkatueleza kwamba kuna nini humu ndani kimejificha ambacho Wabunge hatukifahamu na jamii haijui. Kwa sababu mambo haya yanayojitokeza haya kweli yanatoa taharuki ambayo hatuielewi elewi lakini mimi naamini pale Tanga kuna kiwanda kingine kinaitwa Mawenzi.

Mheshimiwa Spika, sasa najiuliza au kuongezeka kile na kile kiwanda cha *Tanga Cement* kiufupi hakizalishi vizuri, kiuhalisia kabisa. Hata sasa ukituma magari kwenda kupakia unachukua zaidi ya wiki tatu mpaka nne, wanasubiria. Sasa huyu mwingine ameingia, sasa hapa sijui kunakaushindani kakibiashara. Sasa hapa mtusaidie ninyi takwimu zenu za kitaalamu, kwamba takwimu za uzalishaji kila kiwanda. Hivi viwanda 14 vinazalishaje na mahitaji yetu kama nchi ni kiasi gani na bado sisi hapa tumepakana na nchi ambazo ni jirani Rwanda na Burundi, naona *cement* wanachukua kutoka Tanzania inatokea Tanga inaenda kule Uganda na Burundi.

Mheshimiwa Spika, sasa yote haya ni vizuri watu wa Serikali mkitueleza mtatusaidia sana kwamba mkakati wenu ni nini na hiki kinacholalamikia ni kitu gani. Ili kusudi tuwekane vizuri tuweze kufanya kazi hii ambayo imetuweka humu ndani kwenye Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, niwapongeze sana taasisi kwa maana ya *BRELA* na *TIC* sasa hivi *BRELA* pale na *TIC* pale mtaji wako wa dola milioni 50 unapata *incentive* maisha yanaendelea. Kwa hiyo, waendelee kuboresha mifumo yao, isiwe ina kwama kwama kwa maana ya kwamba ili tusicheleweshe mambo, watu wanahitaji kuwekeza na Watanzania wanahitaji kufanya kazi nzuri kwa ajili ya maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuombe Mheshimiwa Waziri kwenye Kiwanda chetu cha Vifaa Tiba Dutwa tusifanye maigizo na kama

kweli tuko *serious* tuna fedha za walipa kodi na huku tuna tatizo la ajira. Tunazitenga hela tunazila zinapotea halafu mradi unasimama. Jambo hili halikubaliki na sio sawa sawa, ilikuwa hakuna sababu yoyote ya kuanzisha mipango mikubwa na shughuli zingine zikawa zinakwama kufanyika, tukiamini kwamba tunakuja kupata mwarobaini, matokeo yake ikaka kimya na tukaanza kusikia sikia, mara kinakwenda Morogoro sijui kinakwenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani mipango ya Serikali anayoianzisha mtu yeyote kwenye eneo ambalo linalenga jamii ya wananchi. Basi anayekuja mwingine ni kuendeleza na ndio maana mama akasema kazi iendelee. Sasa kazi iendelee maana yake yale yote yaliyokuwepo yaendelee kutekelezwa. Kiwanda kile ni kikubwa na kikifanyiwa kazi naamini kabisa kitatoa *solution* ya zao letu la pamba katika Kanda yetu ya Ziwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara hivi karibuni kule kwetu, pale Maswa kuna kiwanda cha chaki hivi ndio kiwanda cha kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vyema ile fedha inayohitajika kutoka kwa vijana wa Maswa basi iende ili kiwanda kile kianze kufanya kazi. Sasa pale kuna bilioni nane zimesimama halafu mambo haya hatuyatekelezi. Niwaombe sana Mheshimiwa Waziri tuna imani kubwa na wewe ni mchapakazi na una weledi wa kutosha. Ni imani yangu ya kwamba mambo haya yakikamilika naamini kabisa tutakwenda vizuri na hitaji kamili litatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest Lwehikila, Mheshimiwa Augustine Vuma Hole ajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kunipa fursa ya kuchangia katika Wizara hii ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa sababu tangu aingie madarakani kati ya vitu ambavyo ameviweka kama maeneo yake ya vipaumbele ni katika kuhakikisha kwamba anaifungua Nchi yetu kwa wawekezaji wa nje, kuhakikisha anakuza uwekezaji wa ndani na kuhakikisha anakuza diplomasia ya uchumi katika Nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nitumie fursa hii kuipongeza Wizara, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara. Kwa sababu kazi inayofanyika ni kubwa na matokeo yake tunayaona, hotuba iliyosomwa ya bajeti ya Wizara hii inatia matumaini.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia nilivyokuwa nimepanga kuchangia, nimevutiwa sana na mchango alioutoa Mheshimiwa Mtenga juu ya changamoto ya viwanda vya chumvi katika Mkoa wake wa Mtwara na Lindi na ningependa tu wakati Mheshimiwa Waziri anakuja kutujibu hapa atueleze nini mkakati wa Serikali au Serikali ina mpango gani katika ku–*control* vibali vya uingizaji wa chumvi nchini, kwa sababu tukiacha hili eneo wazi hatuhatarishi tu viwanda hivi lakini tunahatarisha ajira nyingi sana za vijana…

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ng'wasi Kamani kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Biteko.

## TAARIFA

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Mbunge ninaomba tu kutoa taarifa kwa msemaji na kwa Bunge, kwamba vibali vya kuingiza chumvi nchini vilisimamishwa na Waziri wa Viwanda na sisi Wizara ya Madini tunaotoa vibali toka tumekubaliana na Wizara ya Viwanda kusitisha uingizaji wa chumvi ili tukubaliane namna gani tutumie chumvi ya ndani kabla ya kuagiza ya nje, hatujawahi kutoa kibali chochote na hakuna kibali kinachotolewa hadi sasa. Kwa hiyo, nilitaka tu wakati anachangia awe na *comfort* hiyo na Bunge liwe na *comfort* kwamba Serikali inafanyia kazi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dotto Biteko, nilimsikia Mheshimiwa Nyongo akisema asilimia 70 ya chumvi inaagizwa. Amesema asilimia 70, wewe unasema haiagizwi kabisa, yaani mmesitisha uagizaji ama mimi ndio nimechanganya? Si unazungumzia chumvi. Mheshimiwa Nyongo taarifa uliokua unampa Mheshimiwa Mtenga ilikuwa inasema, tunaagiza asilimia ngapi?

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba mahitaji ya chumvi kwa mwaka Tanzania ni tani 250,000. Tunaingiza asilimia 70 ya mahitaji hayo na wakati nchi ina uwezo wa kuzalisha chumvi tani zaidi ya 300,000 kwa kutumia *source* zote tulizonazo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Doto Biteko, hiyo taarifa sasa iko sahihi ili nimuulize sasa yule anapokea taarifa yako, kwamba vibali havitolewi na yule anasema asilimia 70 inaingia. Au ilikuwa inaingia kabla hamjaweka hilo katazo.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Nyongo nimemuelewa ni kwamba mahitaji ya chumvi ni tani 250,000 ambayo namba imepanda kidogo. Lakini sisi tunaagiza chumvi asilimia 70 wakati tuna uwezo wa kuzalisha zaidi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Nyongo ana *justify* kwamba hatuna sababu ya kuagiza kwa sababu uwezo wa kuzalisha uwezo wa kuzalisha chumvi ndani ni mkubwa kuliko kuagiza nje na ndicho nilichokuwa natoa taarifa kwa Mheshimiwa Kamani.

**SPIKA:** Swali langu ni kwamba hiyo asilimia 70 tunaingiza ama hatuingizi?

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, hiyo asilimia 70 ndio tunayo *import* kwa ajili ya kuja ku-*blend* chumvi ambayo tunayo ndani wakati tunayo ndani inayozidi kiwango hicho.

**SPIKA:** Haya pengine mwenye hoja ameelewa, Mheshimiwa Ng'wasi Kamani unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo naipokea, lakini nitumie fursa hii kutoa rai kwa Serikali kama tayari takwimu zinaonesha kwamba tuna uwezo wa kuzalisha chumvi ya ndani kwa kiwango kikubwa hata kuliko kile tunachohitaji katika mahitaji yetu. Naiomba sana Serikali utaratibu huu wa kufuta vibali hivi basi utiliwe mkazo ili viwanda vya ndani vya chumvi vipate kuzalisha na ajira za vijana na wakina mama wa Tanzania tuendelee kuzilinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya kwanza itakuja kwenye suala la chuma; Imekua miaka mingi sana na Wabunge wengi sana wamechangia suala la Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Silengi kuujadili mradi huo kwa sababu naamini Serikali imesikia inaendelea kulifanyia kazi kwa sababu imekua ni jambo la muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka tu Serikali itueleza katika nchi yetu Mungu ameibariki na chuma inapatikana sehemu nyingi sana na katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri ametuonesha kwamba katika mwaka huu wa fedha wanampango wa ku-*deal* na Liganga na Mchuchuma na Chuma kilichoko Maganga Matitu. Lakini kuna chuma kipi Handeni Tanga, kuna chuma kipo Mayamaya Dodoma, kuna chuma kiko maeneo Hondusi Morogoro lakini Wizara haizungumzii mambo haya. Tunaona kila leo kuna magari ya Dangote yanatoka katika maeneo yale ambako wachimbaji wadogo wadogo wanachimba chuma zinasafirishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali nitaomba ije itupe majibu, je, imekwishafanya tathmnini ya viwango vya chuma vilivyoko katika maeneo haya? lakini wachimbaji wadogo wadogo wanachimba hii chuma na kupakia na zinaenda nje. Je Serikali inafanya tathmini ya kiasi gani cha chuma kinatoka? Lakini Serikali inapokea mapato au maduhuri kiasi gani kutoka kwa wachimbaji wale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano katika Wizara ya Madini, miaka ya nyuma Wizara ya Madini ilikuwa imetoa kipaumbele kikubwa sana na *guidance* kubwa kwa makampuni makubwa ya wachimbaji, ikasahau wachimbaji wadogo. Leo hii Wizara ya Madini imeamua kuwa *incorporate* wachimbaji wadogo na tuona ni namna gani mapato kutoka Wizara ya Madini yameongezeka.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia Wizara hii iangalie mfano huu kutoka katika Wizara ya Madini. Tuna wachimbaji wadogo wa chuma wanaochimba na chuma hii inatoka, itueleze ni kwa nini chuma hii inatoka bila kuchakatwa. Ni kwa nini hatujaja na mpango mkakati wa kuwa *guide* hawa wachimbaji wadogo ili na wao waweze kutuongezea pato na Mheshimiwa Waziri katika taarifa yake ametuonesha mahitaji ya chuma yalikuwa kutoka

tani 200,000 na sasa tunaenda kwenye tani 1,000,000 na tuna *project* kubwa sana za Serikali zinazofanyika za kimkakati zinazohitaji chuma.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kila chuma iliyoko katika nchi hii tukiiutumia ivilivyo na Serikali ikaangalia. Kuacha tu katika hii *project* moja ya Liganga na Mchuchuma ambayo nayo inatakiwa iendelee kufanyiwa kazi lakini tuangalie na chuma zingine zilizoko katika maeneo mengine ili tusipoteze mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja pia katika suala la *NDC*, *NDC* imeanzishwa zaidi ya miaka 60 sasa katika Nchi yetu. Ningependa pia katika majibu ya Serikali Mheshimiwa Waziri aje atuambie *NDC* mpaka sasa ina leseni ngapi? Na leseni ngapi zinazofanya kazi na ngapi hazifanyi kazi, wapi tumefeli na wapi tunatakiwa kurekebisha. Ili kusudi tuweze kuisaidia *NDC* kufanya kazi yake vizuri na iendelee kulipa maduhuri inayotakiwa kulipa katika Serikali.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia Mheshimiwa Waziri katika majibu yake aje atueleze, tumeona mikakati mingi na kwa hilo nawapongeza ya kuweza kuwakuwa wawekezaji wadogo ndani ya Nchi yetu. Kwa namna moja ama nyingine naweza nikasema bado Wizara hii haina wivu na wafanyabiashara wake wa ndani, Wizara hii haina wivu na wawekezaji wadogo wa ndani kwa sababu wawekezaji hao na wafanyabiashara wanapitia changamoto nyingi na mara nyingi Wizara hii imekuwa ikirudi nyuma kuwaachia Wizara zingine ziweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii wafanyabiashara kule nje hata wakipata usumbufu kutoka *TRA* bado Wizara hii itasema hapana hayo ni mambo ya Wizara ya Fedha sisi tunakaa pembeni. Leo hii wafanyabiashara wetu wanachajiwa hela ya kodi kabla ya miezi sita ambayo ndio takwa la sheria. Wizara hii itakuambia inakaa

nyuma haya ni mambo ya *TRA*, mambo ya Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara hii ianze kuwa na wivu na wafanyabiashara wake ianze kuwa na wivu na wawekezaji wa ndani. Wawekezaji wa nje tunawapenda, wanatupa fursa za ajira, wanatupa mapato kama nchi lakini fimbo ya mbali haiui nyoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji Wizara hii ije mkakati kama tunavyolinda wawekezaji wa nje, kama tunavyopambana kuhakikisha wanakuja kwa wingi, tuendelee kuwalinda wa ndani ili waweze ku-*maintain* ushindani. Tuwape nafuu za kikodi tuwajengee mazingira yaliyo salama ili kesho na keshokutwa mfanyabiashara katika eneo lake la kazi akiona Afisa wa Serikali anakuja kumtembelea wasitishike kama wanavyotishika sasa hivi. Waone hawa ni marafiki zao wanataka kuwanyanyua wanataka kuwasaidia katika hili Mheshimiwa Waziri tunaomba utusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kingine nilitaka kuishauri Serikali sasa hivi zaidi ya asilimia 70 ya viwanda vilivyoko katika nchi yetu viko maeneo ya Dar es Salaam na Pwani. Je, Serikali haioni haja ya kuja na mpango wa kutoa *incentive* kwa wawekezaji wa ndani na nje ili kuweza kuanzisha viwanda vingi zaidi katika maeneo mengine ya nchi? Baba wa Taifa aliona umuhimu wa jambo hili na ndio maana walianzisha viwanda vingi sana katika maeneo mbalimbali ya nchi, mikoa mbalimbali kulingana na mazao au vitu vinavyozalishwa katika mikoa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii viwanda hivyo vingi vimekufa kwa sababu ya ubinafsishaji na wale waliobinfsisha viwanda hivi, wamekiri wenyewe hata wengine wameandika vitabu kwamba kuna sehemu walikosea. Sasa Serikali inajifunza nini ili kutusaidia kwanza kufufua viwanda hivi turudishe viwanda katika mikoa

mingine ili tuweze ku-*balance* maendeleo lakini mimi naamini pia ni hatari sana kwa Taifa letu kama tukifanya viwanda vyote viwepo Dar es Salaam na Pwani tu. Hiyo ni ngumu sana tunatishia kwanza *migration* watu wote wa Nchi nzima wahamie Dar es Salaam na Pwani lakini pili maendeleo yatakuwepo kule kuliko sehemu zingine zozote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Waziri atatuambia hapa kwamba pamoja na kwamba Nchi yetu ni *consumers* wakubwa sana wa vitu vingi sana kutoka nchi za wenzetu. Ni kwa nini makampuni haya makubwa ya *manufacturing* yanaanzisha *franchise* na *branches* zake katika nchi za wenzetu zinazotuzunguka na hawaji hapa kwetu.

Mheshimiwa Spika, pia tulikuwa na sehemu za ku-*assemble* scania katika Nchi zetu na matreka. Viwanda hivyo vimefungwa, vimepelekwa katika nchi za wenzetu. Kuna shida gani katika nchi yetu inayofanya wawekezaji wakubwa badala ya kuleta makampuni haya ku-*assemble* mali zao hapa inapeleka katika nchi jirani na sisi tunakosa fursa hizo.

Mheshimiwa Spika, nilishawahi kuishauri Serikali, tuna uhitaji mkubwa sana wa kuiwezesha *TiRDO* na *SIDO* zetu kama tunahitaji kwenda katika uchumi wa viwanda. Leo hii *SIDO* katika bajeti iliyopita ilitengewa *1.9 bilion* lakini mpaka tunavyozungumza imepewa milioni 400 tu. Hatuwezi tukafika katika uchumi wa viwanda kama *TiRDO* na *SIDO* tusipoziwezesha inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Augustine Vuma Holle ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya Nchi yetu. Kwanza kabisa nianze kwa kuipongeza Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa kazi nzuri inayofanya katika kuwekeza viwanda ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu namna Mheshimiwa Rais anavyopambana kuifungua nchi, kukaribisha wawekezaji lakini pia ku-*promote* vitu vyetu vya ndani. Kwa hiyo niipongeze sana sana sana Serikali hii ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Spika, kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na watendaji. Wamejipanga vizuri, sasa hivi husikii makelele makelele mengi ya kuongezeka kwa bei za bidhaa, nchi imetulia na kazi inaendelea. Hongereni sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi hiyo nzuri. Kipekee niishukuru Serikali na nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri. Mwaka jana nilienda kumwona pamoja na wadau kuhusiana na viwanda vya ukoboaji wa kahawa pale katika jimbo langu. Kulikuwa na malalamiko yanajitokeza mara kwa mara kuhusiana na *curing loss.* Kwamba wakati kahawa inakobolewa, kuna taarifa za upotevu wa kahawa, inaitwa *curing loss.*

Mheshimiwa Spika, sasa ilikuwa inatofautiana kati ya kiwanda kimoja na kiwanda kingine. Kahawa hiyo hiyo imetoka kwenye chama kimoja ikipelekwa kwenye kiwanda hiki *curing loss* inakuwa kubwa lakini ikipelekwa kiwanda kingine inakuwa ya kawaida. Nilikuja na wadau kumwona Mheshimiwa Waziri tatizo lile limeshughulikiwa sasa hivi pako shwari. Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ameunda tume juzi imefanya kazi nzuri, imehoji baadhi ya *AMCOS,* zimejibu kwamba sasa hivi kelele ile sasa imekwisha. Kwa hiyo nishukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kulishughulikia hilo. Niombe usiishie hapo endelea kuchunguza chunguza, maana

hawa watu wajanja wanaweza wakawa wamefanya leo vizuri kesho wakafanya tofauti ili wakulima wetu wanufaike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili nimpongeze pia Waziri katika kipindi hiki ndipo tunaposhuhudia ulipwaji wa fidia wa Mchuchuma na Liganga, mradi ambao kwa kweli una historia kubwa na ndefu kweli kweli. Sisi wengine hata tulizaliwa suala la Mchuchuma na Liganga lilikuwa inazungumzwa. Leo watu wamekufa masuala haya yalikuwa yanazungumzwa; lakini leo kipekee tunashuhudia watu wanalipwa fidia. Ni hatua ya kupongeza sana kwamba tunatoka hatua moja kwenda hatua nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu, sasa tukilipa fidia tusikae, tusikae tuanze kutekeleza ule mradi. Nimeambiwa aliyeshinda hii *tender* hayupo tena duniani lakini watu wapo wa kuendeleza hii kazi. Nikuombe sana Waziri simama kama ulivyosimama, sasa hizi fidia zinalipwa, mradi huu uanze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi duniani ndiko kwenye malighafi ya makaa inahitajika. Watu sasa hivi wanavuna makaa pamoja na chuma kwa nguvu na kwa *speed* kubwa sana. Kwa hiyo nimuombe sana Mheshimiwa Waziri kipindi hiki ndicho cha kunufaika na huu mradi. Tusikae tena tunalipa fidia halafu tunaenda kutulia. Hatutai tendea haki nchi yetu, hatutawatendea Watanzania hawa haki. Mimi nina uhakika na Mheshimiwa Waziri suala hili ataenda nalo kwa *speed* kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine niishukuru pia Serikali. Pale kwangu kulikuwa na Mgodi wa *TANCOAL* kwa muda mrefu ulifanya kazi lakini ukasimama kwa muda pia mrefu sana kwa sababu tu ya migogoro ambayo pengine ilikuwa haina hata manufaa kwa nchi yetu lakini kwa Watanzania ambao walikuwa wanafanya kazi pale. Kulikuwa na mgogoro kati ya *NBC,*

Milambo na *Taifa Mine*. Taarifa njema sasa hivi kupitia watu wetu wa *FCC* mambo haya yamezungumzwa vizuri na muda si mrefu kwa maelezo niliyopewa kuna muwekezaji mpya anakabidhiwa huu mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba suala hili nalo liende kwa *speed* ile ile, lisije likakawia tuakona tena kizungumkuti. Kwa sababu limeshaisha linakaribia sasa huyu muwekezaji mpya ku-*take off* pale; na wamesema baada ya kukabidhiwa, pale tu mkataba utakapo sainiwa basi wale watumishi, wafanyakazi waliokuwepo pale wataanza kunufaika na mafao yao ya huko nyuma kwa sababu kulikuwa na kelele nyingi sana za malipo yao ya huko nyuma, lakini pia kulikuwa na madai tofauti tofauti pale. Mara kadhaa ilikuwa nikienda pale unasikia kelele za wafanyakazi, kelele za waliowekeza pale kwa maana ya kwa sababu migodi hii ya makaa ya mawe inakuwa na wawekezaji wengi wengi. Kwa hiyo kila mtu alikuwa anadai kupitia kwenye hii Kampuni ya *TANCOAL*.

Mheshimiwa Spika, sasa nina uhakika Mheshimiwa Waziri baada ya kusainiwa huu mkataba hawa wote watalipwa na sasa hatutapata tena kelele. Lakini shughuli ya uchimbaji ya makaa ya mawe ambayo sasa yanahitajika sana sana duniani itaanza kwa kasi sana. Kwa hiyo nikuombe sana Mheshimiwa Waziri hili lishughulikiwe. Lakini nikupongeze kwa hatua hii ya awali ambayo imefikiwa, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nitoe ombi. Kwa sababu wakati tunaambiwa tumegundua makaa ya mawe katika jimbo letu, wananchi hawa waliaminishwa kwamba sasa viwanda vitakuwepo, maendeleo yatakuwepo. Hata hivyo mpaka leo hatujapata kiwanda hata hiki, kimoja. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu tuna malighafi zetu pale, naomba sasa na sisi tupate kiwanda ili sasa wananchi wale waone manufaa ya kuwa na haya makaa ya mawe pale na

malighafi nyingine. Niombe sana hilo Mheshimiwa Waziri; najua pengine utalitolea ufafanuzi hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la kulinda viwanda vyetu. Nilisikiliza baadhi ya michango hapa jana ya namna tunavyo-*promote* viwanda vilivyopo ndani ya nchi yetu. Tuna viwanda vingi, mimi hapa niwe *specific* kuzungumzia Kiwanda cha Magari cha *GF Motors Limited*. Kwanza tumshukuru sana huyu mtu mzawa huyu kwa kuwa na wazo hili la kiwanda ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu watu kadhaa walijaribu kuanzisha viwanda hapa Tanzania wakashindwa, lakini huyu ndugu yetu kaanza muda si mrefu na sasa hivi *progress* yake ni nzuri sana. Ameshafikia kuzalisha magari mpaka 700 na malengo yake mwaka huu anaenda kuzalisha magari 1,200. Kwa kweli watu wa namna hii wanapaswa kupongezwa lakini cha ziada wanapaswa kulindwa ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa hivi ninavyokwambia mimi nilipata nafasi ya kutembelea pale. Tayari anawafanyakazi 115 wako pale wanafanya kazi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ombi langu watu wa namna hii wanapaswa kulindwa kwa sababu wanai-*promote* nchi yetu, wanakuza uchumi wa nchi yetu na wanatoa ajira kwa nchi yetu. Kwa hiyo tuombe sana Mheshimiwa Waziri watu hawa walindwe kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Amos Bulaya atafuatiwa na Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi namimi niweze kuchangia Wizara hii ya Viwanda na Biashara.

Kwanza Mheshimiwa Waziri ukija kuhitimisha hoja yako sisi wananchi wa Mkoa wa Mara tunahitaji utujibu kuhusiana na viwanda vyetu vilivyokufa pale Musoma. Kiwanda cha nguo, kiwanda cha kusindika samaki na kiwanda cha maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viwanda hivi vilikuwa vina mchango mkubwa sana katika kutengeneza ajira katika Mkoa wa Mara. Mheshimiwa Waziri kuna kipindi mlihamasisha sana wananchi watenge maeneo kwa ajili ya ukanda wa uwekezaji. Eneo moja wapo watu walilolitenga na wakalipwa fidia ingawa wengine wakadhulumiwa ni Wilaya ya Bunda. Ni zaidi ya miaka 10 sasa hivi hakuna hata kiwanda kilichowekezwa. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha maeneo yale yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji yanawekezwa ili wananchi wa pale waweze kupata faida, iweze kutengenzwa ajira kutokana na malighafi zinazopatikana maeneo husika? Ni muda mrefu sana tunahitaji majibu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi ningependa Mheshimiwa Waziri ukija hapa uje utueleweshe sisi Wabunge kuhusiana na hii *issue* ya *Twiga Cement, Tanga Cement;* yaani bado hatujaielewa sana. Tunaomba ukija uchukue muda mwingi sana kulielezea hili jambo ili sintofahamu ziondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kuuliza katika hili jambo, kwamba maslahi ya taifa yakoje, nimejiuliza sana. Sasa, kuna *Tanga Cement* anataka kuuza sehemu ya *share* kwa

sababu kashindwa kuendesha, kwa sababu ameshindwa kulipa kodi kwa zaidi ya miaka saba. Si kwa kupenda yeye bali ni kwa sababu hawezi tena kujiendesha. Kuna athari ya zaidi ya wanfanyakazi 3,000 kupoteza ajira hapo. Sasa yeye pamoja na wabia wenzie, maana hili la kwao, wamehamia kuuza sehemu ya *share* kwa Twiga ambaye yeye anataka ku-*invest* dola milioni 400 sawa na shilingi bilioni 930. Yeye ndiyo ameona huyu sasa anataka kutupa hizi fedha. Wamekubaliana wao, sasa sijui kizungumkuti kiko wapi.

Mheshimiwa Spika, sasa kama kuna mwingine alikuwa na fedha nyingi tulitarajia angewafuata *Tanga Cement* wakubaliane, kwa sababu hapa ni biashara huru. Wao wenyewe wana mamlaka ya kuchagua waende kwa nani, kwa namna gani wao wanaweza kuokoa eneo hili. Kwa hiyo tunahitaji tupewe maelezo ya kina lakini huyu ambaye anataka ku-*invest* hapa ni mlipakodi mzuri. Mwaka jana amelipa zaidi ya shilingi bilioni 80 lakini hapa *Tanga Cement* wamepata hasara zaidi ya shilingi bilioni 46, hawawezi kujiendesha, kizungumkuti kiko wapi hapa?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafanya uchunguzi wangu na nikapata taarifa; nimesoma Gazeti la Jamhuri la uchunguzi la tarehe 24 mwezi wa nne. Limesema, kwa sababu kulikuwa kuna hoja, ooh! huyu akimilikishwa kuna suala la ku-*dominate* soko. Sasa nikaambiwa Tume yenyewe ya Haki ya Ushindani ilifanya kikao na hawa wazalishaji 12 wa saruji, na wakasema kwamba sisi hatuna nongwa, hakuna suala hapa kwamba hawa wata-*dominate* soko kwa sababu mazingira ya sasa hivi yamebadilika, wapo watu ambao wana uwezo wa kuzalisha zaidi ya tani 1,000,000 ya *cement.*

Mheshimiwa Spika, hata kama sasa hivi Twiga anaongoza, Dangote akiamua kufungulia mitambo yake naye anaweza akaongoza vile vile. Huyu mwingine naye akiamua kuongeza

uzalishaji naye anaweza akampita Dangote anaweza akampita Twiga, suala la *dominant* hapa liko wapi? Tunaomba utuelezee. Na nikaambiwa kati ya hao wazalishaji 12 kuna wengine hawakwenda. Hawakwenda kumbe kwa sababu hawazalishi. Sasa tunahitaji tupewe maelezo ya kina hapa tujue *interest* ya taifa iko wapi hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tupewe maelezo ya kutosha; na mimi sitaki kuwa na upande na hizo siyo tabia zangu. Tunataka kujua *interest* ya taifa iko wapi? Mnufaika ni nani? Yaani kama wenyewe wazalishaji wamesema hakuna nongwa, tatizo linakuwa wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri uje utuambie hapa tupate maelezo ya kina ili sintofahamu ziondoke. Maana hapa isije ikawa tunaingizwa kucheza ngoma ambazo hazituhusu, na hizi ngoma inawezekana ziemanzia kwenye Wizara yako huko huko kuna, makundi kwa sababu kuna *interest* za watu. Tunahitaji majibu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ukija hapa hebu tueleze hili suala la ukomo wa asilimia 35 limekaaje. Hivi, kama mtu aliomba kwenye mazingira hayo ya kipindi hicho akakataliwa, hivi ni *alpha* na *omega?* Hana *room* ya kuomba tena? Waliokataa hawana *room* ya kukubali kwamba sasa hivi mazingira ya uwekezaji yamebadilika? Ikoje hii?

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri tunaposema tunavutia wawekezaji kuna wawekezaji ambao wameshaanza ku-*invest*. Tunajua mitaji yao, tunajua uwezo wao, tumewaona; hawa wanatakiwa walindwe. Nilikuwa nakumbuka kulikuwa kuna sarakasi moja hapa ya *issue ya* Dangote akataka kuondoka, kwa taarifa nilizonazo Serikali ikabidi mwende kumbembeleza ili abaki. Tunazungumzia hapa Liganga na Mchuchuma kuna muwekezaji amekaa pale muda mrefu, leo Serikali inabidi muende

mkawalipe fidia ili muanze uzalishaji kwa sababu alikuwa hana *capacity* hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunataka tuendeleze uwekezaji wa *briefcase?* Kama tutakuwa wakweli na tunaipenda nchi hii nyekundu iwe nyekundu, njano iwe njano, uweke historia. Mara mia uhukumiwe kwa kusema ukweli lakini siyo uhukumiwe kwa kupindisha mambo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vuma Agustine Holle atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula ajiandae.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia leo kwenye Bunge lako Tukufu. Nikushukuru pia wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais na wasaidizi wake, kwa maana ya Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kuhakikisha kwamba Wilaya ya Kasulu au Mkoa wa Kigoma kwa ujumla tunapata kiwanda cha kuzalisha sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hapa kwa sababu kwa miaka mingi iliyopita Wabunge wa Mkoa wa Kigoma tume-*push agenda* hii humu humu Bungeni na hatimaye Serikali iliweza kuweka mazingira mazuri na hatimaye mwekezaji wa *Mufindi Papers* au *Kasulu Sugar* ameanza shughuli zake pale, wamepanda miwa na ujenzi wa kiwanda unaendelea. Tunaamini muda siyo mrefu Wilaya ya Kasulu kutakuwa na kiwanda kikubwa sana cha sukari katika Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo hapo nimpongeze Mheshimiwa *DC* na Mkurugenzi kwa kazi nzuri waliyofanya kuhakikisha kwamba wana-*manage* changamoto ndogo ndogo ambazo zilikuwa pale kwenye vijiji husika, hasa wakati wa kupata ardhi na mambo mengine, na kuhakikisha kwamba muwekezaji anaendelea na shughuli zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nimeona kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri, anasema Benki ya Kilimo imetoa bilioni 47 kwenye mwaka wa fedha uliopita kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao na kuongeza thamani ya mazao.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Kilimo inafanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba inawezesha viwanda kwa kuchakata mazao mbalimbali kwenye kilimo na uvuvi. Sasa tumeona kuna *initiative* nyingi sana za Serikali kwenye kilimo na sehemu zingine, lakini bila kuwa na viwanda ambavyo vinachakata mazao hayo ni ukweli usiopingika kwamba kilimo chetu hakiwezi kuwa na tija na mkulima hatuwezi kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ya *PIC* ilipendekeza kwenye taarifa yake ya mwaka uliopita kwamba Serikali iiongezee mtaji Benki ya Kilimo, bilioni 100. Ni vizuri, tunataka kujua kama Bunge au wananchi Serikali imefikia wapi katika kutekeleza jambo hilo? Kwa sababu kwa kufanya hivyo tunaamini watu wengi watakopeshwa. Hata wa Mkoa wa Kigoma tumepata fursa ya kupewa, kuna mwekezaji amepewa mkopo tunajenga Kiwanda cha Kukamua Mawese Mkoa wa Kigoma, tulikuwa hatuna.

Mheshimiwa Spika, Dodoma hapa wamejenga Kiwanda cha Kukamua Mchuzi wa Zabibu. Kwa hiyo lazima tuimarishe, lazima Serikali iwape fedha ya kutosha Benki ya Kilimo ili iweze kuhakikisha inawezesha ujenzi wa viwanda kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, na mimi nitagusa suala hili la *cement* kidogo. Kwa nini nagusa; naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize kwa makini sana. *Cement* kwa Dar es Salaam inauzwa mfuko mmoja shilingi 14,000. *Cement* Kigoma au Kasulu Vijijini mfuko mmoja unauzwa shilingi 28,000, yaani ni mara mbili ya Dar es Salaam. Sasa tumepiga makelele sana kwa maana ya kuishauri Serikali kuendelea kuongeza *production,* yaani uzalishaji na Serikali imechukua hatua ya kushawishi wawekezaji nje ya nchi na ndani ya nchi ili wawekeze kwenye viwanda vya *cement* ili *cement* na kule Mbeya, kule Kigoma iweze kushuka iwe kama Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, sasa amepatikana muwekezaji kwenye kiwanda ambacho kinasuasua anataka kuleta *over one trillion* halafu inakuja *movement* ya kupinga jambo lile kwa sababu kuna *technicalities* eti hazikufuatwa. Sasa nimefikiria unakumbuka hata wakati tunaanza ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere walikuja watu hapa wakasema tumekiuka Sheria za Mazingira. Wakati tunaanza ujenzi wa *SGR* walikuja watu wakasema mnakiuka moja, mbili, tatu. Nataka niseme nampongeza Mheshimiwa Waziri na *FCC* kwa maamuzi ya kijasiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii tumekwamakwama kwa sababu ya kukosa maamuzi wakati mwingine. Vitu vidogo vidogo unakuta vinamzungusha mwekezaji mpaka anaamua kurudi kwao, hatuwezi kwenda namna hiyo, *no thank you. You can not reject* wawekezaji wa *over one* trillion eti kwa sababu kuna *technicalities* za mwanzo hazijafuatwa. Nilidhani wakati tunachangia hapa, tulipaswa tumpongeze kwanza Waziri, halafu tutoe ushauri wa namna ya Kwenda, tuwe *supportive* sio ku-*discourage,* eti unakataa *one trillion* unaijua wewe vizuri, unaijua *one trillion* vizuri wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hela ni ngumu jamani, hatukubaliani. Lazima huyu mwekezaji atiwe moyo, lazima huyu mwekezaji apewe nguvu, apewe mwongozo wa kutosha kwa maslahi ya Watanzania, hasa wa Kasulu Vijijini ambao wananunua *cement* kwa shilingi 28,000 wakati Dar es Salaam wananunua kwa shilingi 14,000 *we cannot accept this.*

Mheshimiwa Spika, hongera Mheshimiwa Waziri anafanya kazi vizuri, lakini sasa ukiangalia hofu ya watu, nilijaribu kuongea na watu hasa wa Mkoa wa Tanga ambako ndio kuna kiwanda chenyewe. Hofu yao kubwa wanasema kwamba huyu akinunua hiki kiwanda kinaenda kufa na walitoa mfano wa baadhi ya viwanda ambavyo vimeshakufa. Wakasema viko viwanda kadha wa kadha ambavyo vimekufa pale.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kujua, *FCC* kwenye mashauri yao wana *ruling* za aina tatu. Moja kumpa mtu yaani anunue au a-*merge* katika jambo hili. Jambo la pili, unampa bila masharti, unampa tu bwana tumekubali, hakuna masharti yoyote, nunua. Jambo la tatu, unampa na masharti, masharti haya ndio ambayo yanaweza kusaidia kumlazimisha ili *production* ya eneo lile iendelee na kiwanda kisifungwe au kumkatalia. Sasa naamini Waziri atakapokuja hapa atakuja kuwaambia vizuri, huyu mtu anakubaliwa kwa misingi gani, anapewa bila masharti au anapewa mashati. Ningeshauri apewe kwa masharti kwa maana ya kwamba tuwe na uhakika kwamba tukimpa kiwanda kile haendi kukifunga, anaenda kukiendeleza, hivyo, ajira zinaendelea kuwepo na *cement* ya kutosha inakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.  Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Sylivia Francis Sigula na Mheshimiwa Patrobas Katambi ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Nianze kabisa kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na jopo lake. Hatuna mashaka na weledi wao ndio maana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amewaamini.

Mheshimiwa Spika, leo nitaongelea mambo mawili katika bidhaa za makundi mawili tu, bidhaa ambazo zinaingizwa ndani ya nchi yetu. Tumekuwa na kasumba ambayo imekuwa siyo nzuri sana inapokuja kwenye kuingiza bidhaa nchini. Kila kitu kwa asilimia kubwa tunaingiza. Nikawaza itafika wakati tutaingiza mpaka dhambi.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, nitaongelea mambo mawili. Jambo la kwanza natamani kuongelea kuhusiana na mradi wa chumvi. Wabunge wenzangu wengi wameongea vizuri kuhusiana na chumvi, wamefafanua vizuri sana. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha, nilipouliza swali la msingi hapa kuhusiana na Kiwanda cha Chumvi Itumbula sikujibiwa kikamilifu. Tunaamini kiwanda kile cha chumvi hakitawasaidia tu wananchi wa Jimbo la Momba kupandisha mapato kwenye halmashauri yetu, lakini ni kiwanda ambacho chumvi inayozalishwa pale inaweza kusaidia Mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini na ambapo Wabunge wengine wametangulia kusema hapa kwamba, tuna uhitaji mkubwa sana wa chumvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bidhaa nyingine ambayo nataka kuongelea hapa ni uingizwaji wa pombe nchini kwetu. Katika imani zetu hapa, Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hatuna dini, lakini wananchi sisi ndio tuna dini. Sasa

najiuliza kama wananchi tuna dini na kila mtu kwa imani yake, wapo tunaoamini pombe ni dhambi na wengine wanaamini pombe ni haramu.

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme mimi sio mtumiaji wa pombe, lakini sina sababu ya kutokutetea maslahi ya watu ambao wanatumia pombe na kama zipo nchini kwetu zinatumika.

Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho nilipokuja hapa nikazitetea pombe zetu za kienyeji, sikupewa majibu mazuri na Serikali na Mheshimiwa Simbachawene akaahidi vizuri sana hapa kwamba atalifanyia kazi na Mheshimiwa Waziri ni huyu huyu na Naibu Waziri ni huyu huyu.

Mheshimiwa Spika, leo nimekuja na pombe zenye thamani kubwa sana hapa, nataka Mheshimiwa Waziri aniambie hizi pombe ziko hapa nchini zinafanya nini na hizi pombe kwa namna zinavyouzwa bei ghali. Hapa nimekuja na pombe mpaka ya 270,000. Hizi pombe nimeenda kuzinunua kwenye hoteli kubwa hapa Dodoma pale Morena kwa Shabiby, ambapo naamini watu ambao wanakwenda sehemu ile ni Mawaziri wenyewe, Makatibu Wakuu wa Wizara, labda na Wabunge wenyewe na wafanyabiashara wakubwa wakubwa. Sasa swali, kama Serikali haina dini na pombe ni dhambi hizi pombe zinafanya nini hapa nchini?

*(Hapa Mhe. Condester M. Sichwale aliweka juu mezani chupa za pombe mbalimbali)*

**MHE. CONDESTER M. SICHWALE:** Mheshimiwa Spika, kuna smirnoff, nisaidie kutoa mama, *green fish* wanywa pombe wanajua, sijui kuna Hennessy, kuna Jack Daniels, kuna hennessy nyingine, hii inaitwa Gordonson. Haya naomba hizi za Tanzania, hizi ndio za kwetu za Tanzania zinazozalishwa hapa K-Vant na

Konyagi. Swali langu hizi zote nimenunua Morena kwa Mheshimiwa Shabiby, zinagharimu zaidi ya Sh.500,000 hapa zilipo. Swali najiuliza hizi pombe zinafanya nini? Tafsiri yake wapo watu ambao wanatumia hizi.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaulize Watanzania wenzangu walioko huko nje na Wabunge walioko huku, ni nani ambaye mtoto wake akienda kufanya kazi kwenye Kiwanda cha *TBL* atakataa, atasema ni dhambi. Tufanye sasa hivi awe ni Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda cha *TBL,* nani atazungumzia masuala ya dhambi hapa? Nataka kujua ni Watanzania wangapi ambao watoto wao wanafanya kazi kwenye Kiwanda cha Konyagi? Ni Watanzania wangapi ambao watoto wao wanafanya kwenye Kiwanda cha *K-Vant* wangapi, hawapati hiyo mishahara?

Mheshimiwa Spika, sasa najiuliza kwa nini pombe zetu mfano wa pombe ya gongo zinamwagwa, vijana wenzangu wakimbiza Mwenge kule Mtwara walimwaga pombe za Watanzania wapika gongo. Kwa nini tunadharau ubunifu wa Watanzania? Kwa nini tunadharau mawazo ambayo ni ya Watanzania. Sasa najiuliza, kwani viwanda maana yake nini? Viwanda si huwa vinaanza na wazo, mtu akipata wazo si ndio atengeneze bidhaa kwa hali ya kawaida.

*Mheshimiwa Spika, hao China wanaotuletea makorokoro feki humu nchini kwetu wanafanyaje? China kila mtu hata mtoto wa miaka 10 ana kiwanda chao wanatengeneza ma-product mabovu ndio wanatuletea huku kwenye nchi zetu.*" **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, sasa sisi kama yupo Mtanzania ambaye anaweza akapata wazo la kutengeneza gongo mpaka watu wakalewa, jamani si Mtanzania huyu alipaswa apewe *support*.

Sasa Serikali ubunifu ambao inautaka inataka ubunifu upi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, angalia pombe hizi zote ambazo unaziona, siku moja Mheshimiwa Waziri Bashe akiwa anaongea huko kwenye viwanda vyake vya miwa huko, anapongeza namna ambavyo wanzalisha sukari. Akawa anasema namna ambavyo wanazalisha *Molasses* wanauza kwenye nchi za nje ambazo wao ndio wanatuzalishia hizi wanatuletea sisi tunakunywa. *Molasses* inatengenezwa kwetu halafu wanasafirisha kwenda nje sisi tunarudi tukaanze kunywa pombe. Imani zetu Serikali zinasema pombe ni dhambi…

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, sasa hii dhambi inafanya nini hapa nchini kwetu?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Mtibwa mwaka huu fedha…

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, walizalisha *molasses* tani…

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, muda hautoshi jamani.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Subiri kidogo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba pamoja na uzuri wa hizo chupa hizo bidhaa alizoziweka mezani, hata watumiaji wengi hawajui imetengenezwa na vitu, lakini hiyo aina ya pombe inayotengenezwa Tanzania, inafahamika kwamba *material* yake yanatoka shambani na yanatoka wapi. Kwa hiyo ni suala la Serikali kuongeza kuwapa motisha wanaotengeneza. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, napokea taarifa ya Mheshimiwa Aida. Yeye Mheshimiwa Aida…

**SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe subiri kidogo inabidi uitwe ndio uanze kuzungumza. Mheshimiwa Sichalwe unapokea taarifa hiyo.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, napokea na wewe kule Ilolo, Mafyati kule Mabatini una wapiga kura wengi ambao mimi nawafahamu na nawajua wanatengeneza pombe za kienyeji. Kwa hiyo mimi na wewe tuna wapiga kura ambao wanatengeneza pombe za kienyeji. Bahati mbaya inawezekana hawatengenezi gongo lakini Kimpumu, Kindi, Komoni, Isute, zote hizo ni pombe za kienyeji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa najiuliza tunapohubiri ubunifu, ubunifu upi ambao sisi kwenye nchi yetu tunauhubiri. Kuna wachangiaji wamepita hapa aliongea Mheshimiwa Tauhida Gallos jana, akasema kuna vijana wa kitanzania ambao wanaweza kutengeneza *system* ambayo mtu akiwa mbali ikaweza kuzima umeme nyumbani kwake. Najiuliza hivi vijana hawa wa Kitanzania waweze kutumia akili yote hiyo kuja na

utaalam wote huo washindwe kutenganisha kati ya *methanol* na *ethanol* kwenye gongo. Maana yake ambacho kinazuiliwa hapa kwenye matumizi ya gongo eti ni *methanol* ambayo sisi tulitegemea.

Mheshimiwa Spika, nimeenda zaidi, nimewasiliana na Profesa wa…

**TAARIFA**

**SPIKA:** Haya achilia hapo hapo kwenye kuwasiliana utaanzia hapo, Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka kumpa mzungumzaji taarifa kwamba wakati wakulima wa korosho wanalalamikia bei ndogo ya korosho ghafi, matunda ya korosho kwa maana ya mabibo yana uwezo wa kutengeneza pombe bora tena yenye virutubisho, lakini huo ubunifu haujatumika kulifanya hilo bibo litengeneze pombe bora, ambayo itatumika na Watanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, napokea.

Mheshimiwa Spika, nimewasiliana na Profesa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam najiuliza kwenye nchi yetu kuna chuo kinachoaminika kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Profesa Kessy pamoja na watalaam wenzake Maprofesa wengine huko sijui Profesa Muhinzi, Profesa Athuman, wanasema wameshafanya utafiti kwenye suala la gongo na pombe zingine za kienyeji. Hakuna madhara makubwa ya kiafya. Serikali inachokikatalia kwenye gongo ni *methanol* iliyopo kwenye

gongo, lakini wanasema iko mitambo ambayo wala sio shida kutenganisha…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** …*methanol* na *ethanol* kwenye gongo ili iweze kufaa…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Sasa kama watu wanasema eti gongo yetu sisi ina matatizo kwa sababu haijatenganishwa. Kwa hiyo Jack Daniel anakunywa nani? Jack Daniel kwenye nchi hii anakunwa nani? tumezikuta pale Morena. Mwananchi wa kawaida mwenye kipato cha Sh.2,500 anaenda Morena pale? Maana yake wanakunywa matajiri wa nchi hii…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, sasa gongo haifai, Watanzania tabia ya sisi kudharau vitu vya kwetu ndio hiyo sababu tuna-*import* mpaka dhambi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Sichalwe, subiri kidogo, Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nampa taarifa mzungumzaji, Mbunge wa Momba, kwa uzoefu mimi natumia hivyo vitu, wala msicheke tupo wengi tu na wala sio dhambi. Natumia hivyo vitu alivyoweka mezani na watu wengi wanaovipinga wanavipinga hasa wanapokuwa makazini, lakini wanapostaafu baada ya miezi miwili, mitatu, wateja wakubwa wa hizo pombe ulizoziweka kushoto Konyagi na K-Vant ni Maprofesa na Madaktari na nina *research* niliyoifanya mwaka jana. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, napokea taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ameshapewa taarifa tatu zinamtosha, tumwache amalize hoja yake, Mheshimiwa…

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, unipendelee na muda kidogo ni ombi tu kwa faida ya Watanzania.

**SPIKA:** Nakupa sasa nafasi ili utulie, uchangie vizuri hoja yako.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana mama.

**SPIKA:** Unaipokea kwanza taarifa ya Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nimepokea, natetea na wapigakura wako wa Jimbo la Mbeya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza Kiwanda cha Manyara *Sugar* wana-*export molasses* tani 1,500 katika mwaka huu wa bajeti tulionao. Sasa ombi langu kwa Serikali ni hili, mimi natoka kwenye familia ya watu wenye dini, sinywi pombe, mlokole mzuri tu, lakini hizi pombe hapa zinafanya nini?

Mheshimiwa Spika, zipo Serikali duniani ambazo zenyewe zimejipambanua kwamba ni Serikali za kidini, mfano Falme za Kiarabu, ni watu ambao hatushangai, wao wanasema Serikali yao inaamini dini, lakini nawauliza watu ambao wameenda

kwenye *state* zote za kule Falme za Kiarabu, Sharjah, Abu dhabi, Dubai hakuna mtu hakuti hizi pombe?

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, kila Serikali inaamini dini, lakini hizi pombe zipo kwenye hizo nchi.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, sasa sisi kwa nini…

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, sasa sisi kwa nini tunakataa utaratibu…

**KUHUSU UTARATIBU**

**SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe kuna kanuni inavunjwa, yuko wapi anayesema kuhusu utaratibu.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hussein.

**SPIKA:** Kanuni inayovunjwa Mheshimiwa.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kanuni ya 75, kanuni ambayo imevunjwa, huwa tunapita pale kwenye *security,* ukiwa hata una chupa moja ya maji wanaizuia. Je, hili suala linaruhusiwa kuingiza vifaa kama hivi Bungeni?

**SPIKA:** Sasa kuhusu utaratibu inabidi kanuni iwe inavunjwa na yule anayehusika, kwa hivyo wewe unaliza kama amevunja kanuni au hajavunja kwa kukaa na hizo pombe hapo, ndio swali lako?

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, swali langu ni hilo kwamba je amevunja kanuni au la?

**SPIKA:** Ahsante sana. Amefuata utaratibu kuingiza pombe humu ndani, kwa hiyo hajavunja kanuni yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Condester Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, mimi sitaki kutenda dhambi, kushika tu pombe inawezekana ni dhambi. Baba yangu namheshimu sana, yale aliyofanya nyuma yanatosha, busara yangu na hekima yangu asiitumie vibaya, mimi ni mtoto mdogo namheshimu kama baba yangu mzazi. Mimi sio kichaa, yaani Spika na usomi wake wote huo halafu mimi nikurupuke kufanya hivi vitu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema kwamba, nataka kusema nini? Nataka kusema tunapoongelea viwanda vinaanza na mawazo ya mtu wa chini, vinaanza na mtu wa kawaida, tuheshimu mawazo ambayo yanatolewa na Watanzania wenzetu, tuheshimu mawazo ambayo yanatolewa na watu wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi K-Vant na hizi Konyagi ni pombe za Watanzania. Sasa hivi Serikali ya South Africa itokee itangaze kwamba inatangaza ajira 100,000 kwa watu wakafanye kazi kwenye viwanda vya *wine,* Watanzania lukuki watamiminika kwenda pale.

Mheshimiwa Spika, tukienda huko duniani *wine* za *South Africa* ndio zinaheshimika wakati zabibu inalimwa hapa Dodoma na Dodoma *wine* inauzwa shilingi 10,000. Halafu Mheshimiwa Waziri wakati alikuwa anajaribu kuongelea sehemu ambazo wamepata masoko huko sijui mpaka pilipili, mbona alikuwa haongei kama K-Vant na yenyewe ni *most selling* pombe kwenye huko nchi za *East African Community*? Si ni bidhaa ya Watanzania. Kwa nini hawajivunii na hizi bidhaa, mbona hivi wanapitisha bandarini, *TBS* wao wanafanya kazi ya kupima hivi tu, ila *TBS* kwenda kukaa kushirikiana mawazo na watu wa chini kwamba huyu mtu asiyejua kusoma na kuandika anawezaje kutengeneza kindi, komoni, kimpumu watu wakalewa wanashindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona Serikali imeweka nguvu tu kwenye kukataza gongo. Ziko baadhi ya pombe nyingi sana pia za kienyeji kwenye jamii zetu zina madhara. Kwa mfano kule kwa Profesa Mkenda, kuna hii pombe moja huku inaitwa vimolari hivyo vimolari kule Rombo inasemekana vinauwa nguvu za kiume vya wanaume wetu huko Rombo. Sasa najiuliza hayo mawazo ndio yalibidi yachukuliwe, yaani kama iko pombe ambayo Mtanzania anaweza akapata wazo, akatengeneza mpaka zikauwa nguvu za kiume za mtu huyu, si ilitakiwa ndio hiyo pombe itumike kuwafanya hawa wanaume ambao wanawaingilia watu kinyume na maumbile ili wasiteseke, kwa sababu tayari ni maarifa hayo. Sasa wanataka maarifa gani?

Mheshimiwa Spika, hizi pombe kwa sababu zimetoka Ulaya na zimepewa majina mazuri sijui *smirnoff* sijui kitu gani, hiyo ndio heshima, lakini ujuzi wetu wa ndani unadharauliwa.

Mheshimiwa Spika, ifike muda…

**SPIKA:** Dakika moja malizia.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ifike muda sisi tuache kasumba, kasumba hapa ndio inayotuponza, kasumba hapa ndio inatuletea shida. Kama soko la ndani linaonesha kuna wanywaji wa pombe wanatumia pombe. Niombe Serikali iwatumie vijana wa Kitanzania, Maprofesa na wasomi ambao wanasema wapo tayari kufanya *research,* kumsaidia mwananchi wa kawaida kuboresha pombe yake. Zile pombe ambazo zinakaa siku tatu hazina kazi tena haziwezi kupakiwa. Nilishakuja na vipombe vidogovidogo hapa vya Sh.3,000, tumsaidie mwananchi huyu aweze ku-*pack*, viweze kuuzwa kwenye nchi zetu za Jirani. Huko ndio kuinua uchumi. Tunapoongelea uchumi wa viwanda inabidi uanze na mtu mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mama Samia peke yake na matajiri hawa wachache, hawawezi wakajenga hii nchi, nchi hii itajengwa na Watanzania wenyewe kwa kuzingatia shughuli zao za kawaida ambazo wanafanya. Ni nani huko kijijini ukiacha kulima na kufuga biashara ambazo wananchi wa kawaida wanafanya ni nini, si ni pombe za kienyeji?

Mheshimiwa Spika, ninayo orodha ya Maprofesa wakubwa hapa nchini hapa, wakubwa wengine mpaka ni aibu kutaja, ukitaja watu watabaki wameshika mdomo, ambao wamesoma kwa kutumia pombe za kienyeji ukiacha gongo. Pia hizo gongo wanakunywa, tabia ya kujifanya watu ni watakatifu, wakati watenda dhambi kama watu wengine wapo hapa, kuwajaji watu ni wa kwanza, lakini laiti Mungu angeleta karatasi zao hapa, tukafunua dhambi zao, watu wangeweza kukimbia na wasingeamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri leo aje aseme ana mkakati gani. Kama hawataki pombe, ushauri wangu basi tuseme Tanzania ni nchi ambayo haihitaji pombe ili tujue moja. Hakuna pombe nchini kwetu na pombe za kienyeji

zisithaminiwe na gongo ndipo ziendelee kuitwa haramu, lakini kama pombe zitaendelea kuingia, ni lazima tutambue ubunifu wa watanzania wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeishamtaja Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, atafuatiwa na Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ajiandae.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Uwekezaji Viwanda na Biashara. Nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha leo kusimama katika Bunge lako Tukufu. Kwa namna ya pekee sana namshukuru Rais wetu, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyopambana kutengeneza mazingira wezeshi kwa wawekezaji wetu wa ndani na nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa na mambo mawili tu ambayo ningependa nichangie asubuhi ya leo. Tunapoiangalia Wizara hii ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara sisi wawakilishi wa vijana tunaziona ajira, tunaona ndiye mkombozi wa changamoto zetu sisi vijana. Nitaongelea kuhusu ubunifu kidogo.

Mheshimiwa Spika, bado tunaona kuna changamoto katika Wizara hii. Bado hatuna mikakati, wala mpango ambao unawezesha vijana wetu wabunifu na wavumbuzi. Nasema haya kwa sababu moja, mbili au tatu. Katikati hapa, miaka miwili, mitatu hii, kumetokea vijana wavumbuzi wengi. Tumeona vijana wamevumbua *local radios,* wamevumbua magari, matrekta na

ubunifu mbali mbali, lakini bado hatujaona mwendelezo wa bunifu zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Mkoa wetu wa Kigoma kuna kijana amevumbua *local radio,* lakini hatuoni mwendelezo wa ubunifu wa kijana yule. Hatuoni Serikali inapoingia kumsaidia kijana yule kuendeleza ubunifu wake. Bado Serikali haijaweka mikakati mizuri ya kuwasaidia wabunifu wetu wa ndani. Hapa Waheshimiwa Wabunge wameongea vizuri, kama ambavyo wabunifu wa pombe wameelezwa, na kama ambavyo wabunifu wa magari wameelezwa, lakini bado hatuna mikakati ya kuendeleza bunifu zao.

Mheshimiwa Spika, naongea haya kwa sababu, ilitokea hapa mwaka 2021, kuna kijana mmoja alivumbua *radio,* lakini cha kushangaza, badala ya kusaidiwa kwenda mbele zaidi, tukasikia kijana yule kapelekwa *Form Five* na *Six*. Sasa unajiuliza, kwa kijana mbunifu, kijana ambaye amekaa, ametengeneza wazo, nini kilipaswa kufanyika? Kumwendeleza katika wazo lake, au kumpeleka shule akasome *Form Five* na *Six* ambayo haimsadii sana kama wangeendeleza ubunifu wake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili napenda kushauri, sisi kama Wizara tuje na mkakati wa *incubation centers*. Tunaposema *incubations centers,* hivi viwe vituo vya wavumbuzi na wabunifu. Tukiwachukua hawa wavumbuzi na wabunifu tukawaweka pamoja, kwanza inakuwa rahisi kuwapa elimu, kuwaendeleza na pia hata tukiamua kuwapa uwezeshaji wa kimitaji ni rahisi kuwa-*manage* na kuwafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *incubation centers* hizi zitatusaidia. Wizara inapokuja kutoa taarifa, inaweza kutuambia, katika miaka miwili hii tumepokea wabunifu sita, tumewaendeleza hivi, wamefikia hapa, na mchango wao kwa Taifa ni huu. Leo Wizara inaweza isiwe hata na *database* ya wabunifu kwa sababu bado

mikakati na mipango hatujaiweka vizuri. Kwa hiyo, nashauri sana Serikali kuhusu suala la *incubation centers*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ukisoma ukurasa wa 11 na wa 10 wa Hotuba ya Waziri, ameeleza vizuri namna ambavyo Serikali imejitahidi sana kuwasaidia wazalishaji wa zabibu. Nami nachukua nafasi hii kuwapongeza, kwa ambacho mmekisema mmewasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme jambo moja, ukiangalia wazalishaji wa zabibu, hata kama Serikali inasema imewapatia soko kwenye viwanda vidogo vya hapa Dodoma, bado changamoto ya soko ni kubwa sana. Nasema haya kwa mambo makubwa mawili; sijui kama Mheshimiwa Waziri ana taarifa, viwanda hivi vidogo ambavyo mnasema Serikali imewasaidia wakulima wa zabibu, kwamba bado vinashindwa kuwalipa wakulima wa zabibu kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo mkulima wa zabibu analima mwenyewe, akimaliza kulima anapeleka kiwandani zabibu zake, lakini inamchukua zaidi ya miezi nane mpaka mwaka kuweza kupata pesa yake. Pesa yenyewe anaipata kwa awamu na kidogo kidogo. Leo mkulima huyu amepeleka kiwandani zabibu za shilingi milioni mbili, anaambiwa leo anapewa shilingi 200,000, anaambiwa uje baada ya miezi miwili upewe shilingi 300,000, uje baada ya mwezi upewe shilingi 100,000. Kwa mazingira hayo, wakulima hawawezi kupenda kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nini kifanyike hapa? Pamoja ya kuwa mmewatafutia soko kwa viwanda hivyo, bado viwanda haviwalipi wakulima kwa wakati. Ukiongea na wamiliki wa viwanda, changamoto yao ni uwezo mdogo. Kwa hiyo, kwa sababu changamoto ni uwezo mdogo, hawawezi kuchukua zabibu zote na kuwalipa kwa wakati. Nini kifanyike? Kwanza naishauri Serikali iweze kuwasaidia hawa wamiliki wa hivi viwanda

vidogo iweze kuwapatia mikopo ya uwekezaji. Hatuwezi kuwasaidia viwanda hivi kama tutawapa mikopo ya kibiashara, haiwezekani. Kwa sababu mikopo ya kibiashara ina riba kubwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali iingilie kati jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuliko kutumia nguvu kubwa kuanzisha mashamba mapya, ni bora kutumia nguvu hiyo kwenda kuwawezesha watu ambao tayari wapo *site,* wanafanya shughuli hizo. Hii itawasaidia waone umuhimu wa kilimo na kuhamasisha wengine. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, nguvu kubwa inayotumika kuanzisha mashamba mapya ni bora itumike nguvu hiyo kuwasaidia watu ambao tayari wapo *site* na wana changamoto ya kukuza mitaja yao ili waweze kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda sana niongelee *SIDO,* kwa sababu sisi kama vijana tulitamani na tulifikiria ingeweza kuwa mkombozi wetu, lakini Mheshimiwa Waziri bado una haja ya kupitia hizi *SIDO,* kwani nyingi hali zao ni tete. Sisi Kigoma pale na Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi karibuni alienda pale kuzindua kiwanda cha kuchakata mafuta, lakini ukikiangalia kiwanda kile utaona, bado kiwanda kile hakina *level* ya kiwanda cha kisasa. Bado mzunguko wake ni mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hatutawekeza nguvu kubwa kwa *SIDO*, kama hatutatoa pesa kuwekeza *SIDO,* bado tutaendelea kuagiza vitu nje, bado tutaendelea kuagiza mashine nje na *SIDO* haitakuwa na umuhimu tena. Leo ninavyoongea hivi, Watanzania wengi hawafanyi biashara na *SIDO* tena, wanaenda zao kuagiza vitu nje. Kuliko niagize kitu *SIDO,* kitu chenyewe bado ubunifu wake au teknolojia yake ni ya kizamani, bora niagize zangu kitu tu nje kwa haraka na gharama nafuu, lakini pia kinakuwa kiko *updated.* Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iwekeze nguvu sana katika *SIDO* ili vijana wengi wapate ubunifu huko na itusaidie kupata mashine nyingi, vijana wengi waweze kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, ukiona mtu mzima analia, ujue kuna jambo. Jana nimesikiliza michango ya Wabunge wa Mkoa wa Tanga, na nimesikiliza michango ya Wabunge wengi, nikajiuliza kunani Tanga? Ikabidi nifuatilie. Nimeenda kusoma hukumu ya *Fair Competition Tribunal* nikabaki najiuliza. Hivi kweli katika nchi inayoongozwa na sheria, nchi inayofuata mifumo ya sheria, nchi kama hii ya kwetu, hivi chombo cha Serikali kinapata wapi ujasiri wa kupingana na maamuzi ya Mahakama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana atakapokuja Mheshimiwa Waziri atuweke wazi, aondoe hii sintofahamu iliyokuwepo, atuelezee jambo hili ili tuweze kulielewa. Pia kuna haja sana ya sisi kama Watanzania kufuata sheria zetu. Tumeweka za nini kama tuna sheria na bado hatuwezi kuzifuata? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, Serikali iokoe viwanda vya mkonge, okoeni ajira.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wizara kwa wasilisho la bajeti na ninaomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tuokoe zao la mkonge na viwanda vyake. Katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025 imetaja kuzalisha ajira milioni nane, ni wazi kuwa ajira hizi kwa kiasi kikubwa zitatokana na mnyororo wa thamani kuanzia katika malighafi za kutoka mashambani/kilimo hadi

viwandani *(agro-processing industry)*. Ajira hizi pamoja na viwandani itaendelea hadi sokoni.

Mheshimiwa Spika, ni masikitiko makubwa sana kwamba wakati tumeamua kufanya zao la mkonge kuwa zao la kimkakati, hakuna jitihada za makusudi za kulinda viwanda vya kuchakata zao la mkonge kwa maana ya kulinda soko. Ndani ya Serikali hakuna ufuatiliaji wa maagizo na maelekezo ya Waziri Mkuu Septemba, 2021 na rejea yake Novemba, 2021 kwamba Wizara inayohusika na Mazingira kwa maana ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira izuie *importation* ya kamba za *plastic* ambazo kwa kiasi kikubwa mbali ya kuvuruga soko la kamba za kitani, lakini pia zinaathiri mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, ni matarajio yangu wenzetu wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara wanayo nafasi kubwa ya kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuhakikisha kuwa zuio hilo linasimamiwa ili kuwalinda wakulima na kulinda viwanda na ajira za Watanzania kama sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Spika, *industrial park* Mafinga Mjini; tumetenga ekari 750 kwa ajili ya *industrial park* na kupitia Mradi wa *TACTIC* tutajenga miundombinu wezeshi na tayari *EPZA* walitembelea eneo hilo na kutoa ushauri, pamoja na kuwa tuko katika hatua za awali za kupanga, kupima na kumilikisha, nawaomba Wizara tufanye kazi kwa ushirikiano ili tuweze kufanikisha suala hili kwa lengo like lile la kuzalisha ajira hasa kupitia fursa ya mazao ya misitu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, naungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali za

ustawi wa amani, kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiplomasia na mambo mengi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini nachukua nafasi ya kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, viongozi/watendaji wetu wote Serikalini kwa utekelezaji wa Ilani ya CCM 2020-2025, kwa kweli kazi nyingi zimefanyika katika jimbo langu la Mbulu Mjini kwa kila sekta, hasa yale mambo mengi ambayo yaliyoshindikana muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii ya uwekezaji, viwanda na biashara. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote Wizarani na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu ni kwamba tuangalie utaratibu wa kuhakikisha maafisa wetu wa biashara ngazi za halmashauri, mikoa tuwajengee uwezo wa kuwalea na kuwajengea uwezo wawekezaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, nasema hayo kwa sababu TAMISEMI ilipoagiza kila halmashauri nchini kuwa na viwanda 100 vingi viliyoanzishwa vilitoa ajira kwa vijana wengi, lakini hadi sasa ni vichache vinavyoendelea kufanya kazi na changamoto kubwa ni ukosefu wa wataalam washauri, mitaji ya kutosha na mazingira ya ukosefu walezi. Hivyo kuna haja kubwa kulinda na kuimarisha viwanda vidogo na vya kati kwa kuwa kundi kubwa la wananchi wataajirika kwa ajira ya muda na mikataba na wawekezaji wa viwanda vidogo watakuja kuwa wawekezaji wa ndani ambao mapato yao yataendeleza uchumi wa Taifa letu na mafanikio ya wawekezaji hawa wadogo watajenga miundombinu hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachoishia Aprili, 2023 Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya viwanda na pia kuna mwelekeo mzuri wa kuboresha mazingira ya biashara *(blueprint)*. Pia kwa kusimamia vizuri diplomasia ya uchumi, imejenga imani kubwa kwa wawekezaji ambao wameonesha nia ya kuwekeza kwenye maeneo muhimu ya uchumi wetu. Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, imeendelea kutekeleza miradi mingi ya viwanda na pia kuboresha mazingira ya biashara *(blueprint)* kwa kuondoa tozo, ada na kodi ambazo zimekuwa kikwazo katika shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Spika, kupitia *blueprint* Serikali inatambua umuhimu wa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato. Pamoja na jitihada za Serikali, bado kuna mahitaji makubwa ya viwanda vya kuongeza thamani ya madini,

kuongeza thamani ya mazao yetu vijijini na pia kuna changamoto za uhakika wa masoko ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iendelee na msukumo wa kujenga viwanda vya mazao ili tuweza kuongeza thamani hapa nchini na pia kuzalisha ajira. Kutokana na neema ya kijografia, nchi yetu inazalisha mazao ya aina mbalimbali ikiwemo zao la pareto na Tanzania inaongoza Afrika, pia ni wa pili duniani kwa uzalishaji wa pareto. Uwekezaji zaidi kwenye Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha kuna fursa kubwa ya kuzalisha mbolea na hata viuatilifu kutokana na pareto inayolimwa hapa nchini. Serikali ichukue hatua za kutafuta wawekezaji wa viwanda vya viuatilifu ambavyo mahitaji yake ni makubwa hapa nchini na hata soko la nje.

Mheshimiwa Spika, pia nchi yetu ina neema ya madini ambayo ni malighafi ya kutengeneza aina mbalimbali za mbolea. Madini aina ya *calcium* (chokaa ya kilimo) na *phosphate* inapatikana kwa wingi hapa nchini na malighafi muhimu kutengeneza mbolea aina ya *CAN* na *DAP* na hata *NPK.* Kuwepo kwa gesi asilimia ni fursa nyingine kwa viwanda vya mbolea aina ya *urea* ambayo mahitaji yake ni makubwa sana Tanzania na duniani kote. Pamoja na madini hayo kuna madini adimu duniani kama vile *Niobium* ya *Panda Hill* Mbeya ambayo kuna fursa ya kujenga kiwanda cha kuchakata hayo madini ili kutengeza *Ferroniobium* ambayo mahitajika yake ni makubwa hapa nchini na pia nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mradi wa Liganga na Mchuchuma, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya *Niobium* ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanda cha *Ferroniobium (FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani. Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR,*

kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapa kwetu. Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya *Niobium* ambayo inapatikana milima ya *Panda Hill,* Wilaya ya Mbeya na mahitaji ya *Ferroniobium (FeNb end product)* ni makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahitaji kujiwekekea mikakati ya haraka *(quick wins)* ili kuhakikisha inakabiliana na athari za kiuchumi kutokana *Covid-19* na sasa vita vya Urusi na Ukraine. Kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa *Niobium* na Kiwanda cha *Ferroniobium,* ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo na ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs 7,000.* Mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 *(US$ 220 million)* ambapo mapato kwa serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 *(US$ 22 million)* uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika *(Modern Manufacturing Plant and Smelter)*. Pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi *(skills transfer)* pia itachangia huduma za kijamii *(Corporate Social Investment in Community)* na chanzo cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Spika, kutokana fursa za kijografia, napendekeza msukumo zaidi kwenye *EPZ* na *industrial parks* hasa kwenye bandari zetu na maeneo yanayozunguka viwanja vya ndege kikiwemo Kiwanja cha Kimataifa cha Songwe kilichopo Wilaya ya Mbeya.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali ichukue hatua za haraka kubadilisha matumizi ya eneo ya iliyokuwa *Tanganyika Packers* litumike kwa *EPZ* na *industrial parks* hasa kwa mahitaji ya viwanda mbalimbali ikiwemo vya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, pia napongeza mkakati wa Serikali kwa kuanzisha Soko la Bidhaa "*The Tanzania Mercantile Exchange (TMX)*." Wizara ya Viwanda na Biashara iwe mstari wa mbele kuimarisha hili soko la bidhaa ambapo wauzaji na wanunuzi wanakutana na kubadilishana bidhaa na fedha katika mtindo wenye mpangilio na utaratibu maalum. Kuanzishwa kwa soko la bidhaa kutamwezesha mkulima kuweza kuuza mazao yake katika utaratibu unaoeleweka bila kulanguliwa. Pia soko la bidhaa linatupa mwanga na mwanzo mzuri wa kuboresha soko la madini kuwa sehemu ya *TMX*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, natambua kazi kubwa inayofanywa na Wizara katika maeneo mbalimbali ya uwekezaji, lakini naomba kushauri yafuatayo:-

Kwanza baadhi ya maeneo yanazungukwa na rasilimali nyingi lakini kwa sababu ya kukosa mkakati wa kuzitumia bado jamii inayozunguka ni masikini. Kwa mfano Visiwa vya Ukerewe; uzalishaji wa samaki ni mkubwa lakini hakuna kiwanda cha kusindika hali inayopelekea mazao hayo kutokuwa na tija. Pia Ukerewe ndio wazalishaji wakubwa wa machungwa katika eneo lote la Uganda wa Ziwa, lakini sehemu kubwa huharibika na kutoisaidia jamii.

Mheshimiwa Spika, ombi na ushauri wangu kwa Wizara isaidie kushawishi uwekezaji wa viwanda vya kusindika samaki na matunda Wilayani Ukerewe ili kusaidia uchumi wa eneo hilo na Taifa kwa ujumla.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji na Naibu wake Mheshimiwa Exaud Kigahe na watendaji wote wa Wizara na taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye umuhimu wa uwekezaji kwenye sekta ya viwanda hapa nchini kwa kuliwezesha Shirika la Maendeleo la Taifa *(The National Development Corporation (NDC)* na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania *(TIRDO)*. Pia nitagusia changamoto za viwanda katika jimbo langu la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi yetu, chini ya Mwalimu Julius Nyerere tangu kujipatia uhuru na baada ya kutangaza Azimio la Arusha mwaka 1967 iliandaa mpango wa kutuletea maendeleo kwa falsafa ya ujamaa na kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, kupitia falsafa hiyo, viwanda vingi vilijengwa nchi nzima ili kusindika mazao karibu yote ya kilimo na mifugo. Kwa mfano, viwanda vya nguo vya *Kilitex, Mwatex, Urafiki, Mutex* viwanda vya korosho, kahawa, magunia, viatu, maziwa, nyama, *Tanzania Cigarette Company, Tanzania Breweries* na kadhalika. Vilevile mwaka 1965 serikali ilianzisha Shirika la Maendeleo la Taifa *(The National Development Corporation (NDC)*. Shirika hili lilianzishwa kusimamia viwanda nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali iliboresha elimu za ufundi katika vyuo vyetu vikuu na kati ili kuzalisha wataalam wa kuhudumia viwanda vyetu. Ili kuimarisha uchumi wetu, Serikali ilianzisha taasisi za kiufundi kama *CAMARTEC, SIDO, TEMDO* na taasisi ya utafiti wa viwanda *TIRDO*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana kama ilivyoelezwa hapo juu, nchi yetu ilibadilika na kukumbatia sera ya kubinafsisha viwanda na mashirika yetu ya umma kama ilivyoelekezwa na Benki ya Dunia kwa masharti ya kupatiwa mikopo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia utekelezaji wa sera hiyo, ramani yetu ya maendeleo ya Taifa ilivurugika na kudhoofisha sekta ya viwanda nchini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya viwanda katika miaka ya mwanzo baada ya Uhuru yalipatikana tukiwa na wasomi wachache sana waliobobea katika nyanja mbalimbali, leo hii tunaingia miaka 62 toka tupate uhuru. Kwa sasa tunao Watanzania wengi wenye elimu, ujuzi, uzoefu na maarifa ya namna ya kusimamia viwanda vilivyoko na vitakavyojengwa nchini. Kwa mantiki hiyo, ni wakati muafaka kuchukua hatua ya kuwatumia wataalam wetu wazawa na rasilimali zetu kusaidia kwenye kuwekeza na viwanda vipya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa, sasa ni wakati muafaka wa kutafakari na kufanya maamuzi ya kuliwezesha Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* ili kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya kuendeleza na kusimamia uwekezaji wa viwanda hapa Tanzania kwa kutumia wataalam wetu wazawa. Hii inawezekana ikiwa watapatiwa rasilimali pesa ya kutosha na wataalam watakaohitajika kwani katika uongozi wa awamu ya kwanza, *NDC* iliendesha shughuli zake kwa mafanikio makubwa. Shirika la *NDC* inatekeleza miradi inayogusa sekta zote muhimu kama kilimo, madini, afya, viwanda, nishati na biashara. Baadhi ya miradi hiyo ni Kiwanda cha Viuadudu Kibaha, Migodi ya Makaa ya Mawe Mchuchuma, Mradi wa Chuma cha Pua, Liganga, Mradi wa Magadi Soda, Monduli, Arusha.

Vilevile *NDC* inasimamia Bandari Kavu ya Nafaka, *ETC Cargo,* Dar es Salaam na mashamba ya zao la mpira yaliyopo Tanga na Morogoro. Pia *NDC* inamiliki kiwanda cha kuzalisha vipuli vya mashine na mitambo mbalimbali kilichopo mkoani Kilimanjaro cha *KMTC*. Kwa mantiki hii, *NDC* wanatekeleza majukumu makubwa sana kwenye sekta ya viwanda na uwepo wao ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TIRDO* liliundwa ili kufanya utafiti na kutoa huduma za kitaalam ili kuendeleza viwanda nchini. Shirika hili ni muhimu sana kwani miundo na ujenzi wa viwanda umebadilika sana kutokana na kuwepo kwa teknolojia mpya sehemu nyingi duniani.

Mheshimiwa Spika, hapa Tanzania viwanda vingi vilivyojengwa miaka ya nyuma vimefungwa kutokana na sababu mbalimbali. Kutokana na ukweli huu, huduma ya utafiti ya *TIRDO* inahitajika ili kutoa ushauri elekezi wa ni nini kifanyike kufufua viwanda hivi.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu la Moshi Vijijini, moja ya kiwanda kilichokuwa kimepata mafanikio makubwa sana ni kile kiwanda cha kukoboa mpunga cha *Kilimanjaro Paddy Hulling Co. Ltd* kilichopo Chekereni – Moshi katika Kata ya Mabogini.

Mheshimiwa Spika, kiwanda hiki kilikuwa kimejengwa kwenye eneo ambalo linazalisha mpunga mara mbili hadi tatu kwa mwaka. Kiwanda hiki hakifanyi kazi tangu Septemba. 2014. Kiwanda cha kukoboa mpunga kilikodishwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahawa *(KNCU)* na baada ya kushindwa kukiendesha, mkoa ulimshauri Msajili wa Hazina kukirudisha Serikalini ili atafutwe mwekezaji mwingine anayeweza kukiendesha. Tayari Msajili wa Hazina amerejesha kiwanda hiki Serikalini tangu tarehe 18 Oktoba, 2018 lakini bado hajapatikana mwekezaji na shughuli zimelala. Kutokuwepo kwa kiwanda hiki

kumeondoa fursa ya wakulima kupata bei nzuri ya mpunga na ajira kiwandani kwa wana Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha pili kilichopo jimboni kwangu na hakifanyi vizuri ni kiwanda cha bidhaa za ngozi Msuni kilichopo Kata ya Uru Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, kiwanda hiki kinamilikiwa na Kamati ya Maendeleo Kata ya Uru Kaskazini *(WDC)*. Kina uwezo wa kuzalisha bidhaa mbalimbali za ngozi kama viatu, mikoba na mikanda.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoomba katika bajeti ya mwaka juzi na mwaka jana, narudia tena kuiomba Serikali itume wataalam wa *TiRDO* kwenye kiwanda hiki ili ushauri wa kitaalamu upatikane na kiwanda hiki kifufuliwe na kuunga juhudi za wana ushirika huu kwenye kukuza uchumi wao na wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, jimbo la Moshi Vijijini ni maarufu sana katika uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo. Kama Serikali itakuwa na mikakati ya kuhamasisha uwekezajj wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kuzindika mazao ya kilimo na mifugo, hii itasaidia kutengeneza ajira na kuongeza kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

Kwanza, Serikali ichukue hatua haraka na kuliwezesha Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* ili litekeleza kikamilifu majukumu yake ya kuendeleza na kusimamia uwekezaji wa viwanda hapa Tanzania. Hii itawezekana ikiwa wataongezewa raslimali pesa na wataalamu wa kutosha.

Pili, kwa kuwa huduma ya *TiRDO* inahitajika sana kwenye kutoa ushauri elekezi wa ujenzi wa viwanda nchini, ninaishauri

Serikali itenge fedha za kutosha na kupeleka wataalam wa kutosha kwenye fani zote ili kuliwezesha shirika hili kutekeleza majukumu yake.

Tatu, Wizara itafute mwekezaji katika kiwanda cha kukoboa mpunga cha *Kilimanjaro Paddy Hulling Co. Ltd* kilichopo Chekereni - Moshi, katika Kata ya Mabogini. Kiwanda hiki kinaweza kuwa ni chanzo cha kusafirisha nje mchele ulioongezwa thamani na kuwapatia wakulima kipato na Taifa kwa ujumla.

Nne, Vyama vya Ushirika vilivyopo Jimbo la Moshi Vijijini vihimizwe na kuhamasishwa kuwa na viwanda vya kuchakata mazao mbalimbali ya kilimo na mifugo na kuyaongezea thamani ili kuzalisha bidhaa zinazotokana na kahawa, ndizi, mboga mboga, nafaka, mikunde, maziwa, asali, alizeti na mengine mengi. *SIDO* na *TEMDO* wanaweza kusaidia sana kwenye hili.

Mheshimiwa Spika, tano, kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka juzi na mwaka jana, bado naliomba tena Shirika la Utafiti wa Viwanda Tanzania *(TiRDO)* lishiriki kikamilifu kwenye kutoa ushauri wa kitaalam kukifufua Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Msuni kilichopo Kata ya Uru Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Mheshimiwa Exaud Kigahe ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nami niungane na wenzangu katika kuwapongeza sana Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kufanya kazi nzuri sana, sana, sana ambazo

zimekuwa *reflected* kwenye takwimu na taarifa mbali mbali. Vile vile nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hali na azma yake kubwa ya kutamani kuona Tanzania ikikua kiuchumi kwa kubadilisha sheria mbalimbali na pia kubadilisha mifumo na kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya uwekezaji ndani ya nchi yetu. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza pia hasa kwa kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara miradi ambayo imesajiliwa kwa kipindi hiki tu kifupi; ukiangalia mwezi Julai, 2022 mpaka Machi, ni zaidi ya miradi 240, ambayo thamani yake ni Dola za Kimarekani milioni 438 na hii imesaidia sana katika kukuza uchumi. Sambamba na hilo, kumekuwa na ongezeko la ajira watu zaidi ya 39,245 ambao wamenufaika na ajira katika usajili wa miradi hiyo mipya.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Mheshimiwa Rais pia ameweka mikakati mbalimbali ya kukuza ajira. Moja ya mikakati ni hili la kuweza kukuza viwanda hasa katika suala la kwenye sekta ya uwekezaji. Tumebadilisha sheria, na pia tumerahisisha mazingira ya uwekezaji nchini kuweza kuwa rahisi zaidi ili uwekezaji ukue na kuweza kupata kipato. Nchi nyingi duniani leo zimetoka kwenye masuala ya kufanya biashara kwa maana ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa imekuwa inatengeneza mazingira wezeshi na kukusanya kodi. Vile vile sehemu kubwa ya biashara, mfano ajira zinatokana zaidi na *private sector* ambayo sasa hivi Mheshimiwa Rais ameamua kui-*enhance* kwa sehemu kubwa sana, tunaona kwenye kilimo mapinduzi makubwa; kwenye uwekezaji tunaona mapinduzi makubwa; na kwenye viwanda tunaona uwekezaji mkubwa ambao unafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika upande wa ajira, tunaweza kuona kwa upande wa ajira za kisekta ni maagizo ya Mheshimiwa Rais na maelekezo mahususi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Wizara zote za kisekta lazima kwenye mwaka wa fedha unazopewa bajeti, zizalishe ajira ili Watanzania waweze kunufaika na ajira hizo katika ngazi mbalimbali. Hilo limekuwa likitekelezwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika miradi tu ya Wizara za maendeleo, zaidi ya Watanzania 1,226,925 walipata ajira. Sasa kwa muktadha huo huo wa *spirit* ya Mheshimiwa Rais ya kutaka kuongeza ajira, kukuza uchumi na kutengeneza uchumi jumuishi ili kila mwananchi aweze kunufaika, ni pamoja na kutengeneza mazingira ya kuwasaidia wawekezaji, na pia kusaidia kwenye sekta ya uchumi ya biashara ili iweze kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nimesikia hili suala la Tanga ambalo limesemwa sana na Waheshimiwa Wabunge hapa. Nimelazima kufuatilia kwa sababu limegusa hasa kwenye sekta na Wizara yetu ya kwenye masuala ya ajira. Ni kweli nimefanya utafiti na nimeangalia kwenye rekodi mbalimbali zilizofanywa ikiwa ni pamoja na hesabu za kihasabu zilizofanywa kwenye Kampuni ya *Tanga Cement,* inathibisha kwamba *Tanga Cement* haina uwezo tena wa kujiendesha, ina-*run* kwa hasara. Zaidi ya hapo, hata fedha zile ambazo inazipata kidogo katika *operation*, inajikuta inashindwa kulipa kodi; na kwenye eneo la kodi lazima uangalie kama ni faida. Unaangalia faida ghafi ambayo ni jumla ya *gross profit,* na pia utaangalia *net profit* baada ya *operational cost*. Pia utaangalia gharama nyingine ambazo utazipata kama unapata faida baada ya kulipa kodi, na vile vile utaangalia kabla ya kulipa kodi na baada ya kulipa kodi. Hizi zote zinathibitisha kampuni hiyo haina uwezo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, katika maamuzi ambayo yalifanyika, *FCC* katika malalamiko yaliyopelekwa tarehe 2 Novemba, 2021 *FCC* iliamua kwa misingi miwili ambayo imeainishwa kwenye

Sheria Ushindani ambapo katika Kifungu chake cha 5 (6) (a) na (b) kinatoa masharti kwamba kampuni haipaswi kuwa na nguvu kubwa kwenye soko, lakini pia (yenyewe peke yake) isiwe na uwezo ambao unaweza kuathiri watu wengine kufanya biashara. Katika tafsiri ambazo zilitumika *FCC,* waliweza kuzingatia matakwa pia ya Sera ya Taifa na pia mwendendo na mtazamo wa Serikali ya Awamu ya Sita, na pia katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi inayotaka kukuza uchumi wa Taifa, uchumi wa Watanzania na mtu mmoja mmoja na pia kukuza uchumi jumuishi na kutengeneza fursa za ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipengele kilichotumika waliangalia muktadha huo na kuona kwamba katika kipengele cha 5 (a) kinachohitaji nguvu ya soko, ambayo kwa lugha ya kigeni inasema ni *sales volume* ambayo inahitaji isizidi asilimia 35, ndicho kigezo pekee ambacho kilionekana. Sheria hii katika kipengele cha pili inahitaji pia huyo mtu ili aweze kuonekana ana *dominance* kwenye soko, ni lazima awe amekidhi vigezo vyote katika kifungu cha 5 hicho, kipengele (a) na (b).

Mheshimiwa Spika, tafsiri iliyofanyika katika *Fair Competitions Tribunal,* wao walijikita zaidi kwenye kigezo kimoja tu cha *installed capacity* ambapo waliangalia katika kipengele cha asilimia 35 bila kuangalia kwamba sheria inataka vyote kwa pamoja vitamkwe kama jinsi sheria inavyosema katika kifungu hicho. Kwa hiyo, wakafanya maamuzi ya ku-*crash decision* ile na kusema kwamba maamuzi ya *FCC* yaondolewe na muunganiko huo usiwepo.

Mheshimiwa Spika, sheria hiyo hiyo pia katika kifungu chake cha pili inaitaka mamlaka katika kutafsiri sheria; haitafsiri katika mazingira yale, na ni *principle* ambayo hata kwenye sheria ipo, ya kusema kwamba *every case should be judged from its own circumstances,* kwamba kila kesi lazima iangaliwe na kutafsiriwa kwa mazingira yake kama jinsi ilivyo. Katika msingi huo huo, hata

kwenye Sheria za Kiuchumi pia maamuzi yanaangaliwa kutokana na jinsi ambavyo hali ya kiuchumi, na mazingira yaliyokuwepo kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2020, maamuzi yaliyofanywa na *FTC (Fair Competition Tribunal),* wao walifanya uamuzi kwa ku-*base* zaidi na tafiti ambazo zilifanyika katika kipindi cha mwaka 2020. Hali ya sasa hata ukiiangalia, mwaka 2020 aliyekuwa anaongoza kama kiwanda kwenye kupata mengi na uzalishaji ilikuwa ni *Twiga Cement* anafuatiwa na *Tanga Cement* na Dangote. Kwa hali ya 2022 kwa tafiti zilizokuja kufanyika na takwimu kwa mujibu wa *data* ambazo zipo, inasema anayengoza kwa sasa, siyo kama ilivyokuwa 2020 tena, takwimu zinaonesha sasa *Twiga Cement* ndiyo anaongoza, anafuata Dangote na kuna kiwanda kingine ambacho hakikikuwepo kabisa kwenye soko, wakati huo kilikuwa hakizalishi, kilikuwa kinaanza, lakini sasa kinazalisha zaidi ya tani 900,000, ambacho ni Kiwanda cha Shuwan Maweni na kiwanda kingine ambacho kinafuata sasa ndiyo Tanga ambacho bado pia kinashuka katika uzalishaji, ambacho ndiyo maana ya maombi haya kuweza kufanya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji huyu amekuwa anazalisha na anafanya kazi ya kuzalisha *cement* za Twiga lakini pia anaenda kuingiza *capital,* ku-*inject new capital* ya zaidi ya Shilingi trilioni moja ili kuongeza *capacity*. Katika maamuzi yaliyotolewa awali ya *FCC,* yalikuwa na masharti. Masharti hayo yalikuwa kumi, kati ya masharti matatu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja nimalizie.

**SPIKA:** Utakuwa unachukua muda wa Waziri hapo. Malizia dakika moja.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, katika masharti hayo yaliweza kukubaliwa pia na hao wadau wa maendeleo. Zaidi nimalizie tu kwa kusema kwamba, hili jambo siyo jipya. Ipo kesi ya Afrika Kusini ya mwaka 2019 na imefanyiwa maamuzi, ambapo kesi hiyo ilikuwa hivyo hivyo kwamba walirudi tena katika kufanya *review* baada ya maamuzi ya awali. Kwa hiyo, hakuna suala la kudharau Mahakama au maamuzi hapa. Suala lipo, linatoa haki. Sheria hiyo ni kwamba unaweza ukarudi tena kupeleka maombi kulingana na hali iliyopo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kuna kesi nyingine pia ya Toyota na *Sifao Motors,* ambayo nayo pia ilifanyiwa maamuzi hivyo hivyo na *FCC* ikakataa ombi lao, lakini pia ilivyokuja kurudi *FCT,* nayo pia ilikuja ikabariki maamuzi yaliyofanywa na *FCC*. Kwa hiyo, jambo hili siyo geni, tunachelewesha uwekezaji, tunachelewesha Watanzania kuweza kupata uchumi, tutaenda kupata hasara ya kupoteza ajira 3,000 za Watanzania, tutaenda kupata hasara za uwekezaji wa kukosa zaidi ya Shilingi trilioni moja kama maamuzi haya tutaenda kuyafanya kishabiki na bila kuangalia maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono kwamba suala hili la uwekezaji ni muhimu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba, atafuatiwa na Mheshimiwa Exaud Kigahe, mtoa hoja, ajiandae.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia. Nianze

kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika eneo hili la uwekezaji pamoja na viwanda. Nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kazi kubwa anayofanya ya kutekeleza maono ya Mheshimiwa Rais katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, mtaweza kuona kwamba uwekezaji ambao umeishaingia ndani ya nchi yetu, pia na *performance* za viwanda ambapo sisi ni wadau wakubwa sana kwenye masuala ya *performance* za viwanda na uwekezaji katika eneo la kupata kodi pamoja na kukuza *GDP,* tunaiona wazi wazi. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia nianzie kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na kukiri kwamba hoja zile ambazo wamezileta zinazo angukia upande wa Wizara yetu tumezipokea na tutazifanyia kazi na bahati nzuri sana wametoa maoni haya katika kipindi ambacho tunaendelea kukamilisha nyaraka ambazo tutazileta kwa ajili ya mjadala mpana wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali lakini pia na katika *Finance Bill* ambayo itajadiliwa mara tu baada ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nikianza na yale masuala ambayo wameyaongea ya kikodi nitaomba uridhie na Waheshimiwa Wabunge niwaombe waridhie nisipitie kamoja kamoja kwa sababu ndiyo tunaendelea kukamilisha waraka huo. Tumepokea maoni yenu na niwaahidi kwamba tutakuja na hatua za kikodi ambazo ni rafiki kwa sekta binafsi kwa sababu huo ndiyo muelekeo wa nchi yetu na ndiyo muelekeo wa Mheshimiwa Rais kwa kutengeneza sheria za kodi ambazo ni rafiki kwa sekta binafsi na ni rafiki kwa uwekezaji, rafiki kwa mazingira ya biashara ili kuweza kutengeneza ajira na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja pamoja na uchumi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liliongelewa kwa sauti kubwa suala la Kariakoo na lenyewe tumelizingatia tumepokea na yenyewe tutakapo kuja kwenye mjadala tutakuwa tumezingatia maoni yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye masuala mahususi yaliyoongelewa, jambo moja ambalo limeongelewa lilikuwa la *ETS* yale masuala ya *Electronic Tax Stamp.*

Mheshimiwa Spika, jambo hili utakumbuka lina maelekezo ya Bunge katika kipindi kilichopita mwaka mmoja ama miwili Bunge lilielekeza Waheshimiwa wabunge kwa kauli moja walielekeza kwamba Serikali iangalie upya jambo hili kwa sababu bei zinazotolewa na mtoa huduma ni kubwa. Serikali ilichukua hatua kwa kutangaza hili jambo hili lifate taratibu za *International Tendering* ili kuweza kualika wadau wengi wanaofanya kazi hiyo tukiwa tunashirikiana na sekta binafsi kuweza kupata mdau ambaye ataweza kutoa huduma hiyo kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, mchakato uliendelea na wakati mchakato unaendela, nilisikia kauli moja anasema mbona akapewa sasa yule aliyekuwepo. Kwa sababu utaratibu wake unachukua takribani miezi sita na kuendelea, tuliona lazima utaratibu wa makusanyo uendelee katika kipindi hicho cha mpito ambacho ni cha mwaka mmoja, kwa hiyo utaratibu umeenda mpaka mwisho na nitawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa umahsusi wa jambo hili katika hatua fulani hivi waridhie kwamba tutalielezea kwa kina katika ngazi ya kamati na kamati inawakilisha Bunge lakini wapokee maelezo haya ninayoyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipofikia katika hatua ya kufanya uchambuzi. Uchambuzi ukafanyika mpaka mwisho na timu iliyokuwa inafanya uchambuzi ilikuwa imekusanya wazoefu wa utaratibu hizi za kimanunuzi kutoka taasisi zetu zote muhimu

tunazozifahamu zote za vyombo pamoja na zile ambazo ni za kimanunuzi.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho wa siku taarifa ile ya mwisho ilionesha kwamba bei zilizokuja hazitofautiani sana na zile zilizokuwepo na wahusika ambao wameenda kwenye hatua hizo wanaeleka kwenye utaratibu ule ambao bei ziko zile zile ambazo zilikuwa zimeamsha hisia hizi za wabunge na kuleta hoja ya kutaka tupate mtoa huduma mpya.

Mheshimiwa Spika, sasa ilivyofika mpaka mwisho pale sifa zile zilizokuwa zinatakiwa zilionekana hazijafuzu kwa sababu kile kilichokuwa kinatafutwa kuanzia maoni ambayo yalitolewa na wabunge ya bei hayakuwa yametimia. Kwa hiyo, kile ambacho kilikuwa kimefikia kwa hatua hii ilikuwa ni mchakato ule ufanyike upya na mchakato wenyewe unafanyika kwa hatua zote ikiwepo ya *Window Shopping*, ikiwepo ya *National Shopping,* kwa hiyo timu mbalimbali zimeenda katika maeneo ambako wananweza wakapata teknolojia mpya, teknolojia rafiki, teknolojia ambayo ina gharama nafuu lakini pia ikizingatia uwezekano wa kuihamishia teknolojia hiyo katika mamlaka zetu za usimamizi ili hitimisho wa siku jambo hili liweze kufanywa na watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ombi langu kwa waheshimiwa wabunge, kama kuna Mbunge ambaye ana mtu ama kampuni, ama taasisi ama teknolojia ama anajua mahali ambako teknolojia tunaweza tukaipata ambayo inaweza ikatoa huduma hiyo hata kwa nusu ya ile ambayo ipo, nimkaribishe aje ofisini aonane na mamlaka yetu inayosimamia jambo hilo Mamlaka ya Mapato Tanzania, halafu aweze kuunganisha timu ile inayofanya hiyo *shopping* pamoja na hiyo taasisi ambayo inaweza ikatoa huduma hiyo ili tuweze kukamilisha mchakato huo kwa ufanisi na tuweze kupata kile ambacho sekta binafsi yetu itanufaika na

watanzania watanufaika lakini na Serikali iweze kupata kodi katika gharama ambazo zinahilimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hilo liko hatua hiyo na tunaamini si muda mrefu sana tutaenda kwenye hatua ya mwisho na tutaendelea kulitolea taarifa jambo hili katika Kamati ya Bunge pamoja na Bunge lenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikihamia katika hoja ya pili ambayo ni mahsusi ni jambo lile la kiwanda cha Twiga, jambo hili ni jambo nyeti sana. Moja, sisi kama Serikali tuna *interest* kubwa sana kwenye jambo hilo kwa sababu kati ya wale wawekezaji kwenye kiwanda hiki ambacho tunakiongelea asilimia takribani sitini na nane ni hawa ndugu zetu wa *AfriSam* lakini asilimia zinazosalia mnajua kwamba upo mkono wa Serikali kupitia mifuko yetu ya hifadhi ya jamii ambalo ni jambo nyeti sana kwetu sisi kama Serikali. Kwa maana hiyo niwahakikishie Wabunge Serikali inapeleka macho yake yote mawili kuhakikisha kwamba jambo hili halifi bali linaendelea na hiyo ndiyo ambayo imekuwa *concern* ya wabunge kwamba labda kiwanda hiki kinaweza ikafanyika janja janja kwamba kikanunuliwa halafu kikafungwa. Hakiwezi kufungwa kwa sababu kimebeba maslahi ya nchi, kimebeba maslahi ya Serikali na kimebeba maslahi ya watanzania, hakiwezi kikafungwa. Mbali na habari ya ajira lakini ile tu yenyewe kwamba kwenye umiliki tuna taasisi zetu ambazo zina mkono mle hatuwezi tukaruhusu kikafa na hatuwezi tukaruhusu wale watakaofanya *merging* wakakipeleka kwenye kufa hilo halitatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili tukiacha utaratibu ukaendela hivi ilivyo sasa mwisho wa siku Serikali itaenda kubeba mzigo ule wote kwa sababu nimewatajia aina ya wamiliki walioko mle. Kiwanda hiki kikifa maana yake wale watu hawawezi wakapata hiyo hasara hii hasara itahamishiwa Serikalini. Kwa maana hiyo kwa hali waliyonayo ya sasa hivi kwa takribani *cash*

*flow* zao ziko *negative* zaidi ya bilioni kumi na moja, hivi tunavyo ongea hawawezi wakastahimili kuendelea wao wenyewe tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye upande wa madeni wana deni kubwa ambalo linazidi bilioni mia mbili na tatu. Mnaweza mkaona kwamba hata wa kuwafufua tu anatakiwa awe na *muscle* kwelikweli. Wana 203 deni na wana *overdraft* ya zaidi ya bilioni 19 wanapumulia mashine hao walipo hapo wanahitaji wa kuwainua mwenyewe awe *very strong*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa taratibu hizo zimeshafanyika zimeenda hatua nyingi. Mheshimiwa Naibu Waziri ameshaelezea vizuri masuala ya kisheria mimi naomba Waheshimiwa Wabunge muiamini kamati yenu Serikali tutaenda kuelezea kwa kina na niwaombe tusije tukalipazia sauti sana hili jambo, kwa sababu ukiondoa uwekezaji huu peke yake masuala ya kiuwekezaji ni *very sensitive*. Hizi *back and forth* tunaweza tukashughulika na mwekezaji mmoja lakini tukakimbiza wengine 50 kwa sababu tu ya *back and forth* ambazo tunazifanya.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukaenda kwenye hatua kama nchi tukaendelea kupunguza yale ambayo kwenye *rating* tunakuwa *rated* chini kwa kuchelewesha uwekezaji na kuwa na milolongo mingi ambayo ina mikono mingi kwenye taratibu ambazo zinahitaji jambo liishe halafu tuweze kuendelea na uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema na nimeshaona kengele ya pili imeshagongwa niwaombe Waheshimiwa Wabunge waiamini Serikali, lakini pia waiamini Wizara, lakini pia waiamini Kamati. Tutaenda kutoa maelezo ya kina Kamati ya Bajeti na tutatoa maelezo ya kina kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara kwa niaba ya Bunge zima ili tuweze kuelewana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa wabunge kabla hajachangia Mheshimiwa Kigahe ambaye nilikuwa nimeshamtaja wako wageni ambao wako humu Bungeni hawakupata nafasi ya kutangazwa asubuhi.

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Abbas Tarimba ambao ni viongozi wa matawi matatu ya Kampuni ya Samaki Samaki na Kuku Kuku za Jijini Dar es salaam wanaoendesha migahawa hiyo ya Samaki Samaki na Kuku Kuku na hawa ni Ndugu Paul Namuhisa ambaye ni kiongozi wa msafara, yupo pia Ndugu Carlos Mella Mwenyekiti wa *Kalitos Group of Companies,* yupo pia Ndugu Twaha Yassin Meneja wa Samaki Samaki, yupo pia Ndugu Deo Mrina Mkurugenzi Mtendaji wa Halisia *Real Estates,* karibu sana. *(Makofi)*

Voingozi hawa wameambatana na wachezaji 25 wa timu ya mpira wa miguu ya Kampuni za Samaki Samaki na Kuku Kuku ya jijini Dar es salaam na kesho kutakuwa na mchezo kati ya Bunge *Sports Club* na wachezaji hawa wa timu ya mpira kutoka Samaki Samaki na Kuku Kuku, majira ya saa 09:00 Jamhuri *Stadium* kwa hiyo tukutane huko.

Waheshimiwa wabunge wapo wageni 42 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni wanachama wa *UDOM Health Club* kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Paschal Lucas, karibuni sana. Wapo pia wageni 68 wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo vijijini wanaotokea Mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na Ndugu Gerald Swai, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wawili wa Mheshimiwa Nashon Bidyanguze ambao ni wapiga kura wake kutoka Mkoa wa

Kigoma Ndugu Noela Shalubobo na Abed Abed, karibuni sana. Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wananfunzi 125 na waalimu 12 kutoka *BSL Daycare Center* na *BSL Open School* ya jijini Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Peter Frank, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nilishamtaja Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara Mheshimiwa Exaud Kigahe, mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu ya Mheshimiwa Waziri wa uwekezaji viwanda na biashara. Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema ambaye ametujaalia kukutana siku hii ya leo tukiwa na afya njema kuhakikisha tunapitisha Bajeti hii muhimu ya Wizara ya uwekezaji viwanda na biashara.

Mheshimiwa Spika, pili nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini, niendelee kutumikia nchi hii katika nafasi ya Naibu Waziri katika Wizara ya uwekezaji viwanda na biashara.

Mheshimiwa Spika, tatu nishukuru sana viongozi wetu Wakuu, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu lakini pia nikushukuru sana na wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika lakini na Wenyeviti wa Bunge hili lako tukufu kwa kuendelea kusimamia na kuhakikisha tunatekeleza na majukumu yetu vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Waziri wangu Dkt. Ashatu Kijaji Kwa kuendela kunisimamia vizuri na kunielekeza katika kutimiza wajibu wangu. Naanza kushukuru sana Kamati ya Kudumu ya Viwanda, Biashara Kilimo na Mifugo kwa namna

pekee mwenyekiti wetu Mheshimiwa Kihenzile lakini pia na Makamu na wajumbe wote. Pia kwa namna ya pekee niwashukuru sana wajumbe wa kamati lakini pia na waheshimiwa wote Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendela kushirikiana nasi katika sekta hii ya uwekezaji, viwanda na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri imebeba dhamana kuu ya kuendeleza kasi ya uwekezji na ujenzi shirikishi na unganishi wa uchumi wa viwanda kwa kutambua nafasi ya sekta binafsi kama injini ya ujenzi wa viwanda na shughuli za ubia kwa sekta binafsi na umma na hii dhahiri kuwa mfumo huu na maboresho mengine yanayoendelea katika nchi hii ikiwemo utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara Mkumbi au *blue print* unalenga kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea hali ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na kuleta maendeleo endelevu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa na mimi nichangie hoja kwa kutoa maelekezo au ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilizowasilishwa kuhusiana na Bajeti ya uwekezaji, viwanda na biashara kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara Kilimo na Mifugo imetoa maoni mengi na maelekezo katika maeneo kadhaa na ambayo kimsingi mengine yameshatekelezwa na yanaendelea kutekelezwa ikiwa ni matokeo ya kazi kubwa ya kamati hii kutuwezesha sisi kama wizara kutekeleza majukumu hayo. Mosi, ni kuhakikisha tunalipa fidia ya eneo lile la mradi huu mkubwa ambao umeongelewa na wabunge wengi Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Serikali ya Awamu ya Sita Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa upenzi mkubwa kuhakikisha sasa anaweka historia kama ambavyo Wabunge wamesema

kwamba sasa tunaweza kutekeleza mradi huu ametoa hizo fedha bilioni 15.4 ambazo zinaenda kulipa fidia ya wananchi wale ambao sasa ni hatua ya awali ya kutekeleza mradi ule mkubwa katika mkoa wa Njombe katika Halmashauri ya Ludewa. Ambapo tunaamini katika zoezi hili la kulipa fidia, mosi ni kitu kikubwa uchumi wa nchi hasa wana Ludewa, lakini pili tutatoa elimu ili fedha hizo malipo haya yanayolipwa yawe na faida yawe na manufaa ili wananchi wale waweze kutumia vyema na siyo baada ya hapo warudi tena kwenye umasikini kama ambavyo baadhi ya wabunge walisema katika maeneo mengine fidia hizi zikilipwa wananchi wale wanatumia fedha vibaya halafu wanarudi kwenye hali ngumu na kuwa masikini zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa spika, pili kulikuwa na suala la kiwanda la viuwa dudu. Tunajua changamoto kubwa ilikuwa ni kuona namna gani kiwanda kile kinaendela kuzalisha kadri ambavyo kilipangwa na sisi kama Serikali tumeishakubaliana kupitia Wizara ya Afya lakini na wenzetu TAMISEMI kuhakikisha lile soko la awali ambalo ni sisi watanzania kutumia dawa zile zinatumika na katika mwaka huu wa fedha tunaenda kutekeleza hayo lakini zaidi tunatafuta masoko ya nje, zaidi na haya yameshaanza na tumeanza kuuza katika badhi ya nchi dawa hizi katika nchi za majirani kwa upande wa *SADC* na *EAC* na tunaamini kiwanda hiki kwa mwendo huu wa mauzo sasa na utaratibu unaokwenda kwa kuzalisha viuwa wadudu lakini viwatilifu na amini kwa kuwa sasa fedha zimeanza kupelekwa katika kiwanda hiki na uzalishaji umeanza na kwa historia ya kwanza walikuwa wanapewa fedha na Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi kuanzia mwaka huu wa fedha wameanza kujilipa wao kutokana na mapato ndani ya kiwanda hicho, kwa hiyo tunaamini huko tunakokwenda tukikamilisha haya tutaweza kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini kulikuwa na hoja ambazo Kamati ya Kudumu ilielekeza kuhusiana na eneo la Engaruka nalo hili tunalifanyia kazi na kutakuwa na fidia kwa wananchi zaidi ya 599 ambao tukisha kamilisha uhakiki kama ambavyo tumeanza kwenye Mchuchuma na Liganga na huku pia tutaenda kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile kulikuwa na hoja ya nini tunafanya kuhakikisha Shirika letu la Maendeleo la Taifa *NDC* wanaendelea kutimiza wajibu wao au uwepo wao. Nitoe taarifa kwamba Shirika letu la Maendeleo ya Taifa *NDC* kwa sasa lina jumla ya miradi 13 ambayo moja ni hili la Mchuchuma na Liganga lakini kuna Mradi wa Engaruka Soda *ash* au Magadi ya soda lakini Maradi wa Makaa ya Mawe Ngaka ambako ndiyo kuna ile Kampuni ya *Tancol* Mheshimiwa Kapinga amesema.

Mheshimiwa Spika, pia tuna Mradi wa Chuma Ghafi cha Maganga Matitu lakini tuna kongane za viwanda lakini zaidi pale *TAMCO,* Nyanza *Grass,* Kange na *KMTC* lakini pia tuna Kiwanda cha Kilimanjaro *Machine Tools* pale kwa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, tuna Kiwanda cha Mang'ula *Mechanical Machine Tools* ambacho hiki kilikuwa mboni ya viwanda vile ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa amavyo tumevirudisha Serikalini kikasimamiwa na Shirika letu la Maendeleo ya Taifa *NDC* lakini pia tuna Mradi wa Bandari Kavu ambao unaendelea lakini pia Kiwanda hiki cha Viua dudu pale Kibaha na Mradi wa Umeme wa *Solar* Singida, Mradi wa Upepo Singida lakini pia tuna Mashamba ya Kihui na Kalunga ambayo ni Mashamba ya Mpira.

Mheshimiwa Spika, katika miradi hiyo 13 miradi ambayo inaenda vyema kwa sasa au tunatekeleza kwa hatua ya awali ni mitano ambayo inafanya kazi ikiwemo ni kongane za viwanda pale *TAMCO* Nyanza *grass* kiwanda cha *Machine Tools* Mradi wa Bandari Kavu lakini pia Kiwanda cha Viua dudu na Mashamba ya

Mpira ya Kiuwi Muheza Mkoa wa Tanga lakini pia Kalunga Kilombero Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kuanzisha Kituo cha Ugavi wa Biashara cha Kurasini au Kurasini *Logistical Centre*. Ni kweli mradi huu ulikuwa utekelezwe chini ya Wizara lakini ninyi ni mashahidi kutokana na msongamano mkubwa pale bandarini, kwa hiyo, kulikuwa na maelekezo maalum kwamba sasa lile eneo liweze kutumika katika upanuzi wa huduma ya bandari pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, lakini mradi ule bado unaendelea na dhamana ya kuendeleza mradi ule ni kuhakikisha kituo hicho cha bishara ya ugavi kinafanya kazi chini ya mamlaka yetu ya *EPZ*. Na dhamira hiyo bado ipo kwa sababu, tulikuwa na changamoto na sasa bado tunayo changamoto ya masoko ya mazao ya kilimo ikiwemo chai.

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu hiyo, mradi huu mpango wake ni kuhakikisha tunatumia eneo lile la Bandari Kavu la Kwala, ambapo kule sasa kutakuwa pamoja na viwanda vingine, lakini pia kutakuwa na hii *agro-processing* na mambo mengine ambayo yatatekelezwa katika eneo lile la Kwala. Kwa hiyo ule mradi haujafa, lakini tumehamisha eneo kwa sababu ya umuhimu wa Bandari yetu pale Dar-es-Salaam ili iweze kufanya kazi vizuri kupunguza msongamano ambao nao ni changamoto kubwa katika kuhakikisha uchumi wa nchi hii unasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya lumbesa. Nitoe taarifa, kulingana na kanuni na sheria kwa kutumia Sheria ya Vipimo Sahihi na Kanuni za Ununuzi na Uuzaji wa Mazao, *The Weight and Measures Act,* tunataka vifungashio visizidi *kilogram* 100 pamoja na kiasi cha uhimilivu asilimia kama tano. Na kwa mujibu huo kwa hiyo maana yake tafsiri sahihi ya ufungashaji ni

kwamba tusifungashe tofauti na vifungashio ambavyo vimewekwa, iwe ni kilo 100 au ni chini ya hapo.

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu hiyo, tumesema lumbesa, kwa maana ya kuongeza kilemba au kofia ni marufuku kwa sababu inaleta dhana potofu ya kuwalinda au kuwanyonya wakuluma au wazalishaji wa mazao katika nchi yetu. Kwa hiyo tutahakikisha tunasimamia sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, tumeshakubaliana Wizara yetu, Wizara ya Kilimo na wenzetu TAMISEMI, ambao wao ndio wako kule kwenye masoko, kuhakikisha tunakuwa na *collection centers* au masoko, maeneo ambako kutakuwa na uuzaji wa bidhaa au mazao haya ili kuhakikisha vipimo sasa, ili Wizara yetu kupitia wakala wa vipimo wawe na mizani pale ambayo itawasaidia kupima mazao haya yanayouzwa kwa wakulima au kwa wanunuzi badala ya wanunuzi kwenda mashambani kwa wananchi au wakulima na kuwanyonya. Kwa hiyo, hili ni elekezo; na tumekuwa na *fine* kadhaa kwa wale ambao wanakiuka sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la uhuishaji wa leseni. Kwa mujibu wa Sheria ya Leseni za Biashara, leseni zote za biashara kundi A na B zinatakiwa kuwa hai muda wote. Kwa hiyo, kwa sasa tunahuisha kwa sababu ziko *manually,* tunakokwenda tutaenda kwenda *automation* kwa maana ya kuwa *electronic*. Hiyo itatusaidia kuhakikisha tunafuatilia kwa urahisi zaidi. Tunaamini hata kama kutakuwa na gharama basi itakuwa ni ndogo zaidi kuliko hivi sasa, lakini badaye kadiri maendeleo yanavyoenda tunaamini hii tutaitoa ili kuhakikisha biashara inafanyika vema na kupunguza usumbufu kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la uingizaji wa bidhaa mbalimbali, vikiwemo vyakula hapa nchini, kuhakikisha tunasimamia ubora wa bidhaa hizo. Ikumbukwe kuwa madai ya

uwepo wa mchele wa *plastic* si jipya na lilishakuwepo hata huko nyuma, lakini kupitia taasisi yetu, shirika letu la viwango, tumepitia na kubaini kwamba bado si taarifa sahihi. Lakini tutaendelea kufanya hivyo pamoja na vyakula vingine au bidhaa nyingine ambazo hazina ubora ili viweze kukidhi viwango ambavyo tumejiwekea kama nchi na kuhakikisha wananchi hawadhuriki kutokana na bidhaa ambazo hazina viwango.

Mheshimiwa Spika, kuliongelewa kuhusu masuala ya ubunifu. Nitoe taarifa kwamba, kulingana na mwongozo wa ubunifu ambayo ni Sheria ya *COSTECH,* Sura ya 5, ambao wameanzisha Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia; mfuko huu tayari umesaidia wajasiriamali wengi kupitia *COSTECH,* lakini pia *TIRDO;* na Waheshimiwa Wabunge wengine wamefika pale *TiRDO;* tunawalea vijana hawa. Kuna wengine ambao kwa mfano wabunifu wa mita za maji, hapa Dodoma, Mvumi, lakini pia kuna wengine wazalishaji wa mbolea ambayo inatumika kwenye parachichi na wengine. Tunaamini Serikali inaendelea kuwapa motisha na kuwapa fedha, na wengine wamepata fedha kupitia *Global Fund,* ambao wanajihusisha na utekelezaji wa ubunifu mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi tunaendelea kuwalea wabunifu na tutaendelea kuhakikisha wanapata uwezeshaji zaidi kadiri ambavyo tunaendelea na maboresho haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kulinda viwanda vya ndani. Lazima sisi kama nchi tujielekeze kuhakikisha tunalinda viwanda vya ndani. Na sisi kama Wizara tumeshaanzisha mchakato wa maandalizi ya Sera ya Taifa ya Ushiriki wa Watanzania kwa maana ya *a local contents policy*.

Mheshimiwa Spika, sasa kuliongelewa kuhusu kiwanda cha magari pale…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja, malizia Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa hiyo, tunaenda kuwalinda wazalishaji wa ndani.

Mheshimiwa Spika, lakini nimalizie kidogo kuhusu hoja ya pombe zinazotengenezwa kienyeji. Kama utaruhusu kwa dakika moja niweze kuelezea kidogo nini tunafanya. Kwa mujibu wa viwango vya pombe kali, pombe kali inapaswa kuwa na kiwango cha pombe, *ethanol,* kuanzia asilimia 37 hadi 42 *volume,* ambayo inammanisha kwamba mchanganyiko wa pombe na maji na haipaswi kuwa kiwango kikubwa zaidi ya hapo. Sisi kama Wizara tumeendelea kusaidia wazalishaji wa pombe hawa wa ndani, wa kienyeji, wengi ikiwemo na mimi kule nyumbani kuna pombe ya ulanzi, tayari wameshapata ithibati ya kutengeneza. Pia kuna Kampuni moja ya *Businde Distillers,* Rubisi, kule karagwe, tayari wamepitishwa kupitia Wizara hii kwa kusaidiwa na *TIRDO, TBS* na *SIDO,* ambao wanawasaidia.

Mheshimiwa Spika, tunaamini wajasiriamali wengine kupitia *SIDO* wajiandikishe na sisi tutaendelea kuwasaidia kuhakikisha kwamba nao wanazalisha kwa tija, ili kuondokana na dhana kwamba hatuwalindi wazalishaji wa ndani na hasa kwenye sekta hii ya vinywaji ambayo inachangia pato kubwa sana la Taifa kwa maaba ya kodi katika uchumi wetu wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda na mimi nakushukuru sana kunipa nafasi. Baada ya kusema hayo machache naomba kusema naunga mkono hoja na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wote tuweze kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, ili tuweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa 2023/2024. Naomba kushukuru kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara ili aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii na kwa ridhaa yako nianze kwa aya moja ndani ya kitabu kitukufu cha Mwenyezi Mungu, inayosema, "*Rabbi-rishirahii swadri, wayassirli amri, weahlul-ukudata minlisani yafqahu kauli.*" *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake; nimemuomba Mwenyezi Mungu aunyooshe ulimi wangu ili niweze kuyasema yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameongea kwa dhamira njema kabisa ya kujenga uchumi wa Taifa hili ili niyaseme na yaeleweke, ndio maana ya aya hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru sana wewe kwa uongozi wako madhubuti, lakini pia wasaidizi wako Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Kamati zetu kwa namna ambavyo mmeongoza na kusimamia vyema majadiliano ya bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka 2023/2024.

Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa uchangiaji wenu makini mlioufanya kwa maandishi na kwa kuzungumza moja kwa moja katika Bunge hili Tukufu. Naomba niseme kuwa ninatambua na kuthamini dhamira na nia njema iliyotawala mjadala huu ambayo kimsingi ililenga kuboresha mikakati na mbinu za kisekta zitakazotumika kutekeleza malengo tuliyopanga kwa mwaka 2023/2024 na hivyo kutoa mchango unaotakiwa kwa Taifal letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naishukuru sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa David

Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa namna ambavyo wanajenga hoja na kushauri ipasavyo kuhusu uendelezaji wa sekta ya uwekezaji, viwanda na biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya viongozi wenzangu na watumishi wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na taasisi zake naomba kupokea pongezi nyingi za utendaji zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge hasa kwa Mheshimiwa Rais wetu na kwetu sisi viongozi wa Wizara. Aidha, tunaahidi kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwa ari zaidi. Vilevile tumepokea ushauri na michango mingi ambayo ni chachu na changamoto muhimu katika kuleta maendeleo ya mipango ya uchumi yenye mchango kwa sekta ya uwekezaji, viwanda na biashara.

Mheshimiwa Spika, mawasilisho hayo yanatambua na kuzingatia pia hoja mbalimbali za sekta hii zilizojitokeza wakati wa kujadili na kupitisha bajeti za Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais na Makamu wa Rais na pia Wizara zilizonitangulia kuwasilisha bajeti zao hapa Bungeni kwani Wizara yangu ni Wizara mtambuka ambayo tunashughulika na Wizara zote.

Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa ushauri wenu na maelekezo ya Bunge hili katika kujadili bajeti ya Wizara hii tutayazingatia na kuyafanyia kazi ikiwemo kutoa mrejesho wa utekelezaji wake. Aidha, kutokana na muda mfupi nilionao katika kuhitimisha bajeti hii, maelezo na majibu ya kina ya michango mbalimbali yameandaliwa na yatawasilishwa kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajielekeza katika kujibu na kufafanua hoja mbalimbali zilizojitokeza naomba kuwatambua

Waheshimiwa Wabunge 39 waliochangia katika majadiliano ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Kati yao Waheshimiwa Wabunge 35 wamechangia kwa kuongea hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge wanne wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, na kati yao, naomba uniruhusu niseme hili, kati ya Wabunge hao Wabunge 23 wamechangia kuhusu suala la *Twiga Cement* na *Tanga Cement*. Inaonesha ni kwa kiwango gani ambavyo Waheshimiwa Wabunge wanaguswa na uwekezaji na biashara ndani ya Taifa letu. Kwa shabaha ya kumbukumbu orodha hiyo itawasilishwa na kuwekwa katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu ambao wamechangia hoja hii na kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali akiwemo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Exhaud Kigahe na Mheshimiwa Patrobas Katambi, nawashukuru sana kwa kutoa majibu kwa hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, hoja na mipango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kujadili hotuba yangu inaonesha nia thabiti ya ushirikiano wenu na Wizara hii katika kuziendeleza sekta ya uwekezaji, viwanda na biashara na kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya Taifa letu. Nimehamasika na jinsi mlivyonitia nguvu kwa kukubaliana nami katika mambo ya msingi na kutetea kwa nguvu zenu zote maslahi mapana na yenye maslahi makubwa ya Taifa na wananchi wetu tunaowawakilisha hapa Bungeni. Kwa ujumla wake hoja na michango mingi iliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote waliozungumza na kuchangia kwa maandishi zinashabihiana katika maeneo mengi na zimelenga maeneo

mbalimbali ambayo sasa napenda kujielekeza kujibu na kutoa ufafanuzi wake.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, hoja kubwa ilikuwa ni jambo la *Twiga* na *Tanga Cement,* nami nitajielekeza huko baada ya kuwa nimeongeza mchango kidogo kwenye majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri; nayo ni kuhusu suala la Liganga na Mchuchuma. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge mliotambua kwamba Serikali hii imejipanga kuleta maendeleo kwa wananchi wake, kuwafikia kulekule waliko.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wanakumbuka ni Bunge hilihili mwaka jana lilielekeza fidia hii ikalipwe. Nampongeza sana kwa dhati ya moyo wangu, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, bila kusita ametoa bilioni 15.4 kwa ajili ya malipo ya fidia ya wananchi wetu wote kwenye mradi huu wa Liganga na Mchuchuma. Hii ni dhamira ya dhati sana. Na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge maelekezo yenu kama ilivyosema Kamati yetu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo tunayatekeleza kwa asilimia kubwa. Sasa hivi timu ile ya majadiliano inaendelea na kazi yake ya kujadiliana, kama ambavyo Serikali ilitoa maelezo yake hapa Bungeni; kwamba tunatamani kumalizana na mwekezaji yule wa mwanzo ambaye tayari tulishasainiana mikataba kwa wema na kuondokana naye ili Taifa letu lisiingie kwenye migogoro na gharama nyingine ambazo hazina msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba taarifa yetu tuliyoitoa mwezi wa 11, kwenye Bunge la mwezi wa 11 hapa Bungeni kwamba, tulipata taarifa rasmi kutoka Serikali ya China, mwekezaji yule amefilisika, ni kweli, amefilisika. Pamoja na taarifa ile ya kufilisika ile ni kampuni inayojitegemea, lazima tushughulikenayo kwa kufuata kanuni na

taratibu na sheria zetu, ili kuliepusha Taifa letu kuingia katika migogoro ambayo haina maana.

Mheshimiwa Spika, aliyefilisika ni yeye, lakini bado ana mikataba na sisi; na kama ambavyo Wabunge walitahadharisha huko nyuma wakasema ni wakasema tumuite tuje tuongee naye. Huko nyuma, miaka sita iliyopita, nililieleza Bunge lako Tukufu, tulimuita hakuwahi kutokea na sasa tumemuita amekuja, yupo mezani. Tunajadiliana naye na bahati nzuri na yeye amekiri kweli amefilisika. Amefilisika, lakini bado ana mkataba na sisi lazima tuhitimishe naye vizuri, hicho ndicho ninachokisema. Kazi mliyotutuma tunaendelea kuifanya kwa kiwango cha hali ya juu kwa uharaka, lakini kwa uzalendo mkubwa wa Taifa letu ili sasa mradi huu uanze kutekelezeka, uondoke kwenye miradi ya historia, miradi ambayo ni simulizi ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, nilimsikia Mheshimiwa Neema Mgaya alisema anataka kuleta hoja binafsi. Nilitamani sana kwamba Bunge tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuonesha njia ya kutaka jambo hili liishe sasa na kuwapelekea ujumbe wawekezaji wetu kwamba Tanzania ni salama. Ameweza kuja tumeanza mchakato huu, tumpe nguvu Mheshimiwa Rais wetu ili tulihitimishe jambo hili kwa wakati na tuweze kuona athari chanya ya mradi huu ambao umekuwa ni historia kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ambayo nilitamani niitolee maelezo inaunganishwa na hoja kubwa ambayo ningetamani nichukue muda wangu mwingi kuieleza. Nayo ni kufutwa, kuondolewa kwenye usajili kwa Kampuni ya *Chalinze Cement Company Limited.* Kwa nini imeondolewa? Ni jukumu letu kuzisajili, ni jukumu letu kuwawekea masharti, ili watekeleze.

Mheshimiwa Spika, msajili analo jukumu la kuhakikisha daftari linakuwa na taarifa sahihi na za uhakika na Sheria ya

Kampuni imempatia mamlaka msajili kufuta kampuni yoyote ambayo wakati wa usajili iliwasilisha taarifa za uongo.

Mheshimiwa Spika, msajili anaendelea na zoezi la upekuzi wa taarifa zilizomo kwenye daftari la kampuni ambapo zoezi hili ni endelevu kwa lengo la kuhakikisha kampuni zisizokidhi vigezo zinaondolewa zote. Katika zoezi hilo msajili alibaini kuwa *Chalinze Cement Company Limited* iliwasilisha taarifa za uongo wakati wa usajili, kama ifuatavyo:-

Moja; anuani ya kampuni iliyosajiliwa haipo kwenye usajili popote pale ndani ya Taifa hili. Kwa hiyo, kwanza anuani ya kampuni ni ya uongo kwa hiyo, ukitaka kumfikia huwezi kumfikia, yuko wapi.

Pili; anuani za wana-hisa alizozisajili hazipo kwenye sajili zozote ndani ya Taifa letu. kwa hiyo, nayo pia hata hao wanahisa ni wa kufikirika.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ya simu ya mkononi yaliyosajiliwa kwetu sisi si ya mwanahisa aliyetajwa kwenye usajili huo. Aidha, kwa mujibu wa sheria msajili alitoa *notice* ya kusudio la kufuta Kampuni ya *Chalinze Cement Company Limited* ambapo wakurugenzi wake walipewa siku 30 kuanzia tarehe 19 Januari, 2023 kuwasilisha maelezo kwa nini kampuni hiyo, isiondolewe kwenye daftari la kampuni kwa kuwasilisha taarifa za uongo wakati wa usajili.

Mheshimiwa Spika, baada ya siku 30 zilizotolewa kumalizika bila ya Wakurugenzi kutoa maelezo yoyote, Msajili aliendelea na hatua inayofuata kwa mujibu wa kifungu cha 400A(3) cha Sheria ya Kampuni na kuifuta *Chalinze Cement Company Limited*. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba waelewe dhamira njema ya Serikali yetu. Tunahitaji wawekezaji, lakini wawe wale wenye

dhamira njema na Taifa letu, siyo wawekezaji wanaokuja kutuchezea Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunabaki na orodha ya makampuni mengi ambayo hayapo, makampuni hewa, lakini kibaya zaidi taarifa zote alizozisema wakati anasajili ni za uongo. Kwa hiyo, naomba hilo Watanzania wajue, mtu huyu alishughulikiwa na sheria iliyotungwa na Bunge hili hili Tukufu, hakuna sehemu yoyote ambapo Serikali ilikosea.

Mheshimiwa Spika, jambo la *Tanga* na *Twiga Cement;* nimepokea maelekezo ya Bunge lako na kama utaridhia, sisi kama Wizara tuko tayari kutoa semina kwa Wabunge wote kuhusu utendaji wa Tume ya Ushindani pamoja na Baraza la Ushindani la Taifa ili sote kwa pamoja tuwe na uelewa wa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hoja na Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema 23, zaidi ya asilimia 50 ya Wabunge waliochangia hotuba ya bajeti hii kuhusu jambo hili na ilianza kuambiwa kwa nini *FCC* imeruhusu. *FCC* ndugu zangu ni Tume yetu ya Ushindani; kwa nini imeruhusu muungano wa Kampuni za *Twiga Cement* na *Tanga Cement* ambazo hapo awali ulizuiwa na Baraza la Ushindani.

Mheshimiwa Spika, jibu sahihi la hoja hii kwa Waheshimiwa Wabunge ni kwamba Tume ya Ushindani haikushughulika na ombi la muungano wa kampuni mbili ambao ulizuiwa na Baraza la Ushindani; hilo ni jibu la kwanza. Haikushughulika na ombi lile lililozuiwa na Baraza la Ushindani. Tunaheshimu sheria zote za nchi hii na hasa zile mimi Waziri wa Uwekezaji niliyebeba Katiba ya Taifa letu, nikabeba kitabu kitukufu kuapa, nimeapa kuzilinda na nitazilinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilichofanyika na Wizara yetu inapenda kusema na kulijulisha Bunge letu Tukufu kwamba mnamo tarehe 22 Desemba, 2022 *Scancem International DA* ambayo inamiliki asilimia 69 pale *Twiga Cement* ilileta ombi la kununua asilimia 68.33 ya hisa za *AfriSam Mauritius* ndani ya Kampuni ya *Tanga Cement*.

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Desemba, 2022 ndiyo tulipokea maombi hayo. Taratibu zote za kisheria zilifuatwa katika kuwasilisha na kuchambua ombi hili. Kwa mujibu wa kifungu cha 11(2) cha Sheria ya Ushindani kinachosomeka sambamba na Kanuni ya 33 ya Kanuni za Ushindani za Mwaka 2018 na Kanuni ya 2(1) ya Kizingiti cha Uwasilishaji wa Maombi ya Miungano ya Makampuni za Mwaka 2017 *(The Threshold for Notification of a Merger)* kinatoa wajibu kwa kampuni ambazo zinataka kuungana na zimekidhi vigezo vilivyowekwa chini ya vifungu tajwa hapo juu kuwasilisha maombi yao bila kujali kama kusudio lao la awali lilikataliwa au kukubaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vigezo hivi ni pamoja na ununuzi wa hisa au mali za kampuni inayonunuliwa, kizingiti cha mtaji wa kampuni zote mbili kama unafikia au kuzidi kiasi cha shilingi bilioni 3.5 na kubadilika kwa uwezo wa kiutawala *(change of control)* imebadilika?

Mheshimiwa Spika, hivyo napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, ombi hili lililoruhusiwa ni ombi jipya kutokana na vifungu nilivyovitaja kabla, ni ombi jipya ambalo tulilipokea kwa barua yenye kumbukumbu namba *CDC127359/144* lililotolewa mbele ya Tume ya Ushindani kwa kuzingatia takwimu za hali ya soko la saruji kwa mwaka 2022. Kwa sababu ombi hili tulilipokea mwaka 2022 hatukuwa na sababu ya kutumia takwimu za mwaka 2020, tutatumia takwimu za mwaka 2022. Natamani sana Watanzania watuelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi hili jipya lililoruhusiwa na Tume yetu ya Ushindani ni tofauti na lile la awali lenye kumbukumbu Na. *CDC127359/136* lililowasilishwa tarehe 2 Novemba, 2021. Kwa hiyo, tuna maombi mawili; la kwanza la mwaka 2021 na ambalo lilitumia takwimu za Desemba, 2020 kwa sababu hatukuwa na takwimu nyingine katikati hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, ombi hili lililowasilishwa tarehe 2 Novemba, 2021, liliruhusiwa kwa masharti tarehe 6 Aprili, 2022 kwa kuzingatia kigezo cha uwezo uliosimikwa. Amelieleza vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri Patrobass Katambi, kisheria maana yake nini.

Mheshimiwa Spika, tuliruhusu kwa sababu utawala wa soko wa kampuni mbili zilizoomba kujiunga kutumia *installed capacity* ulikuwa unafikia asilimia 31.53 ambazo ni chini ya asilimia 35 ambayo ni *threshold* ya mwisho ya kuruhusiwa kwa kampuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na sheria inavyosema, haijasema tutumie *installed capacity* wala *sales volume,* kwa sababu Sheria ya Tume ya Ushindabni is an *economic act* (sheria ya kiuchumi). Sheria ya kiuchumi ina-*deal* na *behaviour* za wateja wake walioko kwenye eneo lile lililopo, *it's a behavioral act,* inabadilika wakati kwa wakati. Wamesema vizuri Wabunge kwamba mazingira yanabadilika na yalibadilika kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa nini *FCC* waliamua ombi ambalo lilizuiwa na *FCT* hapo mwanzo? Nimeshalieleza wazi, ombi tulililoamua ni jipya kabisa, wala siyo lile la zamani.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa taarifa kwamba mchakato wa kupokea, kuchambua na kutoa maamuzi ya muungano wa kampuni kama nilivyosema unaongozwa na nadharia za kiuchumi na kibiashara. Nadharia hizi na viashiria

vyake, *market variables,* lazima viangaliwe na hivyo basi, kutokana na ukweli huu, viashiria kutoka mwaka 2020 mpaka mwaka 2022 vilibadilika na hapo tunatoa picha kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba hata huko nyuma imewahi kutokea ndani ya Taifa letu, kampuni ziliomba kuungana kwa mazingira ya kwanza wakanyimwa kwa sababu mazingira hayakuwa yanaruhusu na waliporejea mazingira yakawa yanaruhusu na wakaruhusiwa kuungana, nayo wala siyo miaka mingi iliyopita.

Mheshimiwa Spika, *FCC* mnamo tarehe 10 Juni, 2021 iliendelea kuzuia ombi la Kampuni ya *Toyota Tshusho,* zote ziko ndani ya Taifa letu kuinunua Kampuni ya *CFAO Motors* kama ambavyo ombi hilo lilivyozuiliwa na *FCC* na baadaye kuafikiwa na Baraza la Ushindani *(FCT)* mwaka 2013. Ya kwanza ilikuwa 2012 na sasa ni 2013, wakaruhusiwa ndani ya Taifa letu kupitia Tume ya Ushindani na Baraza la Ushindani hili hili ambalo tena leo tunasema watumishi wetu wamekwenda ndivyo sivyo na Waziri wamenisisitiza nisimamie haki na niliapa kusimamia haki na nitaisimamia.

Mheshimiwa Spika, siyo ndani ya Taifa letu tu, Nchi ya Afrika Kusini ambao wote tupo kwenye *SADC,* mwaka 2019 ilizuia muunganiko wa *Africa Forest Fund Limited* na *Guka Forest Holding* kwa sababu mazingira wakati huo mwaka 2019 hayakuwa yanaruhusu. Mwaka 2021 kampuni zilezile zikaomba kuungana kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya uchumi ndani ya Taifa na mwaka 2021 baada ya mamlaka za ushindani nchini Afrika ya Kusini kuridhika na mabadiliko na muundo wa soko, kampuni hizi mbili ziliruhusiwa. Kwa hiyo, siyo jambo jipya, ni jambo ambalo lipo kwa majirani zetu, ni jambo ambalo lipo ndani ya Taifa letu na kilichofanyika ni kitu cha kawaida kabisa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingi kwenye jambo hili, naomba niseme tu kidogo, maana yake imesemwa pia kwamba hakukuwa na uwazi kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja hii ya kutokuwa na uwazi katika ununuzi wa hisa za *AfriSam Mauritius* ndani ya Kampuni ya *Tanga Cement,* napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mara baada ya ombi hilo kuletwa Tume ya Ushindani ulifanyika mchakato wa uwazi ambapo kwa mujibu wa Kanuni ya 49 ya Kanuni za Ushindani za Mwaka 2018 tunatakiwa kutoa tangazo kwa Taifa na kwa dunia kwamba kuna mchakato huu unaendelea.

Mheshimiwa Spika, tangazo hilo tulilitoa kwenye magazeti ya *Daily News* na Habari Leo ya tarehe 11 Februari, 2023 ili kuutaarifu umma juu ya jambo hili tena kwamba tumeanza nalo. Hatukupokea malalamiko kwa yeyote na kikao cha wadau ambacho kilihusisha kampuni zote za uzalishaji saruji ndani ya Taifa letu, taasisi ya kuwatetea walaji ndani ya Taifa letu walikuwemo kwenye kikao, hawakupinga wakasema wameridhika mchakato uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyo anayekuja kinyumenyume nani? Siri yake ni ipi? Kwa nini asiiseme wazi basi tukajua? Wakati haya yote yakiendelea, nimewahi kuwaandikia barua hawa *Chalinze Cement,* mimi mwenyewe Waziri kwamba, nataka kwenda kuwatembelea kwenye kiwanda chenu. Mpaka leo sijawahi kupata jibu niende au nisiende. *Chalinze Cement* ni nani? Ni mdudu gani ndani ya Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Chalinze Cement* amesajiliwa baada ya ombi la kwanza la Twiga na Tanga kuungana, hakuwepo huko nyuma. Tumefanya kikao cha wadau, *Chalinze Cement* hakuwepo. Tumemaliza michakato yote anaibuka kuja kusajiliwa na sisi kama ilivyo jukumu letu la kusajili tukamsajili, si mtu ameleta

*documents,* ametuletea tumemsajili. Sasa tumfuatilie, Waziri mwenyewe nimemwita, kama hutaki nije kwako njoo tuongee, niletee malalamiko yako. Mpaka hapa nilipo hajawahi kuja kwangu. *(Makofi)*

*Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenye dhamira njema ya kulinda jitihada za Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuita wawekezaji kutoka nje na kuwalinda wawekezaji wa ndani ambao tayari walishawekeza; nawashukuru sana. Wapo walioniambia na wengine wamenionesha mpaka picha ya watu hao wakizunguka kwa Wabunge kuwaeleza wasaidie kupinga jambo hili. (Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

*Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge tuchukue tahadhari ya hali ya juu na watu wasiolitakia mema Taifa letu. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana kui-brand Tanzania. Wawekezaji wengi wanakuja, nimesema kwa mwaka mmoja tuna wawekezaji 240, hawakuwahi kutokea katika historia ya miaka 60 ya Taifa letu, yametokea sasa, tusitumike.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, kuna watu ambao wanataka kusimama mbele ya Mheshimiwa Rais kumwambia hapana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais amesema hapana na mimi nimeapa kulinda sheria zote zilizopo ndani ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na nitasimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie *podium* hii kumwomba *Chalinze Cement* aje tumsaidie. Tunajua yako mengi yaliyowakwamisha wenzake, sasa aje tumsaidie kama kweli anataka kuwekeza ndani ya Taifa la Tanzania. Mimi niko tayari, wasaidizi wangu wote wako tayari, waje tuwekeze kwa pamoja na tuwahudumie Watanzania wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, naomba kuhitimisha kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupitia kwao, nimesimama mbele yao najiamini ni mzalendo na naiamini imani yangu, nimeapa kulinda Katiba ya Taifa hili, nimeapa kulinda sheria zinazoongoza Wizara ya Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana mtupitishie bajeti ya Wizara yetu kwa mwaka 2023/2024, ili tuendelee kulinda jitihada za Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuita wawekezaji, kuwawezesha wafanyabiashara wetu na hatimaye Taifa letu liweze kuhudumia Afrika kutoka hapa tulipo, liweze kuhudumia dunia kutoka hapa tulipo. Uwezo huo tunao chini ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na utaratibu wetu. Kanuni ya 34(6) inasema iwapo wakati wa kusitisha shughuli umefika na Spika atakuwa analihoji au yupo karibu kulihoji Bunge, basi hatasitisha shughuli mpaka hoja iwe imeamuliwa.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

## KITABU CHA PILI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 44 - Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 44, ukurasa 404, katika Kishkwambi, fungu hili linapatikana katika ukurasa wa 43.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mmeshafika hapo kwenye vishkwambi? Katibu tuendelee.

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*..................................Sh. 15,513,381,832

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri, na yako majina ya Waheshimiwa Wabunge hapa wanaohitaji ufafanuzi wa suala mahususi na ya kisera. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi. Ni ukweli usiopingika kwamba viwanda vingi, zaidi ya asilimia hamsini vimekufa. Tulitegemea kabisa kwamba mbadala wake ungekuwa shirika letu la SIDO ambalo limekuwa likifanya kazi nzuri toka lilipoanzishwa. Kusema kweli *SIDO* ni shirika ambalo likisimamiwa vizuri kwanza linawasidia sana

wale wananchi ambao ni wadogo wadogo kwa kuongezea thamani bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika speech yote ya Mheshimiwa Waziri na vile vile katika majibu yake, hakuna mahali alipoonesha kwamba sasa Serikali inaweka nguvu zake kwenye SIDO ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu. Nilitaka Mheshimiwa Waziri atueleze, kuna mikakati gani mahususi ya kuhakikisha kwamba tunaisaidia *SIDO* ili iweze kusaidia wananchi wetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nimshukuru Mheshimiwa Vedastus kwa hoja yake hii njema kabisa ya kutaka kuona tunaweza kulisaidia Taifa letu kupitia viwanda na hasa kuliwezesha Shirika letu la *SIDO* kuweza kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina dhamira ya dhati kabisa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Manyinyi kwamba hata viwanda vile ambavyo vilifungwa kwenye hotuba yangu nilieleza wazi, tayari tunaanza mchakato. Kwa viwanda vile 28 vilivyokuwa vimerejeshwa Serikalini, tayari tumeshatangaza Viwanda tisa ili tuweze kupata wawekezaji wengine waweze kuwekeza nasi. Viwanda vinne, kwa dhamira njema ile ile ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumewaita wawekezaji wale wale kwa sababu walinesha dhamira, na sasa wameleta mipango kazi mipya, tunawasimamia kati ya Wizara yetu na Wizara ya Fedha ambayo ndiyo ina Msajili wa Hazina ili viwanda vile tuvisimamie sasa viwe na mipango mizuri ya kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya, Serikali yetu ina dhamira njema kabisa, ndiyo maana tumeongezewa bajeti. Mwaka jana 2022 tulikuwa na bajeti chini ya shilingi bilioni 100,

mwaka huu tuna bajeti ya shilingi bilioni 119 ndani ya Wizara yetu. Moja ya taasisi tunayoipa nguvu ni *SIDO* ili iendelee kuwawezesha wenye viwanda vidogo vidogo na wafanyabiashara wetu ndogo ndogo ili wawekeze na tuwawezeshe mashine. Pia tuna mfuko pia ule wa kukopesha ulioko chini ya *SIDO* pamoja na mpango ule tunaoshirikiana na taasisi ya *Azania Bank* na sasa tunashirikiana na Benki ya *CRDB* kuwawezesha watu wetu wapate mikopo ya riba ya chini ya asilimia tisa ili waweze kuwekeza kwenye viwanda kupitia usimamizi wa *SIDO*. Kwa hiyo, inawezekana kabisa, na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alionesha dhamira yake njema ya kushirikisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunahusisha benki ya Azania, benki yetu ya *CRDB* kwa riba ndogo ya asilimia tisa, pamoja na ile fedha ambayo tunapewa na Serikali ya shilingi bilioni moja kila mwaka kuwawezesha wenye viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Manyinyi aweze kuridhika na maelezo haya ili atuachie tukasimamie sasa mipango hiyo na tuweze kuwawezesha wenye viwanda vidogo. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana, naona Mheshimiwa Manyinyi ameketi, kwa hiyo, ameridhika. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tena kwa kunipatia nafasi. *Actually,* sikutamani nisimame tena, nilitegemea Mheshimiwa Waziri kwa kuwa ni mara ya pili nasimama nikiwa na hoja hiyo hiyo ya kuendelea kutetea bidhaa zetu ambazo zinazalishwa ndani, nilitegemea kwa uzito huo huo naye angesimama kusema namna ambavyo anaheshimu ubunifu ambao unazalishwa na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosimama hapa, ametoa majibu mepesi mepesi tu ambayo unaona kabisa hayana tija na tuone hata kama tuna lengo la kutaka kusaidia bidhaa zetu ambazo zinazalishwa ndani ziendelee kupata thamani ili zifanane na hizo ambazo tunaletewa kutoka Mataifa ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati wanawasilisha, miongoni mwa ushauri ambao Kamati waliutoa, walikuwa wamesema, wanatamani kuona bidhaa zetu ambazo zinazalishwa ndani, hususan zile za chakula zinapewa kipaumbele ili zitumike ndani na tuweze kutoa nje. Sasa kama pombe za kienyeji ni chakula, lakini pombe ambazo zinatoka nje pia ni chakula, ndiyo ziko ndani humu kwetu, zimejaa nchini kwa wingi kuliko pombe zetu ambazo watu wetu wanatengeneza: Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha pombe za Watanzania hawa zikitengenezwa, na zenyewe ziende nje kwa wingi kama ambavyo sisi tunatumia pombe zao, nasi tuendelee kujipatia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea Mheshimiwa Waziri atasema kwamba tutaanza kufanya utafiti na watu ambao wanahusika na utafiti ili watusaidie hata namna ya kuifanya gongo iwe halali kwa kuitoa ile methanol ambayo iko kwenye gongo. Pia labda waje na mkakati kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na yeye amekuja…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester hoja yako ni nini ambayo unayotaka ufafanuzi?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba Mheshimiwa Waziri bado hajaji-*commit* kuona kweli anataka kuboresha pombe za kienyeji ziweze kufanana na pombe ambazo tunaingiziwa kutoka Mataifa ya

mbali. Kama ni ndivyo, basi na pombe zinazotoka huko zizuiliwe kuingia nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi. Nisiporidhika, nakusudia kukakamata shilingi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa sababu hoja hii ni mara ya pili kama alivyosema mtoa hoja, na kwa niaba ya Waziri, nitoe ufafanuzi kidogo wa kina kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, Serikali iko kwenye maandalizi kwanza ya kuwa na Sera ya Taifa ya Ushiriki wa Watanzania katika Kuendeleza Uchumi kwa maana ya *local content*. Pili, kwenye suala hili la pombe, kama nilivyosema mwanzo, kwa mujibu wa viwango vya pombe kali; pombe kali inapaswa kuwa na *ethanol* kuanzia asilimia 37 mpaka 42 na hii haipaswi kuwa na kiwango kikubwa kwa sababu zina madhara ya kiafya. Moja, ikiwa zaidi ya hapo inasababisha upofu, na pili, inaweza kupelekea hata kifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tumeshaanza kufanya kazi ya ziada kuhakikisha tunahamasisha uzalishaji wa pombe hizi zifikie viwango. Kwa kupitia shirika letu la viwango vya ubora wa pombe za kienyeji ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango ambacho kimeshawekwa, nilisema mwanzo, moja ya pombe ambazo zimeshahalalishwa ni zile zinazotokana na Lozera, ulanzi na pombe zinazotokana na nafaka, mfano pombe zitokanazo na ndizi, mfano ile Rubisi kule Kagera tayari imeshapitishwa, na nyingine zinazotumia matunda na mizizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna pombe za kienyeji zinazotokana na nafaka. Mfano, Kibuku, Mbege, Nakayoga na pombe nyingine. Pamoja na kutokukidhi mahitaji mengine kwa mujibu wa viwango, pombe hizi zinazozalishwa kwa njia zisizo halali kwa maana ya teknolojia inayotakiwa, kuna kiwango cha juu sana cha *ethanol* na *methanol* ambayo hiyo huhatarisha afya kama nilivyosema. Kwa hiyo, Serikali…

**MWENYEKITI:** Sawa. Mheshimiwa Naibu Waziri, hoja nafikiri ni kwamba, wale watu wanaotengeneza, ile ile teknolojia wanayoitumia, Serikali ina mpango gani wa kuboresha ile teknolojia kule kule waliko ili ile pombe wanayoizalisha isiwe na hiyo sumu ama isiwe na viwango vikubwa ambavyo vinaleta athari? Ndiyo hoja iliyopo mezani. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nitoe taarifa katika Bunge lako tukufu, kwamba Wizara kupitia *SIDO* na *TBS* hadi kufikia Oktoba, mwaka 2022 tumetoa leseni jumla 43 za ubora kwa bidhaa mbalimbali za pombe za kienyeji. Tumeshaanza hatua na tuna maombi mengine mapya kama 22 ambayo yako katika hatua mbalimbali kuelekea kupata ithibati ya ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeshaanza kuwasaidia huko huko wazalishaji ambao wanazalisha bidhaa hizi au vinywaji hivi kwa njia ya kienyeji. Kwa hiyo, Serikali tunahakikisha kupitia Shirika letu la Viwango Tanzania tutaendelea kutengeneza viwango vya pombe za kienyeji kwa kadri ya mahitaji yatakavyojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikuhakikishie na nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali tunatambua jitihada mbalimbali za wazalishaji ambao wanazalisha na kujikwamua kiuchumi kupitia pombe za kienyeji. Kwa hiyo, tutaendelea kuwasaidia ili wazalishe kwa ubora kwa kuwapa

teknolojia sahihi na elimu na kuwawekea mazingira wezeshi kwa maana ya mazingira ya kuzalisha na teknolojia ambazo zinatakiwa ili wazalishe pombe ambazo hazitakuwa na madhara kama ambavyo tumekuwa tukiona kwenye sehemu ambazo zinazalishwa bila kufuata utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Mheshimiwa Condester naona ameketi, kwa hiyo, ameridhika na majibu. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa sababu hoja hii imesharejea hapa mara kadhaa, nadhani hicho ulichosema hapo mwishoni kwamba mtawapelekea teknolojia, lakini sasa pia mfanye utafiti, kwa sababu katika bajeti hii tunayopitisha leo, sioni kiasi kikubwa cha pesa cha kuweza kuwawezesha ninyi kuwasaidia wale wote wenye huo uhitaji. Kwa hiyo, kinachohitajika ni ile teknolojia wanayoitumia wao, wafanye utafiti hao wanaohusika; hao wa *TBS,* sijui na nani, namna ya kuvishusha vile viwango. Ile ile teknolojia anayoitumia yeye mwenyewe, maadam anachozalisha ni pombe, na inalevya, ipunguze kile kiasi. Wakati ninyi mnajipanga na teknolojia bora, mtengeneze mazingira ya kumpa hicho ambacho kitapunguza ukubwa ama wingi wa hicho ambacho mnasema kina athari, kwa sdababu hamtaweza kuwafikia wananchi wote wanaojishughulisha na hii biashara kuwapelekea teknolojia. Kwa hiyo, nafikiri hilo linaweza kuwa limemweka katika mazingira mazuri Mheshimiwa, atakuwa anasubiri mwakani, sijui atakuja na hoja nyingine nadhani kushukuru namna ambavyo mmepiga hatua. Ahsante sana.

Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest.

**MHE. ANATROPIAL L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Tanzania ni moja kati ya nchi 44 zilizoridhia mikataba ya eneo huru la biashara Afrika *(Africa Continental Free*

*Trade Area)* ambayo mpaka mwaka 2022 ilikuwa imesha-*ratify* na ku-*deposit document* za kufanya kazi. Licha ya Tanzania kuridhia kuwa eneo huru la kibiashara, ina maana Tanzania inapaswa kufanya biashara na mataifa mengine. Tanzania hiyo hiyo inatajwa kama nchi ya 141 katika hizo *big business out of* nchi 190. Ina maana haifanyi vizuri kwenye maeneo mazuri ya kufanyia biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua *commitment* ya Wizara, ni namna gani wamejiandaa kuwaandaa Watanzania ili waweze kushiriki hili soko la kufanya biashara kama tulivyoridhia? Kama sitaridhika, nitatoa shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii. Namshukuru Mheshimiwa Anatropia kwa hoja yake hii. Ni kweli, sisi ni kati ya nchi 44 ambazo tumeridhia mkataba huu wa Biashara ya Eneo Huru la Biashara Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa kwamba Tanzania ni moja kati ya nchi saba ambazo zimepewa upendeleo wa kupeleka bidhaa zake mapema kabisa kati ya hizo nchi 44. Upendeleo huu hatukupewa bure, ni kwa sababu tumefanya kazi kubwa ya kuwaandaa Watanzania kuliendea soko hili la Eneo Huru la Biashara Afrika. Maana yake tuliletewa viwango vya kufikia na tukafikia na tukawa ndani ya nchi saba kati ya hizo nchi zote ambazo zimeridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mwaka 2022 mwezi wa tisa, kongamano kubwa la wanawake na vijana Afrika kunufaika na fursa hizi za Eneo Huru la Biashara Afrika lilifanyika Tanzania. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndio

*champion* wa biashara hii hasa itakayofanywa na wanawake na vijana kwa Afrika nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejiandaa vyema. Ndani ya hizo nchi saba, sisi kama Taifa tumeshafanya vikao vingi na sekta binafsi ya kwetu na sasa tuko tayari. Kwenye hotuba yangu nilitaja moja kwa moja kwamba mwezi wa Saba tarehe 01, mpaka sasa tunapeleka bidhaa sita ambazo ziko tayari kupelekwa kwenye soko hili la Eneo Huru la Biashara Afrika. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Anatropia aniachie shilingi yangu ili niendelee kukaa na wafanyabiasha wetu wenye viwanda ili tuweze kulifikia soko hili. Ndiyo maana hata huu mchakato wa Twiga na Tanga, moja ya bidhaa tunayotamani tuiuzie Afrika ni hii ya saruji. Ndiyo maana tunatatuta wengi wawekeze nasi, tuwawezeshe waliopo, ili tuihudumie Afrika kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia ameketi kuashiria ameelewa maelezo ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*………….Sh. 530,924,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*…………….Sh. 1,268,150,000
Kifungu 1004 - Government Communication Unit….Sh. 243,856,000
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*…..…………………...Sh. 231,716,000
Kifungu 1006 - *Legal Services Unit*…….………………..Sh. 248,921,000
Kifungu 1007 - *Management Information System*…..Sh. 386,268,000
Kifungu 1008 - *Procurement Management Unit*…….Sh. 292,293,250
Kifungu 2001 - *Industry*………………………………..Sh.11,599,248,087
Kifungu 2002 - *Small and Medium Enterprises Division*…............Sh. 0
Kifungu 3001 - *Commerce*…………………....…….Sh. 1,511,729,000

Kifungu 4002 - *Commodity Market Development*................................Sh. 27,912,089,129
Kifungu 5001 - *Investment Development Division*..............................................Sh. 3,279,868,051
Kifungu 5002 - *Economic Empowerment and Private*..............................................Sh. 11,717,921,151
Kifungu 5003 - *Business Environment Unit*……………..Sh. 307,360,000
Kifungu 6001 - *Research and Innovation Unit*............Sh. 407,768,500

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahamia Kitabu cha Nne – Matumizi ya Maendeleo. Fungu 44, ukurasa wa 100 na kwenye Kishkwambi inapatikana ukurasa wa 99.

## KITABU CHA NNE

## MIPANGOI YA MAENDELEO

### Fungu 44 – Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*...................................Sh. 1,700,000,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kwa muda uliobaki hapa tunawapitisha mafungu.

Katibu.

Kifungu 1003 - *Policy and Planning*...........................Sh. 8,500,000,000
Kifungu 2001 - *Industry*.............................................Sh. 16,304,819,000
Kifungu 2002 - *Small and Medium Enterprises Division*................Sh. 0
Kifungu 4002 – *Commodity Market Development*….Sh. 200,000,000

Kifungu 5002 - *Economic Empowerment and Private Sector Development*....................................Sh. 3,642,000,000
Kifungu 5003 - *Business Environment Unit*…………Sh. 13,219,685,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.  Mtoa hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake. Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono sasa nitawahoji.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Bunge limemaliza kazi yake. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kusema kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hii ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, yamepitishwa rasmi na Bunge kwa mwaka wa fedha 2023/2024. *(Makofi)*

Nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri,Katibu Mkuu na Wasaidizi wote unaofanya nao Kazi tunawapongeza kwamba Bunge limeweza kupitisha makadirio ambayo mliyaleta mbele yake na tunawatakia kila la heri katika utekelezaji kwa yale ambayo mmewaahidi Wabunge katika kuyafanyia kazi yale ambayo wamewashauri na pia yale ambayo mmeyaahidi tunawatakia kila la heri kwenye kuyatekeleza.

Waheshimiwa Wabunge, pia niishukuru sana Kamati yetu ambayo imefanya kazi kubwa sana. Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wote wa Kamati hii mmefanya kazi kubwa ya kuisimamia wizara hii lakini pia kuishauri. Ndio maana wakisoma hapa bajeti yao wameeleza namna ambavyo mmeshirikiana vizuri na wamepokea ushauri wenu. Kwa hiyo, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge.

Pia wapo Wabunge ambao sio sehemu ya hii Kamati na wao wamepata nafasi ya kuchangia mawazo mbalimbali, naamini yatawasaidia Wizara hii kuendelea kufanya kazi vizuri zaidi. Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri Wizara katika kuyafanyia kazi yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza.

Waheshimiwa Wabunge, mambo mawili mafupi halafu tangazo. Mambo mawili wakati Mheshimiwa Condester Sichalwe akichangia alizungumza kwenye mchango wake kuhusu ubora ama udhaifu wa bidhaa kutoka China. Sasa kwa namna alivyozungumza na kwa sababu muda wake ulikuwa mfupi na

taarifa zikawa nyingi kidogo nikashindwa kumpa fursa kwa wakati huo.

Sasa ule mchango kwa namna ulivyosemwa, kwa ajili ya kulinda mahusiano yetu na Nchi ya China, isije ikaoneka kwamba pengine wamesemwa humu wale wanaotengeneza bidhaa huko kwamba pengine hazina ubora ama zina sura fulani hivi. Kwa hiyo, mchango huo wa Mheshimiwa Condester Sichalwe, kwenye hilo eneo la ulinganifu wa ubora au udhaifu wa biashara, unaondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo la pili ni kuhusu jambo ambalo limejitokeza kwa ukubwa sana hapa Bungeni na kwa hivyo Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu Serikali imetoa maelezo kwa kirefu na pia Mawaziri wamechangia zaidi ya mmoja kuhusu hoja hiyo. Nafikiri ni muhimu kuweka sawa ili isije ikaonekana Bunge limeingia kuwa sehemu ya huu mchakato na hata Serikali ambapo imetoa maelezo ya ziada humu ndani ni kwa ajili ya kuwapa ufahamu wale Waheshimiwa Wabunge waliochangia.

Kwa hiyo, isije ikatokea mahali pengine jambo limeenda kwa namna hii kwa namna ile, halafu Bunge linapaswa kufanya kazi yake au Kamati inapaswa kufanya kazi yake ikaonekana kuna mahali Bunge limeshiriki kwenye mchakato. Huu mchakato ni wa Serikali na mchakato huu viko vyombo vya Serikali vinavyosimamia na Wizara inayohusika kuhusu hili jambo lililochangiwa la muunganiko ama kuungana kwa *Twiga Cement* na *Tanga Cement*. Kwa hiyo, lieleweke hivyo Bunge sio sehemu ya mchakato na Kamati yetu ukiisoma taarifa yake hilo jambo halimo. Hata hivyo, kwa sababu Wabunge wamepata taarifa huku na kule, kokote walikozipata wasingeweza kuzuiwa kusema kwa sababu ushauri unaruhusiwa kwa ngazi hii. Sasa Serikali inafanya nini na huo ushauri? Bunge litakuwa halijashiriki kwa

sababu hilo jambo halijaletwa Bungeni kwa utaratibu unaotakiwa kwamba Bunge liamue ama Bunge lishauri. *(Makofi)*

Kwa sababu, ili Bunge lifikie mahali kwamba tumeishauri Serikali hivi, lazima jambo lipite kwa utaratibu tulionao, lipite kwenye Kamati, liletwe hapa na wao wawe wamelichakata. Ndio maana Bunge lina sehemu yake ya kuishauri Serikali na kwenye kipindi hiki ambacho tunatazama Makadilio ya Mapato na Matumizi, tunaishauri Serikali, hautuisimamii. Pia, tunaishauri kwa kuongozwa na Kamati yetu inasema nini. Kwa hiyo, yale ambayo Kamati imeyasema humu na Wabunge mmeyachangi Serikali inaenda kuyafanyia kazi. Haya mengine ambayo tumechangia kwa kila mmoja kwa kadri Serikali itakavyoona inaweza kuyafanyia kazi, itaenda iyafanyie kazi.

Sasa, tusije tukapeleka picha fulani kwamba jambo kama hili lilishapita Bungeni, limejadiliwa, Waziri kasema, Mbunge fulani kasema, Bunge halijasema chochote kuhusu jambo hili. Kwa sababu, ili tuwe tumesema chochote lazima tuwe tumehojiwa kuhusu jambo hilo na linatoka kama Maamuzi ya Bunge. Kwa hiyo, nimeona hilo ni muhimu sana lieleweke ili lisije likaleta picha ambayo sio.

Waheshimiwa Wabunge, Vivyo hivyo, ujumbe utakaokwenda kwa wawekezaji wetu Waheshimiwa Wabunge hatukuwazuia kwa sababu katika ngazi hii hoja haiko mbele ya Bunge kimsingi kwamba tunataka kufanya maamuzi fulani. Kwa hiyo, hata wawekezaji wawe na uhuru tu yale yanayosemwa humu ndani, Wabunge wanaruhusiwa kuishauri Serikali lakini isije ikaonekana mahali pengine wawekezaji wanaanza kujadiliwa Bungeni halafu ndio Serikali ikafanye maamuzi. Ni kazi ya Serikali kufanya. Sisi litakapokuja kwetu tutalifanyia kazi kwa utaratibu ule ambao tumejiwekea, Kikatiba, Kisheria na Kikanuni. Nadhani hapo nimeeleweka vizuri.

Kwa hiyo, tunawatakia heri katika yale yote ambayo Serikali mmeeleza hapa. Tunawatakia heri na ikiwa yapo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia na mnaona mnaweza kuyafanyia kazi, yachukueni hayo mkayafanyie kazi. Yale ambayo mnaona Waheshimiwa Wabunge wamechangia lakini mngependa mchukue hatua tofauti na Wabunge walivyochangia ni haki yenu kikatiba kufanya kazi hiyo, kwa sababu ni kazi ya Serikali. Litakapokuja kwetu tutakapokuwa tunaisimamia Serikali pengine hapo Bunge sasa litaweza kusema na kufanya kazi yake ambayo inatakiwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.32 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 8 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*